

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 13 Juni, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Yustino Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Tukae. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali tunaanza na TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe. Mheshimiwa Hongoli!

Na. 374

**Mahitaji ya Kidato cha Tano – Shule ya Sekondari Lupembe**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Lupembe iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni ya muda mrefu na tulishaomba na kufanya maandalizi ya kuwa na Kidato cha Tano kwa Mchepuo wa *CBG*.

Je, ni lini Serikali itaanzisha Kidato cha Tano katika Shule hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Lupembe ni miongoni mwa shule mpya 22 ambazo zimeombewa kibali Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili iweze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano katika mwaka 2017. Hivyo, shule hiyo itaanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano baada ya kupatikana kwa kibali kilichoombwa kufuatia ukaguzi wa miundombinu ya shule iliyofanyika.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri na fupi kabisa. Mheshimiwa Hongoli Mbunge wa Lupembe swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa shule nyingi zimekuwa na matatizo ya kutokuwa na Walimu hasa shule zile za *A-level* zenye michepuo ya sayansi. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba shule hizi ambazo zina michepuo ya sayansi zinakuwa na Walimu wa kutosha ili wanafunzi hawa waweze kusoma vizuri na kuweza kumudu masomo yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa imekuwa ni kawaida kwa shule za Serikali kuongeza tahasusi kwenye shule hizi za *A-level* ambavyo huenda sambamba na ongezeko la wanafunzi. Katika shule hizi za *A-level* utakuta wanafunzi ni wengi na miundombinu haitoshi ukilinganisha na idadi ya wanafunzi. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba ongezeko la wanafunzi linaenda sambamba na ongezeko la miundombinu kwa maana ya madarasa, mabweni na miundombinu mingine? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli tahasusi ndio nini?

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Tahasusi ni *combination*.

**SPIKA:** Aaaa! Mheshimiwa Naibu Waziri, nilishindwa kumwambia Naibu ajibu maana yake Kiswahili Kongwa bado hakipo, Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na changamoto ya Walimu hasa wa sayansi katika shule zetu na ndiyo maana hapa katikati tuliomba kibali kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi na tulipata kibali cha kuajiri Walimu na Walimu wale sasa hivi tumewaajiri kuwapeleka sehemu mbalimbali. Hata hivyo, bado hatujaweza ku-*fill* hiyo *gaps* yote iliyonani na hii ni kutokana na jinsi hali ilivyo huko katika soko.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tutaendelea kufanya kila liwezekanalo, hivi sasa tuko katika mchakato kwa lengo kwamba tukipata wale Walimu wengine ambao maombi yao yalikuwa hayajakamilika vizuri, tuweze kuongeza kupeleka katika shule zetu ili tupate Walimu wa sayansi kwa ajili ya kufundisha vijana wetu wanaojiunga na kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili kuhusu suala zima la miundombinu, ni kweli tumeliona hilo ndiyo maana ukiangalia hivi sasa hata wanafunzi waliofaulu na kukidhi vigezo hatukuweza kuwachagua wote kutokana na suala la miundombinu, wengine tutawachagua katika *second selection*.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa hivi imeweza kufanya harakati na kupata takribani shilingi bilioni 21 ili kuweka miundombinu katika shule zipatazo 85, ambazo tunajua tukifanya hivi itasaidia sana kuhakikisha vijana wetu watafika shuleni na kusoma katika mazingira salama na mwisho wa siku waweze kupata elimu bora kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyokusudia.

**SPIKA:** Tunaelekea Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Ruth Mollel.

Na. 375

**Watumishi wa Umma Kupewa Motisha**

**MHE. RUTH H. MOLLEL** aliuliza:-

Serikali yoyote duniani inaendeshwa na rasilimali watu wenye weledi, ari na uzalendo. Ili Watumishi hawa wafanye kazi kwa moyo wanahitaji kuthaminiwa, kutambuliwa mchango wao na kupewa stahili zao bila bughudha:-

Je, Serikali imebuni mkakati gani wa kuwapa motisha na ari Watumishi wa Umma ili wafanye kazi kwa kujituma badala ya vitisho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kutoa maelezo kwamba utekelezaji wa shughuli za Serikali huendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayosimamia Utumishi wa Umma ambapo kila mtumishi hupaswa kuzingatia wakati wa kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Serikali haitumii vitisho wala bughudha katika kusimamia watumishi wake, bali husimamia sheria, kanuni na taratibu hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Watumishi wa Umma ni rasilimali ya msingi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo yake kwani nguvu na mafanikio ya Taifa lolote inategemea aina ya Watumishi lililonao na ni kwa msingi huo, Watumishi hawana budi kuendelezwa na kupewa motisha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kwa kutambua umuhimu wa motisha kwa Watumishi wa Umma, Serikali inayo mikakati

mbalimbali inayolenga kuongeza ari kwa Watumishi wa Umma na hivyo kuwawezesha kufanya kazi kwa weledi na kwa kujituma. Mikakati hii ni pamoja na:-

(i) Kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kwenye mshahara au *Pay As You Earn* kutoka asilimia 14 mwaka 2010/2011 hadi asilimia tisa mwaka 2016/17. Hatua hii imesaidia kuongezeka kwa kiwango cha mshahara anachobakinacho mtumishi baada ya kukatwa kodi.

(ii) Kuongeza kima cha chini cha mshahara kutoka Sh.100,000/= mwaka 2010/2011 hadi Sh.300,000/= mwaka 2015/2016 sawa na ongezeko la asilimia 200.

(iii) Kupitia Waraka Na. 3 wa mwaka 2011 unaohusu utaratibu wa kuwakopesha watumishi vyombo vya usafiri, Serikali imekuwa ikiwakopesha Watumishi vyombo vya usafiri ili kuwapunguzia adha ya usafiri wakati wa kwenda kazini na kurudi majumbani.

(iv) Kutoa dhamana kwa watumishi wakati wanapokopa fedha katika Benki na Taasisi mbalimbali za kifedha.

(v) Kuanzisha *Watumishi Housing Company Limited* kwa ajili ya kujenga nyumba za gharama nafuu na kuwauzia au kuwakopesha Watumishi ili waishi kwenye makazi yenye staha.

(vi) Kupitia sera ya mafunzo katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2013, Serikali imekuwa ikitumia rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya Watumishi wa Umma ili wawe na weledi wa kutosha.

(vii) Serikali imekuwa ikiratibu nafasi za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Watumishi wa Umma kutoka kwa nchi na wadau wa maendeleo kama vile Ubelgiji, Uholanzi, Australia, Jamhuri ya Korea, Ujerumani, China, Japan, India, Malaysia, Indonesia, Singapore, Sweden na Jumuiya ya Madola na nchi zinginezo.

(viii) Pamoja na Serikali kufanya zoezi la tathmini ya kazi kwa lengo la kubaini uzito wa majukumu ya Kada mbalimbali za Watumishi na hivyo kuwa msingi wa kupanga ngazi za mishahara. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/2018.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, nilikuona.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Waziri kwa majibu yake lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Tangu Serikali ya Awamu ya Tano ingie madarakani *annual increment* zimesimama na hata kwa bajeti hii ya mwaka huu, ya Waziri wa Fedha aliyoitoa juzi hakuna mahali popote tunaona kuna *increment* yoyote kwa ajili ya Watumishi wa Umma. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mishahara ya watumishi inaboreshwa ili waweze kupambana na hali ya uchumi na hali ya maisha ambayo imepanda?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, vile vile tangu Awamu ya Tano imeingia madarakani *training* ilikuwa imesimamishwa na *training* ni sehemu moja ya kuwapa watumishi motisha na kuwawezesha kupata weledi. Je, Serikali itaanza lini kutekeleza mpango wa mafunzo ambao upo na haujatekelezwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la *annual increment* nadhani kama atakuwa alifuatilia vizuri hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Mei Mosi ilielezwa kabisa bayana kwa Vyama vya Wafanyakazi *annual increment* mwaka huu itakuwepo.

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia katika bajeti ya mishahara maana yake yeye amesema kwamba hajaiona, *obviously* kwenye bajeti ya mishahara huwezi kusema sasa

hapa hii ndio itakuwa nyongeza ya mwaka. Bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni trioni 6.6, bajeti ya mwaka huu ni nadhani trioni 7.25.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, asubiri aone katika mwaka wa fedha utakapoanza endapo *annual increment* hiyo itakuwepo au la! Nadhani tusichanganye na kima cha chini cha mshahara, nadhani atakuwa ameelewa kwa sababu yeye amekaa Utumishi anafahamu, lakini nimtoe hofu nimweleze tu kwamba Mheshimiwa Rais alishaahidi kupitia siku ya Mei Mosi kwamba nyongeza ya mwaka itakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kupandisha Watumishi mishahara Serikali imekuwa ikifanya hivyo kila mara hali ya kiuchumi inapoimarika na tumekuwa tukijitahidi na tutakuwa tukifanya hivyo kila mara kwa mujibu wa takwimu, lakini vilevile kwa kuangalia mfumuko wa bei pamoja na takwimu nyinginezo zinazotolewa na shirika letu la *NBS*.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mafunzo; mafunzo hayajawahi kusitishwa, mafunzo yanaendelea na hata kama mkiangalia katika bajeti mbalimbali za Mawizara zilizopitishwa, kupitia kwa waajiri wao na Maafisa Masuuli wamekuwa wakitenga bajeti zao. Niendeleo kusisitiza kupitia Bunge lako Tukufu waajiri waendeleo kuweka mipango yao ya mafunzo ya kila mwaka, wajitahidi kufuatilia mipango hiyo lakini zaidi waweze kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza na kutoa weledi kwa ajili ya watumishi wao.

**SPIKA:** Nilikuona Mbunge wa Viti Maalum Iringa, Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali. Kwanza niipongeze Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya katika nchi hii. Hivi karibuni kulikuwepo na zoezi la uhakiki wa vyeti feki na katika uhakiki huo kuligundulika kwamba kuna vyeti feki katika taasisi nyingi na kusababisha

sasa kuwepo na upungufu mkubwa sana katika taasisi mbalimbali na hasa katika hospitali zetu na Halmashauri zetu. Sasa napenda kujua je, ni lini sasa zoezi la kuziba zile nafasi ambazo wale wenye vyeti feki wameondolewa zitaweza kuzibwa ili kusaidia wale wafanyakazi waliopo wasifanye kazi kwenye mazingira magumu sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia ustawi wa watumishi lakini pia kwa namna ambavyo anafuatilia upungufu huu uliojitokeza wa watumishi kutokana na zoezi lililoendeshwa la wenye vyeti feki.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwamba, tumekuwa tukieleza humu ndani tayari kibali kimeshatolewa cha ajira 15,000. Tulikuwa tunafanya mashauriano na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wameshatuletea orodha maana yake ilikuwa ni lazima tujue katika kila kituo ni nafasi ipi ambayo iko wazi.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwamba katika maeneo ambayo yameathirika sana ni sekta ya elimu pamoja na sekta ya afya kwa zaidi ya asilimia 70 na zaidi kidogo. Pia kwa sekta ya afya tu peke yake zaidi ya watumishi 3,360 wamekumbwa katika zoezi hili. Nimweleze tu kwamba tayari tumeshaanza mchakato huo na muda si mrefu nafasi hizo zitazibwa.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali linaulizwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura. Hakuna anayesimama, upande wa CCM.

**MHE: LUCIA M. MLOWE** Niko hapa, niko hapa



Na. 376

**Malalamiko ya Kuwepo kwa Dawa za ARV Zilizokwisha  
Muda wa Matumizi Kigoma**

**MHE. LUCIA M. MLOWE (K.n.y MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya kupokea dawa za ARV zilizokwisha muda wa matumizi (*expired*) kwenye vituo vya afya katika Manispaa ya Kigoma Ujiji na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukaguzi katika Manispaa ya Ujiji na Mkoa wa Kigoma ili kubaini ukweli wa malalamiko hayo?

**SPIKA:** Lilikuwa limefaulishwa hilo swali, majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu mahususi wa kuangalia dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuvitoa katika Bohari ya Dawa na kuvisambaza kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya nchi. Kwa kutambua unyeti na umuhimu wa kutoa dawa salama zenye ubora kwa wananchi, Bohari ya Dawa yenye jukumu la kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi hutumia utaratibu ufuatao:-

(a) Mfumo wa ukusanyaji na utengenezaji wa nyaraka za ugavi una uwezo wa kuona kuwa dawa

inayotakiwa kutolewa kuwa imebakisha muda gani kabla ya kwisha muda wake wa matumizi. Iwapo dawa hizo zitakuwa zimebakisha muda wa miezi sita mfumo huo hutoa tahadhari kwa afisa na kusitisha taarifa hiyo kutumwa kwa ajili ya kutoa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi husika.

(b) Kamati ya Dawa ya Kituo husika hupokea dawa hizo na kufanya ukaguzi kabla ya kusaini *form* mahususi ya kupokelea dawa na kujiridhisha kuwa dawa hizo zimekabidhiwa na kupokelewa kama ilivyoainishwa katika nyaraka za manunuzi kwa idadi baada ya kuhesabu na kuangalia kama zina ubora unaotakiwa. Iwapo kamati ama anayepokea dawa hizo ataridhika basi atasaini katika nyaraka hizo na anayekabidhi dawa huondoka na nakala. Iwapo Kituo hakitaridhishwa na dawa zilizofika, hulazimika kuzikataa na kujaza *form* maalum inayoitwa *Discrepancy form*.

Mheshimiwa Spika, tunaomba vituo au Halmahsauri hizo kuwasiliana moja kwa moja na taasisi za Serikali zinazohusika na usambazaji wa dawa katika Bohari za Dawa za Kanda au Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi ili yaweze kufanyiwa kazi mara moja pindi yanapotokea ili kwa pamoja tulinde afya za wananchi tunaowatumikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucia Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri bado kuna malalamiko makubwa juu ya dawa hizo zilizopitwa na wakati na bado watu wanapata dawa zilizopitwa na wakati. Hapa katika jibu lake amesema kuna watu wanaofuatilia, je, ni nani anaeyefanya *monitoring* ya Kamati hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna wagonjwa ambao mpaka sasa hivi wanapata matatizo kwa sababu vituo vyao ni mbali, wanatembea umbali mrefu na wengine wanakata tamaa wanaamua kuacha dawa. Je, Serikali ina mkakati gani kuongeza vituo? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, mkakati wa kuongeza vituo vya kutolea huduma ya afya, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza nani anayefanya *monitoring* ya Kamati hiyo. Kwanza hii Kamati ya Dawa ni Kamati ambayo ipo kwenye kila kituo na Kamati hii inahusisha Watumishi kwa maana ya wataalam kwenye kituo husika lakini pia inahusisha wawakilishi wa wananchi ambao wanaingia kwenye Kamati hiyo ili kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za afya kwenye kituo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, hii ni Kamati shirikishi na ushirikishi wake unaifanya Kamati hii ipate uhalali wa macho ya wananchi kwa sababu wananchi moja kwa moja wamewakilishwa na kwa msingi huo wanajua wanachokipokea na wanashiriki aidha, kwa kusaini ama kwa kushuhudia mtu ambaye anasaini nyaraka hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna upungufu wowote ule ambao unaweza kuwa umejitokeza, basi ushiriki wa wananchi kwenye eneo hilo utakuwa ni mdogo. Nitoe rai kwa Mheshimiwa Mbunge ashiriki yeye pamoja na Baraza la Madiwani kufanya ufuatiliaji wa kazi inayofanywa na Kamati ya Dawa ya kila Kituo na kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jibu letu ni kwamba, wanaofanya *Monitoring* ni wenye mali, wenye mali ni wanaomiliki Kituo husika na wanaomiliki kituo husika, maana yake ni wananchi na wananchi wamehusishwa humo ndani na wawakilishi wa wananchi, ni wasimamizi wa vituo vyao vyote ndio maana wanaenda kufanya *supportive supervision* kila mwezi na kuna bajeti kwenye Halmashauri zote nchini ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu mkakati ya Serikali kuongeza vituo, kwanza kusema umbali ni mrefu sana hapana, kwa sababu toka ***Alma-Ata declaration*** hata kabla ya hapo toka Afya kwa wote miaka hiyo ya 70 Serikali

imekuwa ikiongeza idadi ya Vituo siku hata siku na mwishoni tumekuwa kuweka hili Azimio kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba tutajenga Kituo cha Afya kwenye kila Kata na Zahanati kwenye kila Kijiji ambalo sasa hivi tuko mbioni kutekeleza kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uwezo wetu wa kuwa na vituo ambavyo vipo karibu na wananchi umeongezeka sana toka miaka hiyo ambayo naisema ya Azimio la Afya kwa wote la miaka ya 1971 – 1972 na kwamba kuna umbali mrefu, hapana. Sema tumejiongezea malengo, sisi wenyewe tumeongeza *target*, *targets* za zamani zilikwishafikiwa na Serikali zilizopita, kwa hiyo tunachokifanya sasa hivi ni kuboresha huduma na kuongeza tena vituo vingi zaidi, lakini hakuna umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kukanusha hilo ili kuweka sawa. Pia mkakati wetu ni huo ambao nimeusema wa kujenga Kituo cha Afya kwenye kila Kata na Zahanati kwenye kila Kijiji.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum Dodoma. Mheshimiwa Toufiq.

Na. 377

### **Kufufua Kiwanda cha Zabibu Dodoma**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais amesisitiza sana kuhusu Tanzania ya Viwanda na katika Mkoa wa Dodoma kulikuwa na Kiwanda cha Kutengeneza Mvinyo (*DOWICO*) ambacho kilikuwa msaada mkubwa sana kwa wakulima wa zabibu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua kiwanda hicho ili kufanya wakulima wapate tija kwa kuuza zabibu zao kiwandani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Taufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Dodoma *Wine Company Limited (DOWICO)* cha hapa Mjini Dodoma kinamilikiwa na Bw. Thakker Singh aliyeuziwa kwa njia ya ufilisi mwaka 1993. Kwa sasa kiwanda hiki kimefungwa tofauti na matarajio ya wakati kinabinafsishwa. Mpango wa Serikali ni kukifufua kiwanda hiki na vingine vilivyofungwa, pia kuendeleza vilivyopo na kujenga viwanda vipya hasa vinavyotumia malighafi za ndani na kuajiri watu wengi kama Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 unavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata Mpango huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina tunashauriana na wawekezaji mbalimbali namna ya kuvifufua viwanda vilivyofungwa na ikibidi kuwapa wawekezaji wengine ili wavifufue na kuviendeleza viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Mwekezaji wa Kiwanda cha *DOWICO* ameingia mkataba na mmiliki wa Kiwanda cha *SETAWICO* kilichopo Hombolo kwa makubaliano ya kukifufua na kazi hii imeanza kwa kufanya ukarabati. Ni matumaini ya Serikali kuwa kazi ya ukarabati na usimikaji wa baadhi ya mashine utafanyika na kukamilika mapema.

Wizara yangu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma tunaendelea kufuatilia ukarabati wa kiwanda hiki kwa karibu ili kuhakikisha uzalishaji unaanza na kukiwezesha kuchangia katika uchumi wa Taifa hasa kutoa ajira kwa vijana na kuwa soko la zabibu ya wakulima hapa mkoani Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq ameridhika, Mheshimiwa Toufiq swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante. nashukuru sana kwa majibu ambayo yametolewa na Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mwekezaji aliyechukuwa *DOWICO* alizembea na kufunga kiwanda hicho, hivyo kusababisha uzalishaji mvinyo bora wa Dodoma kutokupatikana katika soko. Je, Serikali haioni umuhimu wa kumpatia mwekezaji mwingine tofauti na huyu aliyepo ili aweze kukifufua kiwanda hicho?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali imekuwa katika mpango wa kuwezesha uanzishwaji wa Kiwanda cha Kusindika mazao ya Zabibu katika Wilaya ya Chamwino kwa kushirikiana na mfuko wa *GEFF*. Je, ni hatua gani za haraka zilizochukuliwa na Serikali ili kuharakisha ujenzi wa kiwanda hiki ili wakulima wa zao la zabibu waweze kupata soko? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, muhimu sana kwa wakulima wa Zabibu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la kumtafuta mwekezaji mwingine, ndani ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Viwanda *TIRDO* na kwa kushirikiana pia na Ofisi ya Msajili wa Hazina tumeanzisha kitu kinaitwa *Technical Audit* na lengo lake kubwa ni kwenda kuvifuatilia viwanda hivi ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi na kuvifuatilia kuona namna gani vitaanza kufanya kazi kwa kupitia utaratibu huo wa utafiti ambao unafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tunawasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na kama nilivyosema katika

majibu yangu ya msingi kwamba tayari ukarabati umeanza, kwa hiyo tutafanya hiyo *technical audit* ya kufuatilia kuona wanaanza lini kazi hii na baadaye tutatoa taarifa namna ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba jambo hili ni kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma, hasa ukiangalia kwamba zabibu ndio zao pekee ambalo linategemewa sana hapa Dodoma na Dodoma ndio sehemu pekee duniani ambako kuna uwezo wa kuvuna zabibu hii mara mbili. Israel wamejaribu, Afrika Kusini wamejaribu imeshindikana, kwa hiyo tunafahamu umuhimu wa zao hili kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nimwondoa hofu Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, hii pia ni Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwavutia wawekezaji wengi kujenga viwanda vikubwa hasa ukiingatia kwamba mpaka Machi, 2017 tayari tumeweza kuvutia viwanda vikubwa 393 ambavyo vimesajiliwa na tayari vimeshaweka kiasi cha shilingi trillion tano. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata hili nalo litafanyika

Mheshimiwa Spika, la pili ameuliza kuhusu Kiwanda cha Mvinyo pale Chamwino. Nafahamu wakulima wa Dodoma wanategemea sana viwanda hivi vikubwa kwa ajili ya soko la zabibu, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge katika utaratibu wa uwekezaji katika viwanda, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, iliamua kuingia moja kwa moja katika uwekezaji huu. Pale Chamwino Mfuko wa *GEPF, WCEF* pamoja na *TIB* kwa pamoja watafanya uwekezaji wa kiwanda cha mvinyo.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi sasa tayari Bodi za Mifuko hii zimekwisha-*approve* kiasi cha shilingi bilioni 26 kwa ajili ya kwenda kuanza ujenzi wa kiwanda hiki. Niwaondoe hofu wananchi wa Mkoa wa Dodoma, watapata fursa ya masoko ya zabibu na ukiongozwa na wewe Mheshimiwa Spika, ambaye ni mkulima pia. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mambo mswano kabisa, Mheshimiwa Nape nilikuona swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nipongeze juhudi na kasi kubwa inayofanywa na Serikali ya kufufua viwanda vile ambavyo vilikuwa vimekufa, lakini pia kuvutia uwekezaji wa viwanda vipya. Sasa swali langu, ufufuaji wa viwanda vya korosho katika Ukanda wa Kusini hasa katika Jimbo la Mtama na maeneo mengine umefanyika lakini kuna kusuasua kwa ukamilishaji wa baadhi ya maeneo ili ubanguaji wa korosho uweze kufanyika kwa kiwango kikubwa na hasa hapa nazungumzia Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Nachingwea, kwa kuwa Mwekezaji ambaye amefufua Kiwanda cha Mtama, ndiye ambaye amepewa kazi pia ya kufufua Kiwanda cha Nachingwea. Ni lini sasa kazi hii itakamilika ili wakulima wa korosho wapate mahali pa kuuza korosho yao na thamani ya zao la korosho ipate kuongezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape anaposema Kiwanda cha Mtama, anamaanisha kiwanda cha huko Mtama, sio cha mtama huu unaolimwa Dodoma. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inafufua viwanda vyote na ndiyo maana Wizara inafanya kazi ya karibu sana na Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na *TIRDO*, lengo lake ni kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinafufuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa upande wa Mikoa ya Kusini kule Mtwara, Lindi na kwingineko wanakolima korosho, tulikuja na *model* ambayo tumeiita *BOOT* ambayo *Build on Operate* na *Transfer* na hii ndiyo ambayo tuliitumia hata pale Mtama kwa kumtumia huyu Mwekezaji wa kutoka China ambaye anaitwa *Sang Shin industry* alifanya hivyo Mtama na ndivyo hivyo tutafanya katika maeneo mengine



hasa Nachingwea kuhakikisha kwamba viwanda hivi vya korosho vinaweza kufufuliwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali litaulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Subira Mgalu.

Na. 378

### **Nyumba za Polisi na Magereza Bagamoyo**

**MHE. SUBIRA K. MGALU (K.n.y. MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA)** aliuliza:-

Baadhi ya vituo vya Polisi na Magereza nchini vina majengo chakavu sana vikiwemo Kituo cha Polisi Bagamoyo na Gereza la Kigongoni Bagamoyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kujenga nyumba za Polisi na Askari Magereza Bagamoyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya Vituo vya Polisi na Magereza nchini vina majengo chakavu ambayo yalijengwa miaka mingi iliyopita na kituo cha Polisi na Magereza Bagamoyo kikiwa miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga Kituo cha Polisi, Gereza na nyumba za kuishi za Askari katika Wilaya ya Bagamoyo na Wilaya nyingine nchini zisizo na majengo hayo, ujenzi huo utajengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha za bajeti. Sambamba na hilo, Wizara

imeweka msisitizo katika matumizi ya rasilimali zilizopo kama vile ardhi ili kupunguza tatizo hili kwa kujenga vituo vya Polisi katika Wilaya 25 na Magereza katika Wilaya 52 kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakupa nafasi ugeuke tu uangalie wewe mwenyewe uone jinsi ambavyo Wabunge hawaridhiki na hali ya vituo vya Polisi na Magereza nchini. Haya tuanze na Mheshimiwa Bulembo. *(Makofi / Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Mwenye swali lake.

**SPIKA:** Aaa! Mwenye swali lake, mpaka nimekusahau Mheshimiwa Shukuru maana yake Wabunge wamesimama wengi kweli. Tuanze na Mheshimiwa Shukuru halafu Mheshimiwa Bulembo halafu James Mbatia. Mheshimiwa Subira, samahani.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye kuleta matumaini ya ujenzi wa Vituo vya Polisi na Magereza, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Gereza hili la Kigongoni lina changamoto kubwa ya tatizo la mgogoro wa mpaka wa ardhi kati yake na wananchi wa Sanzare na Matibwa, mgogoro huu umepelekea uvunjifu wa amani mara kadhaa. Je, ni lini Serikali itashirikiana na uongozi wa Wilaya ya Bagamoyo katika utatuzi wa mgogoro huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Pwani ukiachia Wilaya ya Mafia una tatizo kubwa la kutokuwepo kwa Vituo vya Polisi na kwa kuwa kuna hali tete ya usalama katika maeneo hayo ya Wilaya za Mkoa wa Pwani ukiacha Mkuranga, Kibiti na Rufiji. Pia kwa kuwa Wilaya ya Mkuranga imeanza ujenzi wa Kituo cha Polisi kwa ushirikiano wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na wananchi wa Wilaya ile ya Mkuranga. Je, ni lini Serikali itakubali kuisaidia Wilaya hii ya Mkuranga kukamilisha kituo hicho cha Polisi ili kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri. Nikianza na la kwanza la mgogoro uliopo kati ya Gereza pamoja na wananchi wa kule Bagamoyo, nikiri ni kweli mgogoro huo upo na Mheshimiwa Mbunge Dkt. Shukuru Kawambwa amekuja mara kadhaa Ofisini na mara nyingine aliongozana na baadhi ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, kitu tulichomuahidi ni kwamba baada ya Bunge, ama tukipata fursa baada ya kupigia kura bajeti, tutatembelea eneo husika tukiwa na Timu ya Mkoa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ili tuweze kujionea wapi na nini chanzo cha mgogoro huo na njia nzuri ya kulimaliza tatizo hilo ili wananchi wake wasipate shida na uwepo wa Gereza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuunga mkono jitihada za Mbunge wa Mkuranga, ni kweli na Mbunge anafanya kazi nzuri sana na sisi kama Serikali ukanda ule tumeupa Mkoa Maalum wa Kipolisi, kwa hiyo Wilaya zote ambazo zinakaa ukanda ule ikiwemo Mkuranga tutazipa umuhimu na upendeleo unaostahili ili tuweze kupata makazi ya Askari, Ofisi za Polisi pamoja na Ofisi za Kanda na kwa pamoja na wingi wa Askari ili kuweza kusaidia shughuli za usalama katika eneo hilo ili wananchi waweze kufanya kazi bila kuwa na hofu yoyote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikutaja Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa watu wanaokwenda kwenye Magereza ni wahalifu na huwa wamehukumiwa, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani iniambie na itoe kauli hapa, ni lini Gereza la Muleba litaenda kuzungushiwa fensi, maana yake leo Gereza la Muleba lina uzio kwa maana wafungwa wakiamua kuondoka leo, kesho wanaondoka,

mtawakamata wale viongozi bure, sasa nataka *commitment* ya Serikali ni lini itafanya *emergence* ya kwenda Muleba kuweka uzio wa Magereza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, lini mnaenda Muleba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Gereza la Muleba linahitaji kuwekewa uzio, tunatambua na tumejipanga kwamba wakati wowote ambapo tutakamilisha kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio huo tutafanya hiyo kazi. Jambo hilo tunalitambua na lipo katika vipaumbele vyetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia, nilikwishakutaja.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kituo cha Polisi cha Himo ambacho kinatoa huduma kwa wakazi takribani 400,000 na kiko mpakani, Serikali iliahidi hapa kwamba itafanya ukarabati wa miundombinu ya kituo hicho hasa Ofisi. Sasa ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya tangu mwaka jana na hali ya kituo inazidi kuwa hoi bin taabani? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, jibu la suala hili, halitofautiani sana na jibu langu nililojibu mwanzo, kwamba kituo hiki cha Himo ni moja kati ya vituo ambavyo vina changamoto na hasa ukitia maanani kipo karibu na mpakani kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amezungumza. Kitu ambacho kimekwamisha kama ambavyo nimezungumza mwanzo ni suala la bajeti. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tuna mpango wa kujenga vituo na kukarabati vituo vingi nchini kama nilivyozungumza katika jibu langu la msingi kwamba tuna upungufu wa vituo katika Wilaya 25 na vituo vingi vipo katika hali mbaya nchini, lakini tutafanya kazi ya kuvirekebisha na kujenga hatua kwa hatua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Savelina Mwijage, swali la mwisho la yongeza kwenye eneo hili?

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Gereza la Bukoba Mjini linakuwa na msongamano mkubwa sana wa wafungwa na tuna Magereza ambazo zimechakaa sana kwa mfano kama Kitengule, Rwamlumba ni lini Serikali itapanua hiyo Rwamlumba ili kuweza kuwapunguza wafungwa walioko Bukoba Mjini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitenga pesa za bajeti kuongeza mabweni mwaka hadi mwaka na hii ni kwa sababu ya kutambua changamoto za msongamano wa Magereza yetu nchini. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tumelipokea, tutajitahidi katika mwaka wa fedha ujao tuweze kuweka Gereza Bukoba Mjini miongoni mwa Magereza ya vipaumbele vya kuongeza mabweni ili kupunguza idadi ya msongamano katika Magereza yetu nchini.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mambo ya Ndani ya Nchi linaloulizwa na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba.

Na. 379

### **Mapambano Dhidi ya Madawa ya Kulevya**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Charles Kitwanga alikaririwa na vyombo vya habari mwezi Desemba, 2015, akiliagiza Jeshi la Polisi kumkabidhi majina ya watu wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya, ambazo ongezeko lake nchini lina athari hasi dhidi ya vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa:-

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani katika kuwabaini, kuwachunguza na hatimaye kuwafikisha Mahakamani wale wote waliobainika kujihusisha na mtandao wa biashara za dawa za kulevya?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana wanaojingiza kwenye dimbwi la matumizi ya dawa za kulevya kuondokana na utegemezi wa dawa za kulevya nchini?

(c) Je, ni vijana wangapi kwa nchi nzima ambao kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita wamepatiwa tiba kusaidiwa kuondokana na utegemezi wa dawa za kulevya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la vijana wa Kitanzania, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi Engineer Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kati ya Oktoba, 2015 hadi Aprili, 2017 Jeshi la Polisi lilifanikiwa kukamata jumla ya watuhumiwa 9,140 wa dawa za kulevya ambapo watuhumiwa 14,410 kesi zao zinaendelea Mahakamani na zipo katika hatua mbalimbali. Watuhumiwa 2,401 walikutwa na hatia, watuhumiwa 615 waliachiwa huru na watuhumiwa wengine 13,071 kesi zao ziko chini ya upelelezi.

(b) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kupitia Programu ya kuzuia uhalifu limeendelea kutoa huduma ya urekebishaji kwa waaathirika wa dawa za kulevya. Kwa kutumia vikundi mbalimbali vya michezo chini ya miradi ya

kuzuia uhalifu kama vile familia yangu haina mhalifu na klabu ya usalama wetu kwanza.

(c) Mheshimiwa Spika, vijana 3,000 walipatiwa tiba katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kwa kushirikiana na wadau.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Katimba, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwanza ningependa kutambua jitihada kubwa sana zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli katika vita dhidi ya madawa ya kulevya na ningependa kuwatia moyo na waweze kuendelea na jitihada hizi. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka katika mitaala ya elimu ya msingi pamoja na sekondari mafunzo kuhusu athari ya dawa za kulevya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, hawa vijana 3,000 waliopatiwa tiba katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kwa kushirikiana na wadau, je Serikali inafahamu vijana hawa wako wapi katika muda huu, yaani kwa sasa na wanafanya nini?(*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainab Katimba kuhusiana na kipengele cha mpango wa Serikali kuweka kwenye mitaala masuala ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba mitaala ya kuanzia shule za msingi, Sekondari pamoja na masuala ya kitaaluma lakini pia inakuwa imebeba masuala

mtambuka. Kwa hiyo, masuala yanayohusiana na masuala ya madawa ya kulevya, masuala ya jinsia, masuala ya UKIMWI yapo katika mitaala yetu na tutaendelea kuyaimarisha ili kuhakikisha kwamba tunaenda sambamba na azma ya Serikali ya kupambana na hili janga la madawa ya kulevya nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, tuko sasa Katiba na Sheria, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Korogwe Mjini, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

Na. 380

### **Hitaji la Mahakama Wilaya ya Korogwe**

**MHE. MARY P.CHATANDA** aliuliza:-

Mhimili wa Mahakama kama ilivyo mihimili mingine unahitaji kuwa na eneo la uhakika la kufanyia kazi na vitendea kazi vya uhakika:-

(a) Je, ni lini Wilaya ya Korogwe itajengewa Mahakama ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama kama Mihimili mingine, wanahitaji mazingira mazuri na muafaka kwa kufanyia kazi zao. Aidha, napenda kukiri kuwa moja ya changamoto kubwa inayozikabili Mahakama zetu ni pamoja na uhaba wa majengo na uchakavu wa miundombinu iliyopo.



Mheshimiwa Spika, Mpango wa maendeleo wa ujenzi wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni pamoja na ujenzi wa Mahakama za Mkoa ikiwemo ujenzi wa Mahakama sita za Hakimu Mkazi, ujenzi wa Mahakama 15 za Wilaya na Ujenzi wa Mahakama 10 za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama imepanga kujenga Mahakama ya Wilaya ya Korogwe kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, katika Mkoa wa Tanga Wilaya zilizopewa kipaumbele katika ujenzi ni Kilindi, Korogwe na Mkinga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chatanda, swali la nyongeza.

**MHE. MARY P.CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwa kutukumbuka Korogwe, Kilindi na Mkinga kwamba mwaka huu wa fedha watatupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama. Swali la nyongeza, kwa kuwa vile vile Mahakama hizi zimekuwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi hususan Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutupelekea Mahakimu Mahakama za Mwanzo Korogwe Mjini na Vijijini? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo zuri fupi la nyongeza, Mheshimiwa ni lini mnapeleka wataalam?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kabla sijamjibu swali lake napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe kwa hatua madhubuti ambayo wameianza ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Mnyuzi na hivi sasa najua wanasubiri tu ramani kuanza ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini tutawapelekea watumishi kwa maana ya kada ya Mahakimu, nimwondoe

tu hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo tutakuwa tuna uwezo wa kibajeti wa kuweza kufanya kazi hiyo tutafanya, kwa sababu tumeanza na ukarabati wa miundombinu, basi jambo hili likikamilika pia tutaona namna ya kuweza kuongezea watumishi katika Mahakama za Korogwe ili nao waweze kupata huduma hii ya Kimahakama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Karatu, utafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wilaya ya Karatu ilikuwa na Mahakama za Mwanzo nne lakini hivi sasa imebaki Mahakama moja tu iliyoko Karatu Mjini ndio inayofanya kazi, Mahakama zingine za Mwanzo zimesimama kutokana na upungufu wa Mahakimu wa ngazi hiyo. Je, ni lini Serikali itapeleka Mahakimu wa Ngazi ya Mahakama za Mwanzo ili huduma hiyo muhimu ipatikane kwenye ngazi za Tarafa kule chini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la wananchi wa Karatu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ombi lake na natumaini mwaka wa fedha unaokuja tutayafanyia kazi maombi yake ili na wakazi wa Karatu waweze kupata fursa ya kupata watumishi wa kuwahudumia katika Idara hii ya Mahakama.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mlinga, swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, asante sana, Wilaya ya Ulanga pamoja na kuwa na Mbunge kijana machachari lakini haina Mahakama ya Wilaya. Je, wananchi wa Ulanga wanaisikiliza Serikali yao ya hapa kazi tu inawaambia nini kuhusiana na jengo la Mahakama ya Wilaya? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Mavunde.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika miaka ya hivi karibuni Serikali imeendelea kujenga Mahakama tofauti na miaka iliyopita na kwa mwaka huu wa fedha unaokuja 2017/2018, tumetengewa kiasi cha shilingi billioni 46 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na kwamba ninacho kitabu hapa kinachoelezea Mahakama zitakazojengwa, kwa hiyo nimwombe tu afike katika Ofisi yetu aangalie, ni orodha ndefu sana ya Mahakama na naamini kabisa eneo lake la Jimbo la Kilombelo lilitakiwa pia liwe limezingatiwa ili nao waweze kupata huduma hii.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Waheshimiwa Wabunge, swali linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David.

Na. 381

**Ujenzi wa Malambo, Majosho na Kisima  
Kirefu-Kata ya Ruvu.**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Serikali iliahidi katika bajeti ya 2012, 2013 na 2014 kujenga Malambo, Majosho na Kisima kirefu kwa ajili ya wananchi na Wafugaji wa Kata ya Ruvu katika Jimbo la Same Magharibi:-

Je, ni lini ahadi hiyo itakamilishwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia bajeti yake na program mbalimbali imeendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya maji ya mifugo kwa kutumia vipaumbele kama maeneo yenye mifugo mingi na yale ambayo yanapokea mifugo wakati wa kiangazi. Kupitia utaratibu huo Wizara imeweza kujenga mabwawa na malambo katika Wilaya za Kiteto, Kilindi na Ngorongoro. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Wizara ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa malambo katika Wilaya ya Same na Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara haikupatiwa fedha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Mwaka 2015/2016, wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same waliainisha eneo la Kijiji cha Ruvu, Kata ya Ruvu kwa ajili ya ujenzi wa lambo. Mwaka 2017/2018, Wizara imetenga fedha kwenye bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye baadhi ya Wilaya ikiwemo Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuzishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutenga fedha kupitia bajeti zao kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji ya mifugo kama malambo, mabwawa na visima virefu ili kupunguza kero ya upatikanaji wa maji kwa mifugo hasa wakati wa kiangazi. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kujenga na kukarabati miundombinu ya maji ya mifugo kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Same Mheshimiwa Dkt. Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza na pili nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutupa majibu ya matumaini. Hata hivyo, napenda kusahihisha kidogo wakati wataalam wamekuja mwaka 2015/2016 nilikuwepo na tuliona maeneo mawili ya malambo kwa ajili ya kujenga malambo na maeneo mawili kwa ajili ya majosho na sehemu moja ya kisima kirefu, lakini jibu la Waziri

hapa linazungumzia lambo. Kwa hiyo naomba hiyo irekebishwe kwamba ni miundombinu hiyo niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, sasa naelekea kwenye swali la kwanza, je, ni kiasi gani ambacho kimetengwa kwenye bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya miundombinu hiyo ambayo nimeitaja katika Jimbo la Same Magharibi na hususani Kata ya Ruvu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa milioni 100 zinaweza zikatosha malambo mawili na majosho mawili kama kazi hii itasimamiwa na Wizara, lakini kazi hii kama itasimamiwa na Halmashauri milioni 100 inaweza ikatosha josho moja au lambo moja. Je, Serikali sasa iko tayari kwa sababu yenyewe ndio inatoa hizi fedha isimamie kusudi miundombinu hiyo ikamilike kwa bajeti ya mwaka huu?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Mbunge wa Same Magharibi, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu wa usahihi wa nilichokisema ambapo amesema anarekebisha tutaenda kuangalia kuhusu makubaliano yale, lakini kimsingi hakuna kitu kilichoharibika, tutaenda kutekeleza kadiri tulivyoahidi wakati tulipokwenda Jimboni kwake.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusiana na ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetengwa, nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa inakuwa ni vigumu kuwa na takwimu sahihi lakini anaweza akanifuata baadaye nikamweleza na ombi lake la kwamba Wizara yenyewe ndio inasimamia ujenzi ule, vilevile tutalichukua na ukweli wa mambo fedha zinazotolewa mara nyingi na Wizara kwa ajili ya kujenga miundombinu huwa tunahakikisha kwamba tunazisimamia ili ifanye kazi iliyoelekezwa.

**SPIKA:** Tunaelekea Wizara ya Elimu, swali la Mheshimiwa Munde, Mbunge wa Viti Maalum Tabora.

Na. 382

**Mkoa wa Tabora Hauna Chuo Kikuu**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Chuo Kikuu katika Mkoa wa Tabora hasa ikizingatiwa kuwa Mkoa huo hauna Chuo Kikuu hata kimoja cha Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna marekebisho madogo sana nadhani atakuwa aliyapata Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa ya uwekezaji inayohitajika katika kuanzisha vyuo vikuu, ni vigumu kwa sasa Serikali kuanzisha Chuo Kikuu katika Mkoa wa Tabora. Hata hivyo, katika Mkoa wa Tabora kuna Tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambacho ni cha Serikali, pia kuna Chuo Kikuu cha Theophil Kisanji Kituo cha Tabora na Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo. Uwepo wa Vyuo hivi na hasa vyuo binafsi ni matokeo ya Serikali kutekeleza sera ya ushirikishwaji wa Sekta binafsi kutoa elimu ya juu nchini

Mheshimiwa Spika, naomba niendeele kutoa wito kwa wadau mbalimbali kujitokeza na kushirikiana na Serikali katika kuanzisha Vyuo Vikuu katika program za vipaumbele vya Taifa kama vile Uhandisi, Teknolojia, Afya, Kilimo na Ualimu wa Sayansi na Hisabati na maeneo mengine ambayo yataonekana yanafaa.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Mkoa wa Tabora ni Mkoa ambao uko katikati ya Mikoa ya Singida, Shinyanga, Kigoma na Katavi; na kwa kuwa Mikoa hii haina Vyuo Vikuu vya Serikali ambavyo mwanafunzi anaweza akapata mkopo wa Serikali tofauti na *Open* aliyoisema Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa Serikali itaweka mkakati wa kukipandisha hadhi Chuo cha Uhazili Tabora ambacho ni kikubwa na ni kizuri kama ilivyofanya katika Chuo cha Chang'ombe cha Dar es Salaam na katika Chuo cha Ushirika Moshi, walivipandisha hadhi, sasa wana mpango gani wa kupandisha hadhi Chuo cha Utumishi wa Umma cha Uhazili cha Tabora? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Chuo cha Uhazili kikipandishwa hadhi kiwe nini.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kiwe Chuo Kikuu cha Serikali ambacho kitaweza kutoa *degree* ambayo sasa hivi haitoki.

**SPIKA:** Ya Uhazili eeh! Haya

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Aah! mchanganyiko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa maswali yake ya nyongeza; nikianza na umuhimu wa Mikoa ya Tabora pamoja na jirani zake kuwa na Chuo eneo hili, kimsingi Vyuo Vikuu ni Vyuo vya Kitaifa na kwa sasa hivi tuna Vyuo ambavyo bado havijaweza kudahili kwa idadi ambayo ni ya kutosha kwa mfano Chuo Kikuu cha *UDOM* bado kina nafasi nyingi na hata vyuo vingine, kwa hiyo tutakuwa tunaanzisha Vyuo kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Chuo cha Uhazili Tabora ambacho kimsingi kipo chini ya Wizara ya Utumishi, naomba tu niseme kwamba hiyo sasa itategemeana na hali halisi ya Mazingira na uainishwaji wa kozi husika kulingana na mitaala iliyoboreshwa, ikitokea hivyo nadhani Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba wataona namna gani kinavyoweza kufanyika

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utumishi na Utawala Bora, majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kwa majibu mazuri nipende tu kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki ni mahususi kabisa kwa kuwaendeleza watumishi wa umma na kitaendelea kubaki hivyo na kama alivyoeleza kwa masuala ya Vyuo Vikuu kwa kuwa yako chini ya Wizara ya Elimu endapo wataona kuna haja ya kufungua Vyuo Vikuu vingine hayo yako chini yao, lakini kwa Chuo hicho cha Uhazili ni Chuo cha Watumishi wa Umma na tuna mipango ya kuviendeleza zaidi ili kuhakikisha kwamba wanatoa kozi nyingi kuwahudumia Watumishi wa Umma. Ni mafunzo maalum kwa watumishi wa umma.

**SPIKA:** Wanyamwezi wote njooni msome Dodoma mmeambiwa. Nakuona Mheshimiwa Maige lakini muda hauko upande wetu utaona pale.

Sasa tuchukue swali la mwisho la siku ya leo ambalo litaelekezwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini. Mheshimiwa Maftaha!



Na. 383

## **Kuiboresha Bandari ya Mtwara**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Bandari ya Mtwara ni Bandari yenye kina kirefu Afrika Mashariki na Kati na Serikali kwa makusudi imeamua kuitupa na kujenga Bandari katika maeneo mengine ya nchi tena kwa gharama kubwa sana:-

Je, Serikali ipo tayari kukiri makosa na kuiboresha Bandari ya Mtwara ili korosho zote zisafirishwe kupitia Bandari hiyo kwa lengo la kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuendeleza bandari zote nchini kadri uwezo utakavyoruhusu ili kuchochea ukuaji haraka wa uchumi. Hii inatokana na ukweli kwamba bandari ndiyo njia kuu ya kuchochea uchumi katika Taifa lolote lililobahatika kuwa na bahari.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mtwara Mjini na Mtwara yote kwa ujumla kuwa Serikali haijawahi na haina nia ya kuitupa Bandari ya Mtwara kwani inafahamu fursa zilizopo katika ukanda wa maendeleo wa Mtwara yaani Mtwara *Development Corridor*.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma yake, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Serikali ilitenga shilingi bilioni 59.32 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa gati moja lenye urefu wa

mita 350 la kuhudumia shehena mchanganyiko ikiwemo ya korosho. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania imetenga shilingi bilioni 87.044 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa gati hilo. Gati hili linasanifiwa na kujengwa na Mkandarasi China *Railway Construction Company (CRCC Group)* kwa kushirikiana na China *Railway Major Bridge Engineering Company Limited* kwa gharama ya shilingi bilioni 137.39 pamoja na VAT. Mkataba wa ujenzi kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na kampuni hiyo ulisainiwa tarehe 4 Machi, 2017 na ujenzi wa gati hilo utakamilika ndani ya miezi 21.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia nashukuru kwa majibu sahihi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri kazungumza hapa kwamba Bandari hiyo ya Mtwara ndiyo itakuwa chanzo cha ufunguzi wa kitu tunachoita Mtwara *Corridor*, maendeleo ya Kusini mwa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Naomba kujua kwamba hili gati linajengwa hivi sasa ni gati moja tu. Mkakati wa Serikali ukoje kuhakikisha kwamba wanamaliza ujenzi wa magati matatu yaliyobaki ili yaweze kukamilika magati manne?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba kujua kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam hivi sasa ina msongamano mkubwa sana na Mtwara sasa hivi hii bandari inajengwa. Je, Serikali ipo tayari hivi sasa kuhakikisha kwamba inapunguza *cargo on transit* kutoka Bandari ya Dar es Salaam waweze kuruhusu Bandari ya Mtwara ili kuweza kuondoa msongamano hivi sasa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Maftaha. Mheshimiwa Engineer Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, magati matatu yaliyobakia mpango wake wa kujengwa kwanza tunataka

kushirikisha Sekta Binafsi lakini vile vile kwanza tunataka tuhakikishe kwamba gati hili moja na kwa namna mizigo ilivyo kwa sasa tunadhani kwamba linatosha kwa muda mfupi na wa kati. Baada ya hapo ikishafunguliwa ile reli ya kutoka Mtwara mpaka Mbamba Baykwa vyovyote vile gati hizi nne lazima ziongezeke. Kwa hiyo, nimshukuru kwa swali hilo, nimepata fursa ya kutoa ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Mtwara kutumika kama mbadala wa Bandari ya Dar es Salaam; sababu mojawapo ya kupanua hii gati kama tulivyosema hili gati ni la urefu wa mita 350, ni kubwa sana ili liweze kuruhusu meli kubwa sana ziweze kutia nanga Mtwara. Moja kati ya sababu ni hiyo, kwamba meli zingine kubwa ziweze kutua Mtwara badala ya muda wote kufikiria kuingia Dar es Salaam.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha pia. Naomba niwatambulishe wageni wangu ambao wanatoka *Media Foundation* wakiongozwa na ndugu Ernest Sungura na wako 74. Ni wafanyakazi na wakufunzi kutoka Tanzania *Media Foundation*. Naomba msimame hapo mlipo. Ahsanteni na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Pia niwatambulishe wageni wanaoongozwa na ndugu Solomon Zakayo Wangwe ambao ni 31, ni wageni wa Mheshimiwa Catherine Ruge. Hawa ni wanafunzi kutoka Umoja wa Wanafunzi Wafamasia hapa nchini. Ahsanteni sana na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Vile vile kuna wageni 21 wa Mheshimiwa Sixtus Mapunda ambao wanatoka kule Ruvuma, nao wanasoma katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana hapa Dodoma au *St. John*. Ahsanteni sana wanafunzi wa kutoka *St. John*. *(Makofi)*

Wanafunzi 136 na Walimu watano wa shule ya msingi St. Jude kutoka Mkoani Arusha. St. Jude, ahsanteni sana watoto wetu kutoka Arusha, mmetoka mbali. Karibuni sana Dodoma mjifunze mambo mbalimbali ya kuhusiana na Bunge na baadaye Maafisa wetu wa Bunge watawapitisha maeneo mbalimbali. Muwaulize maswali bila kuchoka. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada *Chapel* ya Bunge, anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao huwa mnahudhuria ibada katika *Chapel* ya Bunge, jengo la Pius Msekwa, siku ya Jumanne, leo mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge mchana saa saba. Mtumishi wa Mungu John Uroki wa kanisa la Ipagala KKKT Dodoma, pia kwaya kutoka Kanisa la *Mennonite* Tanzania na kwaya ya Uamsho kutoka Veyula Dodoma watahudumu katika ibada hiyo. Kwa hiyo, mnaombwa muweze kuhudhuria maombi hayo.

Waheshimiwa Wabunge, ibada mbalimbali zinaruhusiwa hapa Bungeni kwa madhehebu yote yanayotambuliwa na Serikali. Inatusaidia kuweka hali ya hewa nzuri kidogo na kufukuza fukuza baadhi ya mapepo. Kwa hiyo, ni vyema kuhudhuria, tuombewe ombewe huko kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya hapo, niwatake tu wachangiaji leo mjikite, mjielekeze kwenye mada, dakika kumi ni chache, ukianza kupongeza pongeza na kuzunguka unapoteza muda wako. Kengele ikigongwa hapo unasema; dakika zangu mbona bado? Kwahiyo, nakushauri twende moja kwa moja kwenye mada ili tutumie vizuri muda wetu.

Kwa wale Wabunge wa zamani wanakumbuka wakati fulani tuliwahi kutembelewa na Spika Mstaafu wa Kenya wakati huo akiitwa Ole Kaparo, alikuwa ndiyo Spika wa Kenya wakati huo. Sasa akawa anazungumza nasi kule Msekwa, wakati ule tulipokuwa tunaonesha matangazo yetu ya Bunge *live*, akasema; kule Kenya tunaangalia kidogo hili Bunge la Tanzania namna Bunge lenu linavyofanya kazi, sasa

sisi tunashangaa sana kwa sababu Mbunge wa Tanzania akipata nafasi kwanza anashukuru sana Spika, *as if it's a privilege to speak in the House*, halafu anapongeza sana halafu mwisho anaunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

Akasema, sasa sisi tunajiuliza, kwa nini huyu bwana alisimama mara ya kwanza? Kwa hiyo, naomba sasa kwa sababu dakika zenyewe zinazidi kuwa chache, muda huo unakuwa mfupi, hukatazwi kupongeza na kushukuru lakini tu kutumia vizuri dakika zako kumi ili msiione kama meza hii inapunguza dakika zenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kama kuna miongozo miwili, mitatu nitaichukua lakini wauliza miongozo wasiwe wale wazoefu wa miongozo, leo nataka wapya wapya kidogo. Wale wa siku zote leo sichukui. Katibu andika niletee majina.

Haya nitachukua wawili tu kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Haonga...

**WABUNGE FULANI:** Huyu ni wa kila siku.

**SPIKA:** Ni wa kila siku eeh? Haya kwa kuwa nimeshakutaja haya endelea Haonga na Mheshimiwa Hasunga.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa Kanuni ya 68(7), naomba Mwongozo wako, jana wakati Taarifa ya Awamu ya Pili ya Makinikia inatolewa kuna maneno ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyazungumza kwamba kule Bungeni kama kuna watu wanaropoka, wanasumbua watoe nje ya Bunge. Ukishawatoa nje ya Bunge mimi nitawashughulikia huku nje wanapozungumza. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo, ndiyooo!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa sababu naamini kwamba kuna mihimili mitatu. Je, ni halali mhimili mmoja kuingilia shughuli za mhimili mwingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba mhimili huu una kiongozi wake ambaye ni Spika (ambaye ni wewe hapo) na kama kuna jambo linatokea wewe ndiye utakayelishughulikia hapa. Sasa naomba Mwongozo wako kama kweli huu mhimili unaruhusiwa kuingiliwa na mhimili mwingine wowote ule. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo halistahili kusubiri. Mheshimiwa Haonga, kwanza nikutake uende ukasome Katiba vizuri uielewe vizuri kabisa. Kwa hili ulilouliza, Rais akishaongea mwenye macho na masikio hahitaji tena kuuliza habari kwamba kasema nini hata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hasunga!

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kwa sababu ya muda sitaweza kuisoma. Kwa kuwa katika *Order Paper* ya leo inaonesha ajenda ya kuendelea kujadili Bajeti ya Taifa na kwa kuwa katika Bajeti ya Taifa kuna masuala mbalimbali ambayo tunaendelea kuyajadili ikiwa ni pamoja na masuala ya rasilimali za Taifa ikiwemo madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jana Mheshimiwa Rais alipokea Taarifa ya Kamati ya pili iliyoundwa kwa ajili ya kuangalia athari za kiuchumi zinazotokana na uchimbaji wa madini hapa nchini na usafirishaji wa makinikia. Kwa kuwa katika Taarifa hiyo ilionesha kuwa toka mwaka 1998 mpaka mwaka 2017 Serikali imekosa mapato ya zaidi ya trilioni 108. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameonesha ujasiri mkubwa, umakini, uzalendo na kujitoa muhanga katika kulinda rasilimali za Taifa letu. Kwa

kuwa Wabunge tunaendelea kujadili Bajeti ya Taifa inayohusu hizi rasilimali. Naomba Mwongozo wako kwa nini Bunge lako Tukufu lisiazimie kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya na ambayo ameweza. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia sana)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako ili Bunge liweze kutoa kauli nzito ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, natoa hoja. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo Miongozo ambayo inatakiwa itolewe humu Bungeni. Maana Mheshimiwa anatoa Mwongozo lakini unaungwa mkono karibu na Bunge lote. Kwa kuwa jambo hili ni zito ili likae sawasawa nahitaji ushauri wa kuliweka vizuri zaidi. Mheshimiwa Haonga, binafsi meza yangu nimelipokea. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Hasunga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, samahani, narudia tena, Mheshimiwa Hasunga. Kwa hiyo naelekeza kwamba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wote mliopo mara moja mkutane kwenye ukumbi wa Spika hapa *(Speaker's Lounge)*, mshauriane pale na baada ya ushauri huo mnipe taarifa ili kabla ya saa saba kuahirisha shughuli hapa tuwe tumetoa uelekeo wa jambo hili. Kikao hicho kitaongozwa na Mheshimiwa Mwenyekiti, Mussa Azzan Zungu. Naomba Wajumbe mwende. *(Makofi)*

Tunaendelea, wale wote ambao mpo katika orodha yangu, nikikutaja ukawa hupo nafasi yako itakuwa imekwishapotea, atachukua nafasi mtu mwingine. Kwa hiyo, wale wote ambao mnatarajia kuzungumza, mtapata nafasi, lakini muwepo hapa ndani. Tunaanza. Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa Kwa Mwaka 2016 na Mpango wa  
Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018  
na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na  
Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka na atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na orodha itaendelea. Tuendeleo kuchangia.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii. Naanza kabisa kwa kutoa pongezi na kuunga mkono hoja hii, bajeti iliyo mbele yetu kwa kweli imetayarishwa kwa umakini mkubwa na inahitaji kuungwa mkono. Kwa hiyo ninaposimama hapa nataka kuboresha sehemu mbalimbali ambazo nadhani Mheshimiwa Waziri akiendelea kuzifanyia kazi bajeti hii itakuwa bora zaidi kabla haijakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuokoa muda nina vipengele mbalimbali ambavyo nitaviwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri kwa maandishi, Ibara kwa ukurasa, lakini kwa ufupi tu nianze kabisa na ukurasa wa pili, Ibara ya 4. Mambo yote aliyoorodhesha na matukio makubwa yametokea na namuunga mkono, hiyo nadhani Mheshimiwa Waziri na nimewaambia wapiga kura wangu hii si kwa hila bali kwa kusahau, tukio kubwa sana lilitokea tarehe 10 Septemba, 2016, Mkoa wa Kagera ulikumbwa na tetemeko kali. Katika tetemeko hilo watu wapakoteza maisha yao na watu wapakoteza mali zao.



Mheshimiwa Spika, tunashukuru sisi wa kutoka Kagera kwamba Waziri Mkuu hakuchelewa, alikwenda kwenye mazishi na hatimaye Mawaziri mbalimbali walikuja pale kutufariji na ninyi Bunge Tukufu mkachanga mchango ambao umetusaidia kwa wale wahanga walioathirika. Nawashukuruni sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni bajeti, nilitegemea na naomba Mheshimiwa Waziri aone kwamba sisi wahanga wa tetemeko hatujioni katika bajeti hii, watu walioathirika tunaendelea kuwaleaje ili kuwasaidia kuondokana na kadhia iliyowakuta?

Mheshimiwa Spika, nina pendekezo kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba ahimiza viwanda na aviwezeshe kufungua *factory outlets*. *Factory outlet* nadhani anaelewa maana yake, ni viwanda vya vifaa vya ujenzi hususan Kiwanda cha Twiga, Dangote na hao watu wa Tanga na Mbeya wawe na maduka yao kule Mkoa wa Kagera. Zile zinaitwa *factory outlets*, ni *concept* ambayo anaelewa, ni sehemu moja ya kusaidia watu kuweza kujenga makazi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipofika kule, yeye anahangaika na shule na miundombinu tunamshukuru, lakini sasa wananchi vifaa vya ujenzi inakuwa ni ngumu kupatikana. Nitoe mfano, mfuko wa *cement 'X' factory* pale Dar es Salaam Twiga ni Sh.9,000/=; unapofika Kagera ni Sh.15,000/=. Kwa hiyo, unaona kwamba mwananchi wa Kagera, huyu mhanga wa tetemeko hawezi kwenda mbele. Hilo naamini kwamba atalifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda ku-*highlight* katika orodha yangu ya vitu kadhaa ambavyo naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, kuna *issue* ya ukwasi katika uchumi wetu. Mheshimiwa Waziri, yeye ni mchumi mwenzangu na anajua kwamba ukwasi ndiyo damu inayoendesha uchumi. Katika hili wamejitahidi sana, naomba nimupongeze kwamba katika bajeti hii mabanki yatawezesha sasa. Wamepunguza vile viwango, yaani *minimum reserve* wanayoweka kule Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, kuna sekta moja ya fedha ambayo Mheshimiwa Waziri anayoisahau, nami hapa nitangaze mgongano wa maslahi au na-*declare interest* kwamba mimi ni mdau pia wa Sekta ya Bima kama vile wengi tulivyo wadau katika Sekta ya Benki. Maana yake ukiwa na hisa katika sekta hizi, tayari umeshakuwa mdau, au siyo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. PROF. TIBAJUKA:** Sasa bima hizi; unajua ukwasi katika bima ni mbaya sana na unaendana sambamba na mabenki. Kwa hiyo, nafikiria hapo angepaangalia namna ya kuwasaidia wasije wakafunga Makampuni ya Bima, badala ya kujenga Makampuni haya tukakuta tunarudi nyuma. Kwa hiyo, hilo nalo ni la kufanyia kazi katika bajeti yetu ambayo ni vizuri.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho naomba nipongeze, tumesikia mengi kuhusu vyeti feki, Mheshimiwa Rais amekamilisha mengi. Watu ambao walikuwa na vyeti feki, nadhani sheria imefuata mkondo wake. Katika bajeti hii kuna kitu ambacho nimekiona kimeni-*strike*, kumbe kulikuwa na madai feki katika Serikali! Watu walikuwa wanadai Serikali vitu, kumbe madai yao hayakuwa halali! Naomba jambo hili tulinyooshee bango; watu wanaokwenda kuweka madai feki Serikalini, nao tuwajue, maana Tanzania ni nchi ya uwazi na ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tupo katika awamu ya uwazi na ukweli, kwa hiyo, watu kama hao waliokuwa wanakwenda kudai zaidi ya shilingi bilioni zaidi ya 900 ambazo wamezikomboa, wajulikane ni akina nani, kusudi wawe *blacklisted* wasiendeleo kutusumbua katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia hapo hapo niongezee kwamba katika bajeti hii ambayo ina mambo mengi, kuna suala la wakulima. Ninaposimama hapa, Muleba Kusini sisi ni wakulima wa kahawa, ndizi, mpunga na maharage. Sasa ukiangalia ruzuku zinazokwenda kusaidia

wakulima, Mkoa wa Kagera nasikitika kwamba hazitufikii kabisa. Katika hali hiyo, wakulima unawasaidiaje? Naomba nimpongeze na nishukuru kwamba kodi kwenye kahawa imepunguzwa, lakini bado kuna msururu wa kodi kwenye kahawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi maboresho ambayo wamefanya, hizi kodi 17 zilizoondoka, zimeondoka kwa wale ambao ni wafanyabiashara wa kahawa na viwanda vya kahawa, lakini mkulima bado amebebeshwa mzigo. Naomba Mheshimiwa Waziri yeye ni mchumi, afanye *analysis*, aangalie *cost breakdown* aone kwamba mkulima tunamsaidiaje?

Mheshimiwa Spika, nina pendekezo, hii *cess* ambayo imesemwa kwamba mazao ya biashara yanabaki kwenye 3%, tumetoka 5% mpaka 3% tunashukuru. Nataka nipendekeze kwamba mazao ya biashara sasa hivi na mazao ya chakula, yaani tofauti ni *academic*. Kwa mkulima, analima mahindi na kahawa ili auze. Sasa yule wa kahawa ambaye amebeba Taifa hili miaka mingi au yule wa korosho; ninapozungumza kahawa naweza pia kwenda kwenye mazao mengine. Kwa mfano, wakulima wa pamba, wale ambao wamebeba Taifa hili tangu uwepo wake, sasa hivi ni wakati wa Taifa kuwarudishia kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza hiyo *cess* na yenyewe iteremshwe ifike kwenye kiwango kinachostahili, wakulima waonekane sawa. Hapo sina budi kushukuru sana ukombozi ambao Mheshimiwa Waziri ameuleta kwamba mazao tani moja mtu anaruhusiwa, ni ruksa kabisa kuyatembeza. Huu ni ukombozi kwa mkulima, pia kutusaidia sisi Wabunge huko kwenye Halmashauri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napambana na Halmashauri, wanaweka *barrier* feki, inabidi niziondoe. Mambo ni mengi, lakini nitayawasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu na atafuatiwa na Mheshimiwa John Heche.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ya bajeti ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Wataalam wake kwa kutuletea bajeti hii ambayo ni muhimu sana. Bajeti hii kwa kweli imelenga hasa watu wa chini na wanavijiji. Tofauti na mwaka 2016 ambapo Mheshimiwa Waziri alikuwa anasita kidogo, lakini baada ya kusikia kilio chetu kikubwa, ameweza kuifanyia marekebisho bajeti hii kwa kiwango cha hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuondoa tozo na ushuru mbalimbali, lakini bajeti hii ingekuwa na umuhimu zaidi katika suala la maji ambapo Mheshimiwa Waziri amelisahau kwa kiwango kikubwa sana. Bajeti iliyopita ya mwaka 2016 kwa kweli fedha za maendeleo kwenye Wizara ya Maji zilitolewa kwa kiwango kidogo sana. Kiwango cha asilimia 19 na *point something* ni kidogo sana. Sasa safari hii tulitegemea kwamba Wizara ya Maji itaongezewa na itapata kwa kiwango kikubwa sana fedha ambazo zingeweza kutosha hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nakubaliana kabisa na mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati ya Bajeti ambayo kwa kweli ilishauri kwamba asilimia 70 ya mapato ambayo yanakwenda kwenye mfuko, yaende kwenye Mfuko wa Maji. Suala hili lingeweza kusaidia sana maji vijijini. Kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri aangalie suala hilo, ahakikishe kwamba *atleast* asilimia 70 katika Mfuko wa Maji unaongezewa ili wananchi wa vijijini waweze kuwa na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la miradi 16 ambayo ilijadiliwa, tulipewa mkopo wa Dola milioni 500 kutoka India.

Naamini kwamba fedha hizi zikiweza kupatikana, zitaweza kuondoa matatizo ya maji kwa kiwango cha hali ya juu. Kwa sababu miradi 16 na miradi ambayo imesambaa nchi nzima, kila siku tunaambiwa kwamba kuna *financial agreement* ambayo inatakiwa isainiwe, tangu mwaka 2016. Mheshimiwa Waziri tafadhali sana, suala hili lipo kwenye mikono yake na kwenye Wizara yake, ahakikishe hiyo *financial agreement* inasainiwa ili kazi hii iweze kufanyika kwa bidii.

Mheshimiwa Spika, nilishauri wakati nachangia suala la bajeti ya madini na nishati kwamba sasa hivi ni lazima tuanzishe kiwanda cha kusafishia haya makinikia. Bila kuanzisha kiwanda hiki, Bunge halitaonekana linaunga mkono vizuri juhudi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, jana kwenye mapendekezo ya Kamati, suala hili limetolewa kwamba *atleast* lazima tuwe na kiwanda hicho hapa, sasa huo ni mlango wa kutokea. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri aangalie bajeti yake, ajaribu kuifumua kuhakikisha kwamba tunakuwa na hiki kiwanda tuweze kuondoa haya matatizo mengi kwa sababu taarifa ambayo imetolewa jana, kwa kweli inasikitisha. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni inafanya kazi hapa bila kuwa na leseni, kampuni imechukua madini chungu nzima, kuanzia miaka ya nyuma, matrillioni ya hela. Kwa kweli ni *very absurd*, sikutegemea kwamba kitu kama hicho kingeweza kutoka kwenye ripoti hiyo. Wametuachia mashimo! Wametuachia mahandaki! Kwa kweli sasa hivi *never, never, never ever again*, hatuwezi kukubali kuendelea kuwa na mahandaki humu ndani wakati tuna uwezo wa kufanya kila kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu Mheshimiwa Waziri aangalie suala hilo la uanzishwaji wa kiwanda na ni vizuri hata kama tutabaki na haya mahandaki, tubaki na haya mahandaki na mali zetu ziwe chini, lakini hatutakubali tena sasa hivi kutoa michanga kwenda nje kama alivyosema Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama kuna hizo kesi sasa hivi, sisi ndiyo tuna hoja. Sisi ndio tunatakiwa, kama wakikataa kukaa kwenye makubaliano, sasa hivi tuna hoja ya kuwashtaki sasa kuhusiana na fedha zote ambazo wameiba. Ni lazima tuhakikishe kwamba zinarudi.

Mheshimiwa Spika, suala la utalii utaona kwamba mchango kwenye pato la Taifa umepungua katika mwaka 2015/2016. Tumechangia kwenye asilimia 14 ukilinganisha na asilimia 17.5 ya mwaka uliopita. Hii ni kwa sababu ya VAT. Sasa ni vizuri Mheshimiwa Waziri akaliangalia hilo suala na kuhakikisha hii VAT ambayo inachajiwa. Hili tumelipigia kelele sana kwenye bajeti iliyopita. Kwa hiyo, ni vizuri kuiangalia, pia tuondoe hiki kitu, tupate watalii wengi ili tuweze kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni reli ya Tanga - Arusha na Musoma. Reli hii sasa hivi tunasubiri taarifa ya *feasibility study* ili iweze kuiuza kwa wafadhili kwa njia ya PPP. Sasa bado haijalipwa hela na Kamati ya Bajeti imeshauri vizuri kwamba fedha za kulipa *feasibility study*, basi zitoke kwenye Mfuko wa Reli ili tuweze kulipa mara moja. Kwa hiyo, ningeshukuru sana kama suala hilo lingetiliwa maanani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho, suala zima la bajeti, bajeti ni nzuri lakini tunaomba utekelezaji wake, bajeti ikitekelezwa kwa kiwango ambacho tutaipitisha hapa basi itakuwa na maana, lakini kama bajeti tunapisha na haitekelezwi, kwa kweli inasikitisha sana. Sasa ni vizuri kutengeneza bajeti ambayo tunaweza kuipitisha. Tutakapoipitisha, itakuwa ni vizuri sana na papo hapo ni muhimu kuweka maanani kwamba siku hizi nchi nyingi hazi-include suala la wafadhili ambao wana-support kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri ufadhili ambao unatolewa usiingie kwenye bajeti kwa sababu mara nyingi unakuta wanapoahidi kwamba watachangia bajeti, kwenye hatua za mwisho utakuta hawachangii bajeti. Sasa ile inavuruga mipangilio yote. Ni vizuri tuweke bajeti yetu

ambayo tunaweza kutekeleza kutokana na hela zetu na hizo fedha za wafadhili zije kama ni kitu cha baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo,naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu. Tunakushukuru kwa kutumia muda vizuri. Nilishamtaja Mheshimiwa John Wegesa Heche, atafuatia Mheshimiwa Japhet Haonga. Ni Mheshimiwa Hasunga. Haya majina mawili haya! Mheshimiwa Japhet Hasunga. Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nianze kwa kuwashukuru sana wote ambao mliniombea wakati nilipokuwa naumwa. Nashukuru uongozi wa Bunge na Wabunge wote, nawashukuru sana wananchi wa Tarime, nawaambia nimepona. *I am back firing.*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kodi ya majengo (*Property Tax*). *Essence* ya kuweka *Property Tax* mijini ilikuwa ni kuweza kukusanya kodi ili isaidie kusafisha majitaka mijini; kwa ajili ya zimamoto, kwa sababu watu wanaomiliki nyumba, wanalipa kodi ya ardhi na kodi ya pango la ardhi. Sasa Mheshimiwa Waziri amepeleka kodi mpaka vijijini pale ambapo tu ili mradi mtu amejenga nyumba ya tofali na bati ambapo Serikali hawajamnunulia hawajamchangia kwenye tofali, hawajamchangia kwenye *cement* na vitu vyote hivi alinunua vimelipiwa kodi, wanataka waende kuwachaji watu maskini wa vijijini kodi ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo baya na halikubaliki na ni lazima kwa kweli walingalie, wa-*recitify* hili, huwezi leo kwenda kuwachaji watu ambao huwapelekei huduma ya zimamoto wala huduma ya majitaka, unakwenda kuwachaji pesa ya kodi ya *property tax*, unawachaji kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, la pili, wanaondoa *Property Tax* kwenye Halmashauri ambapo kama leo wanafuatilia Kenya; jambo ambalo linamtikisa Uhuru Kenyatta na linataka

kumtoa madarakani ni mambo mawili tu. Ni kodi, ni kushindwa kugatua pesa kwenye kitu wanachoita *County*. Wanashindwa kushusha pesa kule chini ili ziende kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo wanachukua pesa ambazo kule chini tuna Madiwani, wanalipwa ili wakae vikao, wajadili, wapange huduma kule chini; wanazichukua, wanazileta zote mjini. Leo wanataka watuambie kuwa Serikali hii ina uwezo wa kujadili Kitongoji kimoja kimoja! Kwa mfano, kule Kehero kwetu Kemakorere; wajadili maji kutoka Dar es Salaam yaende kule, haiwezekani. Ndiyo maana tulianzisha Halmashauri ziwe karibu na wananchi zione huduma ndogo ndogo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, choo kikibomoka kwenye Shule ya Msingi, asubiriwe Mheshimiwa Waziri kwa sababu amechukua *Property Tax* ndiyo apeleke pesa choo kiende kutengenezwa, watu waende kutumia! Hilo halitawezekana Mheshimiwa Waziri. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni *Road License*. Hii ni aibu! Leo wanataka kuwapelekea akinamama vijijini *Road License* wanaotumia mafuta ya taa kwenye koroboi, yaani maana yake ni kwamba kibatari wanatakiwa kukilipisha *Road License*, hii itafanyika Tanzania peke yake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili ni muhimu akaliangalia.

Mheshimiwa Spika, la tatu, uporaji wa ardhi Tarime. Kuna kiwanda kimeletwa pale, nami nimesema na mwingine alikurupuka humu, hana *research*, akaongea wakati nikiwa naumwa.

Mheshimiwa Spika, sipingi kiwanda, lakini napinga utaratibu wa ardhi ya wananchi wa Tarime ambayo ni ndogo sana inavyotaka kuchukuliwa kwa nguvu. Wanakwenda wanaweka *beacon* kwenye ardhi za watu, mashamba ya watu ambapo Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 inasema, ili uchukue ardhi ya mtu, ni lazima umlipe *fare prompt and adequate compensation*.



Mheshimiwa Spika, hilo halijafanyika, wanatumia nguvu, wanatengeneza makinikia nyingine pale Tarime. Nasi watu wa Tarime mnatufahamu; kwenye ardhi tunailinda kwa nguvu zote. Tutailinda!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vyema wakaangalia hilo la ardhi. Juzi wamemwingiza Makamu wa Rais kwenye mkenge kwa makusudi, wanataka kupora ardhi waweke pale kiwanda, mwisho wa siku itakuwa kama hili la makinikia ambalo tumelisema miaka yote, unamchoma mtu kisu halafu unachomoa unamchekea, yaani CCM iliwachoma Watanzania kisu kwenye madini sasa imechomoa kisu halafu inashangilia. Hayo ndiyo yanayotaka kufanyika pale. Kwa hiyo, ni muhimu yakaangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la nne, ni suala la madini. Kama kuna watu wameumizwa, kama kuna watu wana vilema, kama kuna watu wana kilio cha madini kwenye nchi hii, ni watu wa Tarime, ambao wamezika ndugu zao miaka na miaka, kwa sababu ya kupigania madini yao yaliyokuwa yanaporwa na sasa wamethibisha yale tuliyoyasema kwamba madini yalikuwa yanaporwa miaka yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili nashauri kama Rais yupo *serious alete constitution amendment* hapa tuwaondolee kinga Rais Mkapa na Rais Kikwete wachunguzwe kwenye suala hili la madini. Baraza la Mawaziri, wanajua wanavyofanya kazi, huwezi kuniambia kwamba Mheshimiwa Daniel Yona aliondoa *fifteen percent* yetu peke yake bila *concert* ya Rais.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kama leo Rais anavyonunua *Bombadier*, haijapitishwa kwenye utaratibu wa kibajeti, haiko popote, uje uniambie kwamba kuna Waziri hapa anaweza kumwambia Rais tusifanye hivi? Au Rais mwingine mwaka unaokuja aje amkamate Mheshimiwa Mbarawa bila Rais kuchunguzwa! Kwa hiyo, tunataka *constitution amendment*, hawa watu wachunguzwe waonekane nini mkono wao kwenye hili suala? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kwa sababu wamedhibitisha kwamba *Acacia* ni kampuni *fake*, ni kampuni hewa ambayo haipo na iko Tarime inawaibia wananchi wa Tarime, kuanzia leo nawaambia wananchi wa Tarime wajandae tuingie mle mgodini tuchukue kila kilicho chetu. Nami hili nalisema humu na nitalifanyia kazi na sidanganyi kwa sababu wananchi wa Tarime wameumizwa na kampuni ile Rais amesema ni *fake* na hakuna *formula* ya kukamata mwizi.

Mheshimiwa Spika, mlisema wenyewe na Bunge limesema, *formula* ya kukamata mwizi ni kupambana naye. Sisi hatutaruhusu madini yatoke pale. Ndege ikitua, itapigwa mawe na hilo linaendelea na *organization* pale. Magari yao tutayakamata. Kwanza tunawadai fidia nyingi kweli kweli, pale Tarime. Tunataka hayo mambo yafanyike sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sisi tulitegemea tumwone Rais anaagiza kwamba kuanzia sasa madini yoyote yasiondoke nchini mpaka hayo mambo yote yapitiwe, tutazuia mchanga, dhahabu inaondoka. Hili halieleweki! (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche namwona Mheshimiwa Kigwangalla amesimama mahali pake.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, naomba ulinde muda wangu tafadhali.

**SPIKA:** Nakulindia muda muda wako.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kauli anazozitoa Mheshimiwa John Heche ni kali, lakini pia zinataka kukiuka misingi ya utendaji haki na misingi ya sheria. Alichokifanya Mheshimiwa Rais ni kufanya uchunguzi kwa kutumia wataalam ambao wamejiridhisha na wameleta taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuleta taarifa kuna utaratibu mahususi wa kiserikali ambao utatumika

kuchukua hatua dhidi ya mtu yoyote yule ambaye ameguswa kwenye mikataba inayozungumziwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hajasema wala hajaelekeza wananchi tuchukue sheria mkononi kwenda kuanza kuvamia mali ama kwenda kunyanyasa watu wengine. Ndiyo maana katika maagizo yake Mheshimiwa Rais ameagiza Wizara zinazohusika ziende zikatazame namna gani zitazungumza na hao wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ile mali iliyoko pale inawezekana siyo mali ya *Acacia*, ni jambo linalozungumzika, lakini ni mali iliyowekezwa na mwekezaji aliyekuwepo kabla ya *Acacia*. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile ile mali pale siyo ya watu wa Tarime wala siyo halali kwa Mheshimiwa Heche kuhamasisha wananchi wake wakafanye vurugu kwa sababu watachukuliwa hatua na vyombo vya dola. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche bado una muda, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, sipokei. Nami nilijua tangu mwanzo kwamba hamtavumilia tupigane vita hii. Mnafanya mambo ya ukinyonga.

Mheshimiwa Spika, mwizi hana *formula*. Mheshimiwa Rais amesema *Acacia* ni mwizi. Yaani wewe unataka tupate utaratibu wa kukamata mwizi Tarime? Sisi watu wetu Mheshimiwa Spika wewe unajua ukiwa Naibu Spika, wameumia na maji ya sumu. Ngombe wamekufa, watu wamepigwa risasi kwa mujibu wa ripoti ya Waziri wa Nishati na Madini; watu wa Tarime zaidi ya 64 wameuawa; na hao ni kwa mujibu wa ripoti ya Mheshimiwa Waziri peke yake. Wameuawa pale mgodini Serikali hii ikilinda wezi wa *Acacia*. Ndiyo maana nasema watu wengine tuna machungu na tuna maumivu na hili.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema na kama mtanikamata, Watanzania watajua hamko tayari kupigana

vita hii ya kuokoa rasilimali hizi. Watu wa Tarime wajiandae waanze maandalizi, tuone atakayeenda kulinda mwizi pale, tumwone! Kama Serikali hii itaruhusu Polisi waende kulinda magari ya mwizi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye haya ya madini, rasilimali za nchi hii zinazoibiwa siyo madini peke yake, wala siyo *Acacia* peke yake inayotuibia. *Geita Gold Mine* inatuibia, magogo ya nchi hii yanasafirishwa nje bure. Twigwa walisafirishwa kutoka kwenye nchi yetu hii, wengine wako humu tunawafahamu, waliosafirisha twigwa wako humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Loliondo wanalia mpaka sasa hivi kwa rasilimali zetu zinazoibiwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche, muda wako umeisha.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unga mkono hoja.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Heche. Waheshimiwa Wabunge, msione nilinyamaza, hiyo ndiyo lugha ya Tarime. Kule Tarime, lugha anayoongea Mbunge wao, wao wanaelewana. Ninyi msiwe na wasiwasi hata kidogo. Huko ni lugha ya Kimura huko! Kule lugha ya Kipemba yakhe yakhe, hakuna yakhe kule. Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kabisa kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa bajeti nzuri ambayo amelleta Bungeni, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii bajeti kwa kweli inatekelezeka, ina vipaumbele ambavyo vinakuna maisha ya kawaida ya Watanzania na ina mambo mazuri. Kwa hiyo, nadhani kazi yetu sisi kama Wabunge ni kuendelea kushauri labda marekebisho au nyongeza, mambo gani yaongezewe katika hii bajeti ili iweze kuwa nzuri zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie kwenye Sekta ya Kilimo. Kwenye Sekta ya Kilimo inaonekana kwamba kilikua kwa asilimia 1.7 kutoka asilimia 2.1. Sekta ya Kilimo ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi hii. Kuna sekta ambazo tukiweka nguvu ya kutosha tunaweza tukaleta maendeleo ya kweli katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, labda nitaje sekta chache. Tukiweka nguvu kwenye Sekta ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, tukafanya vizuri, tunaweza kutoa mchango mkubwa sana katika nchi hii. Sekta hii ndiyo inayotoa ajira ya Watanzania walio wengi. Zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo. Kwa hiyo, lazima tuiangalie. Sekta ya Nishati na Madini, tumeona madini yako mengi. Tukiimarisha hii, tukaweka vipaumbele vizuri, tukaifanyia vizuri, tutakuwa hatuna shida ya fedha za kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Maliasili, ukiangalia mbuga za wanyama tulizonazo, ukiangalia mlima mrefu katika Afrika na wa pili duniani, ukiangalia mambo mbalimbali yanayohusiana na utalii, tukiyawekea mkazo mzuri, tunaweza tukafanya kazi nzuri na maendeleo ya nchi hii yatakimbia haraka sana.

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa kwenye Sekta ya Kilimo. Kwenye kilimo Serikali imesema, sasa hivi kwenye upande wa pembejeo wamesema tutafanya *bulk procurement*. Ni imani yangu kabisa kwamba Serikali itatekeleza mwaka huu vizuri kabisa. Tukifanya hivyo, pembejeo zitashuka bei na kuwawezesha wakulima wetu kuweza kupata pembejeo kwa bei nzuri na hivyo kuongeza tija na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kwenye Jimbo langu la Vwawa, Wilaya ya Mbozi, sisi ni wakulima sana, lakini tunahitaji pembejeo zije kwa wakati na kwa bei nzuri. Hiyo itatusaidia sana kuchangia mchango mkubwa katika Taifa hili. Pia kuna zao la kahawa ambalo lilikuwa linaongoza Tanzania kwa kutuingizia fedha za kigeni. Zao hili sasa limeshuka, sijui sasa limeshika nafasi ya sita! Lazima Serikali tukae chini tuangalie nini kimetokea kwenye zao la kahawa ili tuweze kulifufua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeona kabisa sasa hivi mazao kama korosho yameanza kuongezeka na yameongeza mchango mkubwa, lakini zao la kahawa, nini kimetokea? Hebu Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu aangelie nini tufanye katika hilo?

Mheshimiwa Spika, kwenye ufugaji tuondokane na uchungaji, twende kwenye ufugaji wa kisasa. Sasa hivi hakuna ufugaji wa kisasa, kuna uchungaji katika nchi yetu. Tukifanya hivyo, tukiwa na mashamba ya ufugaji, naamini kabisa tutaona mchango wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna bahari kuu kule, kuna *deep sea*, hatujaweka jitihada za kutosha kwenda kuvua. Wananchi wetu wanakufa, watoto wetu wanakufa kwa magonjwa mbalimbali yanayotokana na ukosefu wa chakula. Tungekuwa tumeimarisha uvuvi tukapata samaki, tukawalisha wananchi wetu, mimi naamini hata magonjwa yangepungua. Kwa hiyo, nadhani jitihada lazima zichukuliwe

na Serikali katika kuimarisha hii Wizara ili tuhakikishe kwamba inatoa mchango mzuri katika kuimarisha uchumi huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili katika upande wa kilimo, nimeangalia sana hii bajeti, inazungumzia *subsistance agriculture*. Hatuwezi kuendeleza nchi kwa kilimo kidogo kidogo hiki, lazima kama nchi twende kwenye *commercial farming*. Bila kwenda kwenye *commercial farming* hatutafika. Lazima jitihada ziwekwe. Nimeangalia mkakati, bado hautoshi, *commercial farming* bado haipo. Huwezi kuleta maendeleo ya nchi kama hakuna *commercial farming*, huwezi!

Mheshimiwa Spika, sekta hii ambayo tunasema inatoa ajira kubwa, watu wengi *are not included*. So, kwenye ile tunaita *financial inclusion* wengi hawapo *included*. Huwezi kuwa- *support* mmoja mmoja, lakini kukiwa na kilimo cha kisasa, kukiwa na maeneo au mashamba yametengwa, tukazalisha vizuri, tutatoa ajira nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuchangia, nimeona watu wengi wamechangia kuhusu *Property Tax*, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema *Property Tax* sasa itakuwa inakusanywa na Wizara ya Fedha kupitia *TRA*. Naomba niliweke vizuri. Mheshimiwa Waziri alichosema, hajasema *Property Tax* yote itakusanywa na *TRA*. Amesema kwa mwaka huu wanaanza na miji, fedha zitakusanywa na *Property Tax* na *TRA* na baada ya kukusanywa ndiyo zitapelekwa sasa, zitarudishwa huko.

Mheshimiwa Spika, huko vijijini bado hawawezi kufika, itakuwa bado ni kazi ya Halmashauri. Hebu tuangalie bajeti ya maendeleo. Maendeleo ya nchi hii tunapozungumzia bajeti ya maendeleo ya nchi hii, maendeleo yanayofanywa na Serikali Kuu yanahusu nchi nzima bila kujali ni wapi. Tumeona sasa hivi *flyover* zinajengwa pale Dar es Salaam, tunasubiri zije hata huku Dodoma zijengwe *flyover* maana huku ndiyo Makao Makuu ya Mji, tunahitaji maendeleo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inapokusanya, nami naona kabisa kuna *logic*. Hebu makusanyo haya tuyakusanye mahali pamoja ili tuweze kutekeleza vipaumbele vile ambavyo vitachochea maendeleo ya nchi. Hii kutawanya mapato mara huku, mara huku, ndiyo kunakuwa na wizi na matumizi mabaya ya fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye Halmashauri yangu kule matumizi ya fedha yalivyo. Makusanyo watu wengi wanaiba. Hata ukiwaambia watumie vifaa vya *ki-electronic*, wanakuwa navyo lakini hawatumii, wanaiba. Hawa wenye uzoefu wa kukusanya, wakikusanya zikakaa kwenye kapu moja, tutatenga vipaumbele, tutaelekeza kwenye vipaumbele na maendeleo yatakimbia haraka sana, tutaona nchi yetu inaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri, ni vizuri, maana uzoefu unaonesha kule kwenye Halmashauri zetu zipo Halmashauri sasa hivi hazina uwezo wa kulipa posho za Madiwani. Fedha hizi zikikusanywa zikaanza kupelekwa kule, watatekeleza miradi ya maendeleo, wataweza kufanya mambo mengine, watalipana hata posho za Waheshimiwa Madiwani, kuliko ilivyo sasa hivi makusanyo hayaridhishi katika maeneo mengi kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, naunga mkono hoja, lazima Serikali ikusanye makusanyo pamoja ili yaweze kutoa mchango mzuri na maendeleo ya nchi yaweze kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kule Jimboni kwangu, ile asilimia 20 inayotakiwa irudi kwenye vijiji, hairudi. Wakikusanya zinatumiwa hovyoy. Hawawarudishii wale wakusanyaji. Usipowa-*motivate* wakusanyaji, kesho hawawezi kukusanya, nao wanatafuta mbinu nyingine za kuweza kujilipa wenyewe. Kwa hiyo, lazima mikakati iwekwe vizuri ili kuhakikisha kwamba hii fedha inakusanywa na inawekwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hii Sekta ya Utalii mwaka 2016 tuliweka *VAT*. Hebu tuangalie, idadi ya watalii waliongia kwenye nchi hii inaonekana wameongezeka, lakini



ukiangalia mapato yanayotokana na Sekta ya Utalii, bado siyo mazuri ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya.

Mheshimiwa Spika, hii inatupa kwamba kuna mambo lazima tuyafanye kwenye Sekta ya Utalii ili tuweze kuhakikisha kwamba hii sekta inatoa mchango wa kutosha katika kuiendeleza nchi yetu. Naamini tukiweka mikakati mizuri, tukatathmini ile *impact ya VAT*, maendeleo ya nchi hii yatabadilika kwa haraka sana. Ni muhimu haya mambo yakaangaliwa kwa mapana na marefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja na juhudi zote zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuwatetea na kuleta maendeleo ya kweli katika nchi hii. Sote lazima tushikamane; na hivi ni vita, lazima wote tupigane katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya kweli. Hizi tofauti za kisiasa hazitusaidii kutupeleka kokote, hebu tushikamane kuleta maendeleo ya kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Nilishamtaja Mheshimiwa Danieli Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake nzuri aliyotoa. Wale mnaokumbuka, kwa miaka 10, 15 iliyopita, hii ni hotuba ya pili kwa ubora. Hotuba ya kwanza ni ile ya wakati ule wa Mzee Mkapu aliyotoa Mzee Mramba kufuta kodi, *Nuisance Taxes* kama mnakumbuka mliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii kwa ubora wake imejikita kuondoa matatizo na mizigo kwa wakulima wetu na watu wa kipato cha chini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango

hongera sana, kama nilivyokwambia siku ile, ulikuwa kwenye *form* vizuri na ulifanya kazi nzuri, hongera, tena hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine bila kusahau, unakumbuka wewe na mimi tulikwenda *North Mara* kipindi kile kwenye vurugu ya Mto Tigite wakati kuna zile tuhuma kwamba yale maji ya Mto Tigite yameua watu wengi sana kule. Naomba kwa namna ya pekee Waheshimiwa Wabunge wote kazi ambayo ameifanya jana Mheshimiwa Mzee Magufuli ni kazi ya peke yake kabisa. Unaibiwa, sasa ametokea jasiri kusema jamani tunaibiwa, tusiibiwe, huyo amekuwa mbaya? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasema, nawe tumekusikia jana uliona ile nguvu iliyokuwepo pale, mmefanya kazi nzuri sana, hongereni. Tunaibiwa na kama alivyosema Mbunge mmoja, sasa basi, tusiibiwe tena. Maana mtu kama anakuibia, kwanza anakudharau. Nasi tunasema hao Wazungu waliokuwa wanatuibia, sasa basi tumeona. Tumsaidie Mheshimiwa Rais, rasilimali za Taifa tuzilinde. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa shahidi yangu, wala siyo madini tu, wewe unajua ni maeneo chungu nzima. Ile *spirit* kwamba sasa tupitie maeneo yote yenye fedha, yanayozalisha fedha katika nchi yetu, tuyapitie yote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilibahatika mwaka 2009, niliongoza Kamati Ndogo kwenda Mwadui, tukiwa na Mheshimiwa Mzee Shellukindo kama mnakumbuka. Tulipofika pale Mwadui, Williamson Diamond, tuliyoyakuta pale ni mambo ya aibu. Wale *De Beers* wamekopea *shares* zetu kule London bila sisi wenyewe kujua. Tulikuwa na Mbunge wakati ule Bwana Mpendazoe, alikuwa ni *Board Member* kwenye ile *group* ya *Williamson Diamond*. Wanasema walikwenda London pale wakakuta hisa zilishauzwa na Serikali haijui.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami nakubaliana nawe kuunda Tume Ndogo kwenda Mwadui pale kuona. Ni uchafu uliopitiliza kwamba *shares* zetu za Serikali ya Tanzania ndizo

*De Beers* alikwenda kukopea na kuanzisha migodi, Niger na Namibia. Mambo ya aibu kabisa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii vita ni kubwa, nina hakika Mheshimiwa Rais peke yake haiwezi. Ni lazima tumuunge mkono kama Bunge, tusimame pamoja kulinda rasilimali za Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitakuwa na machache tu. La kwanza, nianze na miradi ya kipaumbele. Mheshimiwa Waziri tangu bajeti iliyopita na bajeti hii tumezungumzia habari ya miradi ya vipaumbele. Mimi nataka nijikite kwenye miradi hii ya kipaumbele; nianze na mradi wa kujenga reli ya kati. Tumeanza vizuri, lakini bado tunawakumbusha na hasa wenzetu wa Hazina ambao ndio mnatoa fedha na kumshauri Mheshimiwa Rais, endeleeni kumkumbusha kwamba hii reli ya kati itakuwa na faida kubwa zaidi kama itaanza kwenda Kigoma kabla ya kwenda matawi mengine; na sababu ziko wazi; ni za kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule Kigoma ndiyo kuna mzigo ambao utaifanya reli hiyo iwe na faida kiuchumi. Mzigo uko Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo ya Mashariki. Hilo tumelisema sana. Sasa kwa sababu kuna mkakati huo, nashauri, wakati anatafutwa Mkandarasi wa kujenga tawi la Tabora kwenda Mwanza, wakati huo huo atafutwe Mkandarasi kujenga tawi la kwenda Kigoma ili tuwahi ule mzigo wa *DRC* ambao utaifanya hii reli ya kati iwe na maana kiuchumi. Mzigo mkubwa uko *DRC* na kila mmoja anafahamu. Siyo *DRC* tu, hata hii Msongati ya Burundi ambapo kuna *nickel* nyingi, maana yake ni karibu zaidi na Bandari ya Kigoma, ni karibu kabisa na *Station* ya Uvinza ambayo iko katika Mkoa wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda niliseme, Mheshimiwa Waziri alikwenda Korea ya Kusini wakasaini mradi unaoitwa *North West Grid* ambao unatoka Mbeya – Sumbawanga – Katavi – Kigoma – Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha na kwenye kitabu chake amezungumza mradi huu, napenda kujua vizuri, huo mradi unaanza lini? Unaanzia wapi? Kwa sababu kutoka Tunduma pale mpaka Nyakanazi ni kilometa zaidi ya 2,000. Ni dhahiri kabisa kwamba huo mradi utakuwa na maana kama utakuwa hauna Wakandarasi wengi, mmoja atokee Tunduma aje Sumbawanga, aje Katavi na pengine mwingine atoke Nyakanazi kuja Kigoma. Nina hakika kama ni Mkandarasi mmoja itachukua miaka mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia habari ya uchumi wa viwanda, maana yake ni pamoja na kuwa na umeme wa viwandani. Maana huu umeme wa REA ni mzuri, lakini ni dhahiri kwamba ni umeme ambao hauimarishi viwanda kwa sababu siyo umeme mwingi sana. Kwa hiyo, napenda sana kujua hilo kwa sababu yeye mwenyewe alisaini mkataba ule pale Korea Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilisitize kwenye Mpango wa Kipaumbele ni pamoja na barabara. Kwanza hongera kwa barabara hii ya Tabora. Sisi tukisikia barabara ya kwenda Tabora, maana yake hiyo barabara inakwenda Kigoma.

Mheshimiwa Spika, tumeshukuru sana hii barabara ya Chaya – Nyahua, imepata fedha, tumeshukuru sana, maana yake inakwenda mpaka Kigoma. Tunashukuru pia kwamba juhudi ziko kubwa na tumeshapata fedha kujenga kipande cha Daraja la Malagarasi kwenda Uvinza kwa fedha za *Kuwait Fund*. Sisi kwetu ni faraja kubwa sana. Napenda hiyo juhudi iunganishwe na ujenzi wa barabara ya kimkakati ya kutoka Kigoma kwenda Nyakanazi. Barabara hiyo imetengewa fedha, lakini fedha kidogo sana, shilingi bilioni 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikurejeshe, Sera ya Ujenzi wa Barabara za nchi hii, tumeshakubaliana huko nyuma, Sera ya Ujenzi wa Barabara na Sera ya Chama cha Mapinduzi

kwamba tutaunganisha mikoa na mikoa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, waende kwenye misingi ya Sera ile kwamba mikoa ambayo haijaunganishwa na mikoa iwe ndiyo kipaumbele Waheshimiwa Wabunge. Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na Katavi, haujaunganishwa na Geita, haujaunganishwa na Kagera na pia haujaunganishwa na Shinyanga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lazima twende kwenye misingi hiyo. Hizi barabara nyingine za Wilaya kwa Wilaya, Tarafa kwa Tarafa, Kijiji kwa Kijiji zisubiri kwanza. Kwa sababu nchi hii lazima ufanye *equalization*, lazima Keki ya Taifa tunufaike nayo wote. Kama tunasema tunajenga kuunganisha mikoa kwa mikoa basi, iwe ndiyo kipaumbele na iwe ndiyo mtazamo wa Hazina na uwe ndiyo mtazamo wa Serikali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumze habari ya vyeti *fake*, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi yuko hapa. Nashauri tu, kazi nzuri sana imefanyika kubaini vyeti *fake*, lakini waende sambamba na kufanya kitu kinaitwa *performance audit*. Kuwa na cheti halali hakufanyi mtu awe bora. Ndiyo ile hadithi kwamba afadhali kuwa na cheti *fake* kuliko kuwa na akili *fake*. Fanyeni *performance audit* ya Watumishi wa Umma hawa tuweze kujua kwamba hawa watu kweli wana manufaa na wana tija katika uendeshaji wa shughuli zetu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, pia nipendekeze jambo moja tu kuomba Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mazingira kwa Mheshimiwa Makamba pale na Wizara ya Maji, waje na mkakati *comprehensive* wa namna ya kulinda mito yetu katika nchi hii. Mito inakauka, Ruaha iko *threaten*, Malagarasi iko *threaten*. Naomba sana, mje na kitu *comprehensive* kwa ajili ya kulinda mito mikubwa hii ili tuweze kuendelea kuwa na rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. Sasa namwita Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Deodorus Kamala na Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae na atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Lijualikali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sasa ni sauti kutoka Pemba ya kiyakhe inataka kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah-wataalah* kutujalia uzima na afya njema. Leo ni siku ya nane kwenye Kumi la *Maghufira*. Baada ya hapo, naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani yaliyokuwa mazuri sana. Nawapongeza Viongozi wetu Wakuu wa UKAWA, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Riziki pamoja na Mheshimiwa Mbatia. Tunaenda kwenye bajeti hii ambayo ni kiini macho, kizungumkuti na bajeti ya kusadikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ambayo haitarajii kuondoa maumivu waliyonayo Watanzania kwa sababu zifuatazo: la kwanza, ikiwa tumefikia wakati tuna deni la Taifa shilingi trilioni 50.8 na tumejipangia sisi wenyewe kwenda kulipa kwa mwaka shilingi trilioni 9.6, ina maana kwamba tunaenda kulipa shilingi bilioni 788 kwa kila mwezi. Sambamba na hilo, kuna mishahara shilingi bilioni 600. Kwa hiyo, jumla itakuwa kwa kila mwezi tunatakiwa tulipe shilingi trilioni 1.3 na ushee, lakini makusanyo unaambiwa ni shilingi trilioni 1.4. Ina maana ni bajeti ya kusadikika, bajeti ya kufikirika, ni bajeti ya kwenda kulipa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nashangaa na hilo. Watu wanapiga makofi, kumbe tunaenda kulipa madeni tu sisi. Ninachohisi ni kwamba wakati huu mzunguko wa fedha haupo, umaskini unaongezeka, mfumuko wa bei uko juu na juzi tarehe 8 saa 4.10 niliuliza swali hapa Bungeni kwamba katika hiyo APRM Serikali mnajitathmini kiasi gani katika hali hii ya uchumi?

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali ninayo hapa. Walisema kwamba; changamoto waliyonayo ni ukuaji wa uchumi usiowiana na kupungua kwa umaskini. Uchumi unakua, umaskini haupungui. Leo Mheshimiwa Waziri wa Mipango anakuja anasema aah, umaskini unapungua. Siku hiyo hiyo moja, Serikali hiyo hiyo moja! Tofauti ni dakika tu. Tutakwenda kweli? Nashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapokwenda kuongeza shilingi 40/= za mafuta huko vijijini, wakati wanaotumia, wanaokoboa na kusaga mashine zao, wanaangalia kinachoongezeka kwa siku vijijini. Wanatumia *generator*, wananunua mafuta ya dizeli; ina maana umewaongezea mzigo wale watumiaji maskini ambao ni wakulima. Halafu unasema unapambana na umaskini. Kuna kitu hapo? Hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shilingi 40/= iliyoongezwa huko vijijini ni taabu kweli. Wakoboaji na wanaosaga mashine zile pale huko basi ni shida. Sasa Mheshimiwa unaposema kwamba unataka kuwakomboa maskini, ni kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa. Wala wananchi wa Tanzania hawahitaji maneno yenu ya kitaalam, sijui urari wa kibiashara, deni himilivu eeh, mnasema kwamba maoteo hayajakamilika, amana za benki hazijaiva bado mbichi, madeni chechefu. Hawahitaji hayo madeni chechefu! Maoteo ya fedha yameota mbawa; amana za benki hazijaiva. Zikiwa mbichi? Ndiyo nikasema kama Bunge hili lingekuwa *live* tukawaambia wananchi haya madeni chechefu, maoteo hajakamilika, amana za benki bado mbichi, hazijaiva vizuri, wananchi wakatusikia, twende kwenye uchaguzi mtazame kama hamtatumia nguvu ya dola nyie. Tuseme sisi na nyie msemi yenu mtazame. Hamtaki kuweka *Bunge Live* kuwaambia ukweli wananchi. Ni hilo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba niendee. Kinachonisikitisha, alipotuachia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mwishoni tulikuwa tuna deni la Taifa shilingi trilioni

39.1. Ndani ya mwaka mmoja na nusu tumeongeza shilingi trilioni 11. Tuliondoka na shilingi trilioni 39 *point*, leo tuna shilingi trilioni 50.8. Mwendu kasi. Hapa kazi kweli mwaka huu za kulipa madeni. Nashangaa. Hii haihitaji kufikiri sana na utaalam, madeni chechefu kweli mwaka huu, tutafika kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 50 vijijini ni ndoto. Hamna uwezo wa kutekeleza, imekuwa ni hadithi za hapa na pale, paukwa pakawa. Mimi natoka, shauri yenu, mtajua wenyewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud, deni chechefu ndiyo kitu gani? *(Kicheko)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Aaah!

Mheshimiwa Spika, deni chechefu ni deni baya lililokuwa huna; maana huwezi kulilipa kwa ufupi, ndiyo deni chechefu. Madeni yao chechefu, maana huna hakika ya kuyalipa. Madeni chechefu eeh, maoteo ya fedha, amana za benki hazijaiva bado mbichi, urari wa biashara. Wananchi wanataka nini bwana? Wapeni fedha wananchi sogezeni huko! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna bajeti ya kupandisha mishahara ya wafanyakazi, hakuna. Ndogo sana! *Pension* ya wazee, watu ambao wametulea, hakuna *pension* ya wazee wasiojiweza. Hawana bajeti hawa. Wanasema aah, tunapunguza umaskini, deni chechefu. Haya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa ukanda ambao unataka uzalishe uvuvi katika Bahari Kuu, amesema Mheshimiwa Mbunge wa kule juu, mrefu mrefu kama mimi kidogo hivi; amesema kwamba uvuvi katika Bahari Kuu bado haujapewa nafasi yake. Ina maana ukiambiwa je, Serikali ina bajeti ya kununua meli za kisasa za uvuvi ambazo tutaweza kuvuna mazao yetu kwenye Bahari Kuu? Serikali hamna bajeti, hakuna kitu. Hawana! *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, sisi siku zote tule samaki kutoka China. Nunueni meli ya kisasa, meli kubwa za uvuvi ziende katika Bahari Kuu tuvue samaki. Samaki wanakufa tu huko! Eeh, hawana kitu! Hee, shida mwaka huu. Nashangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukija kwenye afya, Watanzania ambao afya zao wanataka ziende vizuri, bajeti ya Afya kwa Azimio la Abuja 15% ya shilingi trilion 32 waulize, wameweka? Hakuna. La kwanza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, ukiangalia katika magonjwa makubwa sasa ambayo yanasumbua Tanzania, ni suala la *TB*. *TB* hivi sasa kwa mujibu wa wataalam ambao wametupa semina juzi, wagonjwa wa *TB* kwa kila siku wanakufa 150. Ni mabasi maana yake yanapotea, lakini ukiwaambia je, ni kiasi gani mmeweka fedha za kupambana na *TB*, hakuna.

Mheshimiwa Spika, kuna mkakati gani kwenye mikutano ya hadhara, mna mkakati gani katika maeneo mengine ya migodi kukomesha mambo haya na kupunguza mambo ya *TB*? Hakuna. Aah, urari wa biashara huo! *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu. Aah, mwaka huu! Ukiwaambia wastaafu, wanakwambia aah, sisi tumetoka tangu mwaka 2016, kipindi gani, tumeweka wastaafu wa chini wale Sh.100,000/=. Hivi ni kweli inatosha? Itapunguza kweli umaskini!

Mheshimiwa Spika, hii Serikali, nikasema kwamba kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, Ripoti ya *CAG*, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alisema hapa kwamba kuna wizi wa fedha karibu shilingi bilioni 92. Hii ni mkataba baina ya Shirika la Ndege la *ATCL* ilipoingia mkataba na *South African Airways* wakati wamekodi ndege kutoka China, *Air Bus*. Ndege hizi kwa bahati mbaya sana zimetusababishia hasara ambayo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, hapa imekuja wakati ndege hizi zililetwa hapa zikafanya kazi kwa muda wa miezi sita tena kwa kubahatisha. Ndege zikaondolewa zikapelekwa Ufaransa, mkazipaka rangi. Baada ya kupaka rangi, mkaziondoa mkazipeleka Guinea, mkazipaka rangi, baadaye hakuna aliyekamatwa. Deni chechefu hilo. Bado tu umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wapo, majibu ya Serikali yanasema kwamba TAKUKURU bado ipo kwenye mkakati wa kuchunguza, mnachunguza nini? Kumbe mnalindana? Wengine wakamatwe watumbuliwe, wengine wabinywe, wengine wapekuliwe. Hilo hamlijui Serikali au bado tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa! Sauti ya chombezo toka Pemba hiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifikiria kwamba Serikali hii itakuwa makini kuangalia namna gani ya kuwakomboa Watanzania katika hali ya umaskini? Ni namna gani ambapo mtapambana na umaskini? Namna gani mtadhibiti mfumuko wa bei? Namna gani ambavyo mtaangalia kwamba umaskini uliopo hivi sasa unachangiwa na mambo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasema katika ripoti yao Ukanda wa Pwani wana viwanda vidogo vidogo, sekta binafsi 82 ambavyo watajenga, lakini Serikali inasema itatoa vibali, watatoa leseni, sijui watatoa na ardhi. Ukiuliza huko Mkoa wa Pwani kwenyewe ni vichekesho.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoona ni kwamba, kwa hali tunayokwenda nayo hivi sasa ni kwamba, kuna tatizo kubwa sana, Serikali hajajipanga vizuri. Ukija kwenye mambo ya haya makinikia yanaitwa, haya sawa, kwani muda wote upungufu huu wa mabilioni ya fedha, matrillioni, Serikali iliyokuwepo; Serikali gani? Ya chama gani? Si Chama cha Mapinduzi! Serikali ipi? Mawaziri si ndio hao hao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo upotevu wa madini hayo yanayosemwa, kama kuna watu wamefanya ubadhirifu mkubwa, sawa nakubali, lakini tulipokuwa tukisema hapa Bungeni leteni mikataba, mlikuwa hamtaki kuleta mikataba. Ndiyo urari wa biashara huo. Haya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, ya mwisho?

**SPIKA:** Eeh, unga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. Bajeti ni mbaya, inaenda kuumiza Watanzania. Nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Huyu ni Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim. Sasa Mheshimiwa Munde Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi, Dkt Diodorus Kamala.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia bajeti ya Serikali. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, lakini niwapongeze Menejimenti nzima ya Wizara ya Fedha kwa kutuletea bajeti nzuri, bajeti ya kihistoria, bajeti ya Watanzania, bajeti ambayo Wabunge wengi walipigia kelele vitu vyao, leo tumeviona kwenye bajeti hii. Tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu *Motor Vehicle*. Sisi Wabunge kwenye bajeti ya fedha tulisema kwamba tunaomba *Motor Vehicle* iondolewe, Serikali imetusikia. Napata taabu kuwaona Waheshimiwa Wabunge leo hapa wanalaumu kwa nini Serikali imeondoa *Motor Vehicle* na imeweka Sh.40/= kwenye lita ya mafuta kama tozo kwa ajili ya *Road License*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana dada yangu Mheshimiwa Susan Lyimo aliongea hapa kwamba tunawaonea watu wa vijijini wanaowasha vibatari, kwa nini tunawawekea tozo ya mafuta? Mheshimiwa Msigwa pia aliongea, kaka yangu Mheshimiwa Heche ameongea hapa. Niwaulize tu, tunalipa tozo ya *Railway Development Levy*, Arusha kuna treni?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Iringa kuna treni? Mtwara kuna treni?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mbona hawahoji?

Mheshimiwa Spika, tunalipa tozo ya *REA*...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, mimi nimezaliwa Tabora tena Mjini. Toka nimezaliwa umeme unawaka kwetu, lakini natozwa tozo ya *REA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunalipa tozo ya maji, mimi kwetu mjini, kuna maji toka nimezaliwa, lakini nalipa tozo ya maji. Waache kutuchonganisha na Watanzania. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde, naona Mchungaji amesimama.

**MBUNGE FULANI:** Anataka kumbariki.

#### TAARIFA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nitoe taarifa kwamba Mheshimiwa Munde labda

amepoteza kumbukumbu. Katika hili suala mimi sijachangia kabisa, naona anasema nimeongea haya masuala. Naomba aweke kumbukumbu zake vizuri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Munde, taarifa ni hiyo tu.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Msigwa.

Mheshimiwa Spika, wamesema kuna mtu ana *generator*, kuna mtu ana mashine ya unga, kwa nini anatozwa Sh.40/= kwa ajili ya *Road License*? Wamesahau tunalipia reli, tunalipia maji, tunalipia umeme wa *REA* na sisi tunakaa mijini. Kwa hiyo, mimi wa mjini ningesema sitaki kutozwa tozo ya *REA* kwa sababu mimi sikai kijijini. Baba yangu alishakufa, mama yangu alishakufa, bibi yangu alishakufa; sina ndugu kijijini.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mtanzania, tumejengwa kwenye umoja, ndiyo utamaduni wetu, tumejengwa kusaidiana. Leo napata taabu anaposimama hapa Mbunge anatubagua, anasema kwamba hawa watu wa vijijini tunawatoza Sh.40/= wakati hawatunii barabara. Nani asiyetumia barabara? Nani ambaye hatunii barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waache kutuchanganya, waache kutuchonganisha. Sisi ni wamoja na tutaendelea kuwa wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa watu waache kuichanganya Serikali. Hawa watu wamwache Rais Dkt. Magufuli afanye kazi! Niliwahi kusema humu ndani tumwache Rais afanye kazi na anafanya kazi. Kazi yetu sisi ni kumwombea na kumuunga mkono; lakini wenzetu hawa mimi napata shida kweli, sijui wanamaanisha kitu gani? Wanakuja kuleta sababu ambazo hazina msingi kabisa hapa. Uzalendo wao ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais leo anapambana kuhusu rasilimali za Taifa. Mgogoro huu ukikaa mezani, mambo haya yakiwekwa vizuri tutapata zahanati, tutapata maji, tutapara barabara. Mheshimiwa Rais ambaye anafanya kitu ambacho ni cha ukombozi kwa Tanzania, tumeibiwa muda mrefu, tumeonewa muda mrefu, anapambana, badala ya sisi tumuunge mkono, mtu anakuja kulalamika. Halafu mtu huyo huyo anasema sina maji kwenye Jimbo langu, sina zahanati kwenye Jimbo langu, rasilimali zinaibiwa. Mheshimiwa Rais leo amejua, anapambana tuzirudishe, lakini mtu huyu hataki, anasema tunawaonea Wazungu, tunavunja mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza, jana umesema kama nimenukuu vizuri: "Hata kama mikataba imeingia miaka 50 iliyopita, lakini kama ni mikataba ya hovyota itaikataa." Amesema kipande chake cha Bunge kitatenda haki ikiwa ni pamoja na kubadilisha sheria hizo haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa uzalendo wako, nasi Wabunge wako tuko nyuma yako tunakuunga mkono, tunazubiri sheria hizo zije tuanze kuzibadilisha haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima Watanzania waelewe kwamba huyu mzee wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli anafanya nini? Jana kuna *statement* aliitoa mpaka nilitamani kutao machozi. Alisema: "Jamani na mimi nina damu, nami ni binadamu, lakini naumia kwa sababu yenu ninyi."

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Hivi Mheshimiwa Dkt. Magufuli angetaka kupokea mabilioni, angetaka kupokea mahati ya nyumba ya Marekani ili akae kimya tu, tungemfanya nini?

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mbona tunaibiwa siku zote hivi vitu? Ameonesha uzalendo wake. Mimi sitaki kuamini kwamba hakufuatwa kupewa hela, lakini amekataa chochote, anataka Watanzania wote wafaidi.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Usituchanganye na wewe.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Anainuka Mbunge anakutaja kupingana na jambo hili ambalo ni kwa faida yetu sisi zote. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumpongeze Mheshimiwa Rais, tumuunge mkono na tuendeleo kumwomba Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazofanya...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

## TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde naona kuna Mheshimiwa amesimama, ni Mheshimiwa Rhoda au!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Sophia Mwakagenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia eeh, samahani.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mbunge mwenzangu wa Viti Maalum anayeongea sasa hivi. Mimi ni Mbunge kwenye Bunge hili kwa mara ya kwanza, kwa lugha nyepesi ni *Form One*. Naamini yeye alikuwepo kwenye Bunge lililopita, najaribu kumweleza na kumkumbusha kwamba naye ni mmojawapo aliyepitisha mikataba hiyo. Nilikuwa nampa taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Si unabadilisha!

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia ili taarifa yako ikae vizuri, unaweza ukataja ni mkataba gani alioshiriki kuupitisha? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nifahamu nawe pia ni mwenyeji wa Bunge hili, mikataba yote iliyokuwepo mlihusika nyote mliokuwemo humu ndani.

**SPIKA:** Waheshimiwa mnapotezeana muda jambo ambalo siyo zuri. Mnafahamu kabisa kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano huwa halipitishi mikataba, isipokuwa mikataba ya Kimataifa ambayo imeingiwa kati ya Serikali na Serikali. Siyo Mkataba wa *Acacia* na mtu mwingine, hauingii Bungeni. Kwa hiyo, tusisingiziane. Endelea Mheshimiwa Munde.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Hajui huyo!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba unitunzie muda wangu. Naomba nimwambie dada yangu Mheshimiwa Sophia, mabadiliko hayana wakati. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kutuletea Rais jembe, Rais mpambania wanyonge, Rais mpambania maskini, Rais ambaye hana tamaa yake binafsi na familia yake. Leo hii Rais Magufuli angekuwa na tamaa yake na familia yake angekomba mahela yote akaenda kuweka Uswiss huko na yeye na tungeendelea kuibiwa hapa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie hawa watu ambao hawajui madini; siku ile Mheshimiwa Musukuma aliwaambia, mimi nimetoka Tabora Nzega, ukiona mashimo yaliyopo kule utalia. Kodi iliyolipwa kwa muda wote na *Resolute* haizidi shilingi bilioni 30. Wametuibia vibaya sana, wameondoka Halmashauri ya Nzega tunawadai *Development Levy* ambayo walitakiwa walipe shilingi bilioni 10 mpaka leo hawajalipa, Serikali inajua. Toka wameingia mpaka wanaondoka pale wamelipa shilingi bilioni mbili tu ya *levy* ya Halmashauri. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, kuna mtu mwingine anaongea tu, hajui chochote anachokiongea. Mimi nampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli na nimefunga na sala zangu zote namwombea kwa Mwenyezi Mungu. Maadui wengine wa Rais Magufuli tunao humu ndani, sijui wanataka nini hawa watu. Mtu anapambana kwa sababu yetu na watoto wetu, hivi vyama kuna vipindi tuweke itikadi pembeni tuangalie Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde, nakuongezea dakika kumi nyingine za meza. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniongeza dakika kumi. Kwa kweli kuna vitu ambavyo tunashangaza sana kwetu sisi. Nikitoka kuongea mambo ya makinikia ambayo ni mambo yamegusa Tanzania nzima; kule Tabora kuna Mwenyekiti wa UKAWA, jana amenipigia simu ameniambia Mheshimiwa Munde nimeenyoocha mikono kwa Mheshimiwa Dkt. Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutaka kuwadhibitishia hilo, nikimaliza Bunge nitafanya mkutano wa hadhara Tabora nitamkabidhi kadi ya CCM ili wajue kwamba Watanzania wamemkubali Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa asilimia 100. Nilisema humu Bungeni kwamba wataelewa tu na wameelewa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba kazi tuliyonayo mbele yetu ni kui-*support* Serikali yetu ya Awamu ya Tano, Inafanya kazi vizuri sana. Nimekaa Bungeni, nimepita bajeti saba za Bunge, sijawahi kuona bajeti kama hii.

Mheshimiwa Spika, tuisahau kwamba Mheshimiwa Dkt. Magufuli ndiyo bajeti yake ya pili. Ana miaka miwili tu. Hata sisi Majimboni tuna mambo mengi hatujayafanya ya kwetu peke yetu. Leo kuna mtu anafanya kana kwamba Mheshimiwa Rais Magufuli leo ana mwaka wa kumi. Sijui kwa

sababu amefanya mambo mengi, wanajisahau kwamba huyu mtu ameanza juzi tu. Sijui wamechanganyikiwa! Mimi hata sielewi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nawaonea huruma na kuwapa pole na kuwaambia bado nafasi tunazo mpaka 18 Juni tunafunga kupokea watu wa kutoka Upinzani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, bajeti imekuwa nzuri, nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Mpango, lakini niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba bajeti haiwezi kumaliza matatizo ya nchi nzima, hii bajeti ya pili tu. Tuendeleo kuipongeza bajeti hii, watufanyie kazi kama walivyotuahidi kwa kasi yao ya Awamu ya Tano, lakini kila mwaka tutaongea watatukubalia kama walivyotukubalia safari hii.

Mheshimiwa Spika, tumeongea *motor vehicle* wamekubali, tumeongea sana kuhusu kurasimisha Wamachinga na Mama Lishe. Leo hii wamekuja kutuambia kwamba wanarasimisha sasa. Watajulikana sasa. Wamachinga na Mama Lishe watakuwa wanajulikana na sekta rasmi.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Tabora tuliongea sana kuhusu reli, leo tunaenda kwenye *standard gauge*. Naomba niongelee sasa kuhusu suala zima la viwanda. Mheshimiwa Dkt. Magufuli wakati anajinadi, akiomba kura alisema anataka Tanzania ya viwanda. Bajeti hii imetuonesha mwelekeo mzuri wa Tanzania ya viwanda. Hivi jamani tunataka nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii wamefuta *capital goods*, wameifuta kabisa imebakia *zero*, wamefuta *VAT* kwenye vifaa vya uwekezaji, wamepunguza kodi ya mboga mboga na matunda, wameondoa kodi kwa mtu anatayekwenda kuuza mjini tani moja ya mazao na ndiyo wengi mama zetu hawa, ndiyo wengi baba zetu hawa; anajilimia ekari zake kumi anaenda kuuza mjini kila siku kidogo kidogo. Walikuwa

wanapambana na watu wa kuwadai kodi, sasa hivi hakuna. Jamani Mheshimiwa Rais afanye nini? Serikali ifanye nini? Hii ni bajeti yake ya pili tu, wamejitahidi sana jamani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde. Tunakushukuru sana. *(Makofi/Vigelele)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi/Vigelele)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa uchambuzi wako mzuri.

Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Peter Lijualikali ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Labda nianze kutoa tu masuala machache ya utangulizi na hii ni kwa faida tu ya wachumi na wale ambao siyo wachumi wanaweza kujifunza. Jambo la kwanza ambalo ni *neutral*, tunaposema Serikali inatekeleza *D by D*, jambo muhimu siyo nani anakusanya fedha hizi, ni kwamba fedha hizi zikishakusanywa nani anazitumia? Nani anafanya maamuzi ya kuzitumia? Hilo ndilo jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia unapoamua kwamba unaongeza Sh.40/= kwa lita, sasa wachumi hata tungekusanya Maprofesa wa Uchumi humu kwenye ukumbi huu, wote wanaweza wakabishana; kuna wengine watasema labda bei zitaongezeka, kuna wengine watakwambia bei hazitaongezeka. Inategemea wachumi hawa walisomea Vyuo vipi na waliwaelewa vipi Walimu wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmoja aliyefundishwa vizuri atakwambia kulingana na taarifa zilizowasilishwa Bungeni, Kitabu cha Mpango wa Maendeleo 2017/2018, ukikiangalia na taarifa iliyotolewa na *World Bank* iliyoko kwenye kitabu kile, kinakuonesha kwamba bei ya petroli mwaka 2014 kwa ujazo wa lita 1,000 ilipungua kutoka dola 905 kwa wastani mwaka 2014 mpaka dola 462. Kwa hiyo, atakwambia *trend* ya bei ya mafuta katika Soko la Dunia imekuwa ikipungua kutoka dola 905 kwa wastani mpaka dola 462.

Mheshimiwa Spika, mwingine atakuambia kuhusu *diesel*. Utauliza, je, *diesel*? Atakujibu kulingana na takwimu ambazo zimetolewa na *World Bank* kwamba nayo ilipungua bei kutoka dola 809 mwaka 2014 mpaka dola 380; na mwingine atakwambia kuhusu mafuta ya taa nayo pia yalipungua kutoka dola 407 mpaka dola 406 kwa ujazo. Kwa hiyo, atakwambia kwa kuwa *trend* inaonesha bei hizi zimekuwa zikipungua, hivyo, ongezeko lolote litalotokea katika masuala mengine ita-*offset* kile kinachotokea kwa sababu bei katika Soko la Dunia mwenendo ni kupungua sana kuliko chochote kile unachofanya kuongeza. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Wafundishe, wafundishe!

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Kwa hiyo, itategemea huyo mtu alisomea wapi na anaelewa vipi kutafsiri hizi takwimu. Ukikutana na mwanafunzi wangu niliyemfundisha darasani ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Fedha, yeye atakwambia alipofundishwa na Mwalimu mmoja aliyebobea kwenye uchumi, alimwambia unapoangalia haya masuala ya bei kuongezeka na kupungua, kuna kitu kinaitwa *surplus demand* na kuna kitu kingine kinaitwa *consumer surplus* na *producer surplus*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, atakwambia siku zote unapooongeza bei *most likely*, *consumer surplus* inaweza

ikabadilika, lakini katika hili inaonekana ambaye atalazimika kupunguza bei ni yule *consumer surplus* kwa sababu kuna ushindani katika soko hili na kama mtu hatataka kushindana, ataondoka. Sasa huu ni uchumi mwepesi ambao nisingependa kuendelea na nawakaribisha wengine wasome vitabu vya *Economics Made Simple*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme haraka haraka kabla sijasahau kwamba bajeti hii ni nzuri na naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa kuzingatia bajeti nyingi ambazo nimeziona nikiwa katika Bunge hili, lakini pia na bajeti zinazotokea maeneo mengine; na ukiangalia malengo yetu manne ni kwamba bajeti hii itatusaidia kuweza kuyafikia. Malengo yetu siyo mengi, ni machache. Tunasema tunataka kujenga uchumi wa viwanda, tunasema bajeti hii itatusaidia; tunasema tunataka kujenga uchumi wezeshi, bajeti itatusaidia; tunasema tunataka bajeti hii itusaidie kuunganisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu, bajeti hii itatusaidia.

Mheshimiwa Spika, kubwa tunasema ili bajeti hii iweze kutekelezeka, tunahitaji watu wenye uwezo wa kuisimamia vizuri na tunaona sasa tunaye Rais ambaye anaonesha yuko tayari kusimamia na ameanza na makinikia. Kwa hiyo, tusiwe na wasi wasi na jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya kuzingatia ili tuweze kufanikiwa vizuri. Siwezi kuyataja yote, nitataja machache. La kwanza ambalo lazima tulizingatie, chakula ni uchumi, chakula ni ushindani. Lazima tuongeze nguvu zetu za kuhakikisha tunasimamia vizuri Sekta ya chakula. Ukiangalia takwimu tulizonazo, taarifa iliyotolewa na Benki Kuu inaonesha mwaka 2014 wastani katika Wakala wa Hifadhi ya Chakula, zilipanda mpaka wastani wa tani 455,000. Ilipofika mwaka 2017 zimepungua mpaka wastani wa tani 86,000 kwa mwezi, Januari, 2017 zilipungua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutoka tani 455,000 wastani wa hifadhi ya chakula ndani ya ghala kwenda

mpaka tani 86,000 lazima zote tukubali kwamba kuna tatizo. Kwa hiyo, lazima tuelekeze nguvu zetu za kuongeza wastani, kwa sababu tunapozungumza uhaba wa chakula kwenye nchi au chakula kilicho kwenye nchi tunaangalia chakula kilichoko kwenye ghala la Taifa na maghala mengine ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unapoona kwenye ghala la Taifa inapungua kutoka wastani wa 455,000 kwa mwezi hadi 86,000 kwa mwezi, maana yake kuna tatizo ambalo hatuwezi kulifumbia macho, lazima tulishughulikie. Lengo letu kwa kuwa sitaki kusema mengi, tulenge kuongeza wastani wa chakula kwenye ghala letu la Taifa kutoka tani 86 kwa mwezi hadi kuelekea tani 500,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ukisoma kitabu cha Mpango wa Maendeleo kimeeleza vizuri kwamba chakula ni muhimu na lazima tujielekeze katika kuongeza hiyo hifadhi. Ili tuweze kufanya hivyo yapo mambo mengi ya kufanya. Moja, ni lazima tutoe uhuru kwa wakulima wetu kuwa na uhuru wa kulima na kuamua wapi wauze mazao yao bila kuwekewa masharti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *South Sudan* sasa ni mwanachama wa Afrika Mashariki, wana soko kubwa la kupenda kununua mazao yetu, lakini mara nyingi tumekuwa tukizuia wakulima wetu kwenda kuuza mazao popote wanapotaka wakati inatolewa bei kubwa. Kwa kufanya hivyo, tunawaondolea uhuru wa kuuza popote na tunawazuia kwenda kwenye mabenki kukopa ili kuongeza uzalishaji. Ndiyo maana nasema, lazima tuongeze uhuru kwa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia lazima tuachane na kutoa vibali vya upendeleo. Kule Mtukula ukienda unakuta kuna baadhi ya watu, wengine tunao Bungeni humu, sitapenda kuwasema, wengine wanapata vibali vya kupeleka mazao nje cha nchi, wengine hawapewi vibali.

Mheshimiwa Spika, nilijaribu kufuatilia hili, nikagundua inahusisha Waheshimiwa wazito tu. Ni uchafu gani huu? Sasa sitawataja majina yao humu, lakini niwaombe tu waache kwa sababu wale wakulima wadogo wadogo na wao wanayo haki ya kuuza mazao yao kokote kule. Kwa hiyo, jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa haraka haraka kuzungumzia hoja nyingine ambayo inahusu suala la kuondoa ugonjwa wa mnyauko wa migomba. Kule Kagera tunao ugonjwa unaosumbua sana, tumejitahidi kupambana nao lakini wataalam wetu wa MARUKU wakubali kwamba wameshindwa. Serikali iongeze fedha ili tuweze kuondoa ugonjwa huu kabisa kuliko kudhibiti tatizo la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba ukiangalia taarifa ya hali halisi ya uchumi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kamala muda wako umekwisha.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama muda umekwisha, mengine nitachangia kwa maandishi, lakini naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Ahmed Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Lijualikali na Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatia.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba hii iliyopo mbele yetu. Leo nilikuwa sitaki kuchangia habari za haya mambo ya *Road License* lakini imenibidi nichangie kidogo tu ili tuelewane vizuri tu siyo labda kwa kushindana au nini ila kueleweshana tu.

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, nafikiri kama Waziri wa Fedha angefuata yale mawazo yetu ambayo tulikuwa tunampa siku tano za nyuma basi ina maana kwamba angepandisha Sh.140/= kwenye bei ya mafuta, asingepandisha Sh.40/=. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu Wabunge wengi tuliokuwa tunachangia humu, mimi sikupata nafasi lakini wengi walikuwa wanasema kwamba, Sh.50/= weka kwenye maji, Sh.50/= weka *REA* na *Road License* weka kwenye mafuta. Sasa leo kwa busara zake tu akaamua kuweka Sh.40/= tu peke yake ile Sh.100 akaiacha lakini bado na hii nayo tunamgeuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ndugu yangu hapa Mheshimiwa Kamala yeye ni Mwalimu, ameeleza vizuri sana na mimi sasa ni Mwalimu wa huko mtaani nitawaeleza kidogo. Kwa hesabu tu nyepesi, niwape hesabu nyepesi tu, *Road License* gari lenye *CC2500* ilikuwa inalipiwa Sh.200,000/= kwa mwaka. Sasa tuchukue mfano tu mwenye gari hiyo, maana yake tuangalie kwanza hawa watu wa kawaida, kila siku akijaza lita 10 ya mafuta kwa mwezi atajaza lita 300. Akijaza lita 300 ukiweka mara ile Sh.40/= kwa mwezi analipa Sh.12,000/=, ukiweka ile Sh.12,000/= kwa mwaka analipa Sh.144,000/= . Kwa hiyo, hata hiyo Sh.200,000/= bado hajafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwapeni mfano mmoja, tunaposema kwamba usafiri utapanda sijui kilimo kitapanda, Mungu ananisaidia mimi ni mkulima na msafirishaji, lazima ku-*declare interest*, bei ya *EWURA* ya mwezi huu tuliomaliza nao ilishusha dizeli kwa Sh.81/= na petroli kwa Sh.30/=, kwa



mwezi huu wa Tano tuliomaliza. Mwezi huu bei iliyotangazwa juzi, dizeli imepanda Sh.43/= na petroli imepanda Sh.25/= . Kwa hiyo, hata ukiweka na hii Sh.40/= hatujafika bei ya mwezi wa Nne na bado hizo nauli zipo pale pale. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna mtu jana alizungumza, nataka nizungumze kweli, bei ya mabasi iliyotolewa na *SUMATRA* imetolewa miaka mitano iliyopita lakini mpaka leo hakuna basi limefikisha ile bei waliyopangiwa na *SUMATRA*, hakuna. Dar es Salaam – Arusha ni Sh.33,000/= lakini watu wanaenda kwa Sh.25,000/=; Dodoma – Dar es Salaam ni Sh.24,000/= watu wanaenda kwa Sh.17,000/= mpaka Sh.20,000/= . (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hii kodi, hata Wabunge wengine wapo upande wa CCM na wengine wapo upande mwingine, walikuwa wanasema iingie kwenye maji, tumetoa *Road License* na gharama za *Road License* zilikuwemo kwa wasafirishaji hata msingepandisha mafuta walikuwa wanalipa *Road License*, kwa hiyo gharama ilikuwa ipo pale pale tu. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Tena kubwa zaidi.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, gharama hii ya *Road License* ibaki kama *Road License* kwenye mipango yake ya Serikali. Kama kuna mpango mwingine wa kupandisha maji basi tuweke tena Sh.50/= nyingine. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Yes.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, tusiingize hii huko kwamba tuitoe kwenye mipango yake ya Serikali, sijui ifanye hiki na kile kwa sababu hata usipopandisha mafuta, ukiacha *Road License* si ni pesa msafirishaji ataingiza tu ile.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze tu...

**SPIKA:** Mnasikia uzoefu huo? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumze tu ili watu walielewe hili suala vizuri, hii ni nchi yetu. Kule China watu walikuwa wanavaa *chunlai* siyo kwamba walikuwa wanapenda, leo wanavaa bluu watu wote kesho kijani, walikuwa wanafunga mikanda ili wafike mahali wanapohitaji. Kwa hiyo, twendeni tufunge mikanda tufike mahali tunapotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine huyu Ndugu yangu Mheshimiwa Mpango leo nampa shikamoo. Mara ya kwanza humu tulikuwa tunakujadilijadili, tukaona huyu jamaa mpole sana kwa sauti lakini mbona kama haelewielewi, hataki ushauri.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini wewe.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Hataki ushauri, tulikuwa tunashangaa kwa nini hataki ushauri lakini sasa hivi...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi kwenye Bunge hili tumegundua kwamba katika watu wanaopenda ushauri Mheshimiwa Mpango naye mmojawapo. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Yes.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwa nini nimempa shikamoo. Ukiangalia taarifa ukurasa wa 54...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mara hizi taarifa zimekuwa zikitumika vibaya tuseme tu ule ukweli.

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**SPIKA:** Hebu kwa mapenzi kabisa wote naomba tumsikilize Waitara kama kweli hiyo taarifa ni taarifa. *(Kicheko)*

## T A A R I F A

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ni kweli kwamba ni muhimu ukasikiliza kwanza hoja ya mtu kabla ya kumhukumu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shabiby ni rafiki yetu, tunajua shughuli anayoifanya lakini taarifa yangu ni kwamba wakati anaeleza na uzoefu aliotaja hakueleza anafanya shughuli gani, alikuwa anazungumzia *areas of interest* zake, hakueleza na ndio hoja yangu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hiyo ndiyo hoja yangu kwamba haku-*declare interest* shughuli ambazo anafanya, ndiyo taarifa ninayotaka kumpa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby ameeleza kwamba yeye ni mkulima na yeye ni msafirishaji. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**SPIKA:** Tuendeleo Mheshimiwa, ndiyo maana nikasema taarifa nyingi yaani kwa kweli ni *uncalled for*, zinatuharibia tu mijadala kwa kweli. Ningeomba muwe mnavumilia zaidi mpaka pale mahali ambapo kwa kweli

kuna ulazima wa kumkatisha mtu ili dakika zetu ziende vizuri, kama hivi nataka Mheshimiwa Lijualikali apate nafasi sasa mnapoteza muda, Mheshimiwa Shabiby. (*Makofi*)

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Taarifa yake naipokea kwa sababu ni rafiki yangu huyu najua ananichangamsha tu, hakuna hata matatizo lakini najua nilishamwambia kwamba ni mkulima na mfugaji, ni rafiki yangu Waitara hakuna matatizo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nilikuwa nasema Mheshimiwa Mpango shikamoo, amerudi pale pale kwenye vile viwanda vya Mwalimu Nyerere. Hii ni kwa sababu ukiangalia ukurasa wa 54, kipengele cha tatu, amezungumzia kupunguza ushuru wa vile viwanda vitakavyoletwa kwa ajili ya kuunganisha matrekta, boti na magari. Ametoa ushuru huu wa *Corporate Income Tax* kutoka asilimia 30 mpaka 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nitoe ushauri, mpaka leo hakuna mtu aliyefikia rekodi ya mzee wetu Mwalimu Nyerere. Wakati ameanzisha kile Kiwanda cha *TAMCO* pale Kibaha cha kuunganisha magari ya *Scania*, pamoja na kuwaambia wawekezaji waje lakini aliwapa masharti ya kununua bidhaa zinazotengenezwa Tanzania ili kuunganisha yale magari.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, rejeta zote zilizokuwa zinatumika kwenye magari yote yaliyokuwa yanaunganishwa Tanzania zilikuwa zinatoka kwenye Kiwanda cha Serikali kinaitwa *Afro Cooling*, betri zote zilikuwa zinatoka kwenye Kiwanda cha Serikali kinaitwa *YUWASA*, *wiring* zote zilizokuwa zinafanyika kwenye magari zilikuwa zinatoka *East African Cable*, matairi yote yalikuwa yanatoka *General Tyre*, *spring* zote zilikuwa zinatoka *Tasia Spring* na *muffler* zote zilikuwa zinatoka Tanzania kwenye kiwanda cha Serikali. Sasa hapo ndiyo unaongeza ajira kwa sababu bila kufufua viwanda kama *General Tyre*, *Afro Cooling* na viwanda vyote nilivyovitaja na vingine viko vingi tu bado kuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ulikuwa ukiangalia ile gari ilikuwa inatengenezwa na Watanzania kwa asilimia zaidi ya 18. Kwa hiyo, ile gari ili ifanyiwe *assemble* hapa hivi viwanda vingine vyote vilikuwa vinafanya kazi na vinatoa ajira nyingi sana kwa Watanzania. Kwa hiyo, naomba kwenye huu ukurasa wa 54 hapa basi aweke hayo masharti ya kwamba mwekezaji yeyote atakayekuja kuunganisha magari hapa Tanzania basi lazima atumie bidhaa za Tanzania. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajitahidi juu chini ahakikishe hivi viwanda vinafufuka kama *General Tyre, Afro Cooling...* (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby malizia sasa.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri afufue hivi viwanda ili hii dhana yake iende vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Peter Lijualikali atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Zaynabu Vulu ajiandae.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nataka nizungumzie ushuru wa mazao ambao Mheshimiwa Waziri ametoa kwa mazao ya kilimo. Alisema kwa hawa wakulima ambao wanasafirisha mizigo yao kwa maana ya mazao kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine, kama ni mzigo usiozidi tani moja wasitoe ushuru.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana mimi nina Halmashauri mbili, ya Ifakara na Kilombero. Wananchi wangu hasa wa Ifakara wengi wanalima Halmashauri ya Kilombero wanakuja Ifakara hapa katikati huwa kuna *barrier* ambapo huwa wanawekwa pale Askari Polisi wenye bunduki kwa ajili ya ushuru. Kama Halmashauri ya Kilombero tulisema mkulima kutoka Ifakara anayelima Kilombero, akirudi na magunia yasiyozidi 20 anapita bure.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hili agizo kwamba tani moja ndiyo ipite, tani moja ni wastani wa magunia 10 maana yake ni kwamba tayari tumesha-*confuse* utaratibu wetu kule Ifakara. Maana yake tunawaambia wananchi wa Ifakara kama tulikuwa tunasema wapite na magunia 20 sasa wapite na magunia 10 tu kwa mujibu wa sheria hii, tayari ni *confusion*. Maana yake ni kwamba hapa sasa hatusadii. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Peter hayo magunia mliyoamua huko ni ya mpunga au mchele?

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mpunga.

**SPIKA:** Sasa mpunga gunia 20 ni tani ngapi ya mchele? Maana nadhani Waziri anazungumzia mchele hazungumzii mpunga.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, mimi nasema tani na ningependa unisikilize mpaka mwisho kwa sababu katika hicho kizuizi wanapokaa askari hapo, mkulima hata kama ana gunia tano za mpunga, hawezi kuchukua *fuso* au usafiri mkubwa kwa ajili ya kubeba hizi gunia tano, maana yake lazima wakulima watachanga, watakodi usafiri mkubwa waweke kwenye hilo gari waweze kuja Ifakara. Haiwezekani mkulima atoke na mzigo Idoko akiwa na gunia 10 atembe nazo mpaka Ifakara, hawezi kukodi maana yake lazima wachange wawe wengi. Wakifika pale wanaambiwa huu mzigo ni wa mtu mmoja wakati wale ni wakulima wengi wamechanga gari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili Mheshimiwa Waziri aliangalie, aende kule Ifakara aweke sawa, haiwezekani mkulima mmoja akodi gari wakati ana magunia matano au sita maana yake lazima wakulima wengi wachange kwenye hili gari moja ili wawe na mzigo mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia niseme nina shida ya barabara pale, barabara yangu ya kutoka Kidatu mpaka Ifakara ni

mbovu kwa miaka mingi. Sasa Mheshimiwa Waziri nimeambiwa imetengwa shilingi milioni 300 kwa ajili ya fidia, maana barabara hiyo sasa hivi ndiyo inataka kujengwa, hivi kutoka Kidatu mpaka Ifakara pale kuna nyumba ngapi, ni nyingi sana. Hii fidia ya shilingi milioni 300 ni takribani nyumba mbili tu hizi, hawa wengine fidia yao iko wapi? Kwa hiyo, naiomba Serikali kama ina ya dhati ya kujenga barabara hii, fidia iongezwe siyo hii hela ndogo ambayo imewekwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo lingine, hotuba ya Mheshimiwa Msigwa, hii hotuba ya akili ndogo nafikiri itaishi milele. Kwa sababu mambo yanayotokea leo katika nchi hii yameshasemwa miaka mingi sana na hata Msigwa alisema akili ndogo haiwezi kuongoza akili kubwa. Leo ambacho kinatokea hapa ni kwamba akili ndogo ile ambayo ilikuwa inapiga makofi wakati sheria mbovu zinatungwa hapa Bungeni, ile akili ndogo wakati akina Zitto wanasema hawa Mawaziri wanakwenda kusaini mikataba nje, Waziri anapewa ndege aende nje akaingie mkataba mlikuwa mnapiga kelele nyie mnasema kwamba huyu Zitto mwongo, hafai na ametumwa, Zitto akafukuzwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati haya yanatokea huyu Rais wetu alikuwa pale amekaa. Wakati Mnyika anaongea haya maneno kwamba nchi hii inaibiwa, nchi hii inafilisiwa, mlikuwa mnapiga makofi nyie, akili ndogo hiyo inapiga makofi. Akili kubwa akina Msigwa, Zitto na Mnyika wakati wanasema haya maneno walionekana wabaya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali, kwa hakika kabisa najua kuna ujumbe unataka kufikisha lakini kwa mfano unaotoa ni mfano unaodhalilisha Wabunge wengine. Kutufanya sisi wengine wote akili ndogo na hao unaowataja akili kubwa na hujaleta vyeti vyetu vya *form four* vya hao na sisi uone kwa Mama Ndalichako kule kama kweli wana akili kubwa kuliko sisi. Nadhani ungetafuta lugha fulani ya kufikisha ujumbe wako, bado ujumbe wako una maana lakini kwa mfano huo unaoutoa nadhani siyo sawasawa sana.

Endelea kuchangia bila kutumia lugha za kuudhi na kudhalilisha watu wengine wenye familia zao, endelea Mheshimiwa Lijualikali. *(Makofi)*

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, sawa nimekuelewa. Mimi ninachokisema ni kwamba wakati haya yanasemwa, wakati akina Lissu, Zitto na Mnyika wanasema mlikuwa mnawazomea, mnasema hawafai. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali, tuelewane hivi, Kiti kikishakupa mwongozo unapaswa kuzingatia. Sijui kwenu huku ni Mbunge yupi wa muda mrefu zaidi ya Mbowe, sikumbuki, nani?

**WABUNGE FULANI:** Grace Kiwelu.

**SPIKA:** Grace Kiwelu ni wa 2000?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Ndiyo Grace Kiwelu anaweza akakumbuka pia, Bunge hili wakati wa kipindi cha bajeti kama hiki miaka yote ya 2000, 2002 na kuendelea hakuna bajeti ilikuwa inapita kwa ugumu kama bajeti ya nishati na madini. Nyeie wote ni mashahidi. Bunge hili halijawahi kama Bunge kuunga mkono ufisadi, tusipotoshe. Tusifanye kama jambo hili ni la fulani na fulani. Wabunge humu wanachangia kwa namna mbalimbali, kuna wanaochangia kwa maandishi, wewe unajua wote waliandika nini? Kuna wanaochangia kwenye Kamati lakini humu hawakupata nafasi, kwa hiyo, tusidharauliane. Kuna kamtindo alianza huyu Mbunge wa Arumeru, Mheshimiwa Nassari, fulani ana akili na wengine hawana akili, akili ndogo sijui akili kubwa, hivi huwa mnakosa hoja huko za Majimboni? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Niwahakikishie kwa Ubunge wa mwaka jana ambao wewe umeingia, mwaka jana peke yake asilimia 70 haikurudi hapa. Sasa unaowahutubia wako wapi? Kama



hawa wasingekosea wewe ungekuja? Walikosea, wakaadhibiwa huko yameisha, wewe tumia nafasi ya leo hali ilivyo una shauri nini badala ya lawama na vitu ambavyo, Mheshimiwa Lijualikali endelea. (Makofi)

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu unakuja hivi, kwa kuwa tumeshasema na kama Taifa tumeona kwamba *Acacia* ni wezi na kwa kuwa na Rais amesema hawa watu wanatakiwa wafanyiwe kazi, kwanza lazima kinga ya Rais itolewe, tufanye *amendment* hapa, Marais wa nchi hii wasiwe na kinga ya kutokushtakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu hainiingii akilini wakati leo unamwambia Karamagi, unamwambia mzee wangu Chenge kwamba wahojiwe Marais waliopita wanaachwa. Haiwezekani Chenge alifanya makosa Rais asijue, haiwezekani *Cabinet* ilikuwa haijui. Tufanye *amendment* ya sheria Marais wote na hii vita siyo iwe ni *one man army*, isiwe vita ya jeshi la mtu mmoja ndiyo lipigane iwe vita ya Taifa zima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama ni kuomba radhi, CCM lazima muombe radhi kwa hasara ambayo mmeleta kwenye Taifa hili. Leo hapa mnajifanya mnapiga makofi, mnashangilia wakati nyie mmeua watu, watu wamekosa madawa kwa sababu ya uamuzi wenu wa hovyoo. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu, *amendment* ije, Rais aombe radhi, Bunge liombe radhi na CCM muombe radhi kwa maamuzi mliyoyafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Nakuacha tu lipite hilo maana unapowaambia watu hapa wameua watu sijui nani kua nani. Kuna wakati mkianza kuongea mnakuwa kidogo *unguided, unruly*, bado wageni, ni vizuri kukua katika mambo haya, kujilinda katika kuhakikisha unapozungumza unazungumza vitu ambavyo huwezi kubanwa kirahisi sana na kwa wepesi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliiongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Hata hivyo, mkumbuke pia hao viongozi mnaotaka sijui tubadilishe wakamatwe mna wawili huko ndani Mawaziri Wakuu Wastaafu, watakapobanwa msianze kupiga kelele hapa. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliiongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema hivi, CCM ni ileile, Mawaziri ni walewale, Wabunge ni walewale, Mheshimiwa Magufuli ni yuleyule na wananchi ni walewale. Sasa nasema hivi, wananchi wamejipanga vizuri kwa ajili ya kumuunga mkono Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Kwa maana hiyo, nimeimba kwa kusema, ningesema CCM ni ileile, kwa hiyo, tumejipanga kuhakikisha 2020 hakitoki kitu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono bajeti hii na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Dokta Mpango na Naibu wake pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha kwa bajeti yao nzuri. Naomba niunge mkono mapendekezo yote ya Kamati ya Bajeti ya tozo ya Sh.40/=. Mapendekezo yao ni mazuri, nayaunga mkono kwa asilimia 100 kwa sababu yatakwenda kumwondolea mwanamke adha ya ndoo kichwani. Kwa hiyo, bajeti hii ni nzuri na mapendekezo ya Kamati ni mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa tozo hiyo ya Sh.40 pesa zile ziweze kupelekwa kwa ajili ya maji vijijini. Wananchi wanapata shida sana ya maji kule vijijini, wanawake hawawezi kufanya shughuli za maendeleo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Kwa sababu ya shida ya maji, lakini pesa hizo zikigawanywa zikapelekwa kule kwenye maji kwa kweli...

**SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, kuna Mbunge amesimama.

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa mzungumzaji hapa. Wakati haupo Waziri wa Nchi, Sera aliwahi kusema hapa akiwaambia watu wa Upinzani kwamba anapotajwa Mheshimiwa Rais lazima useme Mheshimiwa Rais, tena Mtukufu. Sasa mzungumzaji amesema tu Mheshimiwa John Pombe Magufuli, John Pombe Magufuli ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, hii isiwe kwa Wapinzani tu, itajwe na watu wa CCM kwamba Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli, twende sawa. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa vile analitambua hilo na mimi nilisema Mheshimiwa Magufuli ni yuleyule kwa sababu hata ule wimbo wa CCM unasema Magufuli ni yuleyule. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke endelea, wanamfahamu vizuri na wasiomfahamu watamfahamu taratibu.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naendelea, wananifahamu kwa sababu niliwahi kuwaambia Wapinzani Kigoma hawatarudi na tuliwafuta wote wakabakia wawili. Kwa hiyo, wale waliosalia nafikiri wanajua kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga asilimia 69 kwa ajili ya zahanati na vituo vya afya ili pesa

hizo ziweze kwenda kumaliza miradi ile ya vile vituo vya afya na zahanati ambavyo wananchi kwa nguvu zao walianza kujenga. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa kutenga pesa hizo shilingi bilioni 69 kwa ajili ya kwenda kusaidia miradi hiyo. Pesa hizo zikipelekwa kule wanawake watanufaika kwa sababu hawatapata shida sana kwenda kuvifuata vituo vya afya au zahanati maeneo ya mbali kwenda kutibiwa. Kwa maana hiyo, vifo vya wanawake na watoto vitapungua kwa sababu huduma zitakwenda kupatikana karibu. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali yangu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mkoa wa Kigoma ulikuwa kati ya mikoa maskini na ilikuwa ni kwa sababu ya miundombinu ambayo haikuwa mizuri lakini naishukuru sana Serikali kwa sababu imeendelea kuutupia macho Mkoa wa Kigoma. Naomba pesa zilizotengwa kwa ajili ya barabara ya kutoka Nyakanazi kwenda Kanyonza, kutoka Kidahwe kwenda Kasulu, zipelekwe kwa ajili ya kwenda kumaliza barabara ile na ikibidi barabara ile yote iweze kumalizika kwa sababu ya kuunganishwa na Mikoa mingine ya Kagera na Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Kigoma ni wachapakazi sana, kwa hiyo miundombinu ikiwa mizuri kwa sababu ni wakulima wataweza kusafirisha vyakula vyao kwenda sokoni na tutawahamasisha wawekezaji waje kujenga viwanda ili wananchi wanapokuwa wanalima mazao yao waweze kupeleka kwenye viwanda ambavyo vitakuwa viko jirani na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, sisi tumejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji, tuna Mto Malagarasi, Mto Lwiche na Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kumaliza miundombinu ile ili wawekezaji waweze kuja kufanya kilimo cha umwagiliaji tuweze kuwa na viwanda vya sukari na kukamua mawese. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kuutupia macho Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya kuweka miundombinu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa kuendelea kuuona Mkoa wa Kigoma, ndege zile za *bombardier* zinaenda Kigoma. Naomba sasa, reli ile inayojengwa ya *standard gauge* ianzie Dar es Salaam mpaka Kigoma, nyote mnajua reli ile ilikuwa inaanzia Kigoma kwenda Dar es Salaam, Dar es Salaam kwenda Kigoma, ndiyo maana inaitwa mwisho wa reli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba inapokuwa inafanywa mipango kuelekea Mwanza, chondechonde, tunaomba reli ile ije Kigoma. Kigoma mnaifahamu, tumepakana na *DRC* na Burundi, kwa hiyo, mkituwekea reli hiyo ya *standard gauge* hatutapata shida sana, tutaweza kuendelea kufanya biashara kwa kushirikiana na nchi hizo jirani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali na naipongeza kwa mipango ya umeme. Kwa hiyo, naomba pesa zipelekwe kwa ajili ya umeme wa *REA* awamu ya tatu ili pesa zikipatikana ziweze kuja Kigoma kwa ajili ya kuweka umeme katika vijiji vyetu vinavyozunguka miji yetu katika Miji ya Kibondo, Kakonko, Kasulu, Uvinza, Buhigwe na maeneo mengine yote. Kwa hiyo, naomba *REA* iongezewe pesa kwa sababu baadhi ya vijiji havijaweza kupata umeme, pesa zikipatikana umeme utaweza kupatikana katika vijiji vyote vinavyozunguka miji yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko ya mawakala ambao wamefanya kazi ya kusambaza mbolea kwa wananchi. Nafahamu wapo mawakala waliofanya kazi kwa uaminifu na uadilifu mkubwa, naomba Serikali ijipange, wale ambao ni waaminifu walipwe pesa yao. Ni muda mrefu sasa wamesubiri, nyumba zao zimeuzwa, wengine wamekufa kwa sababu walikopa kwenye mabenki lakini wameshindwa kurejesha kwa sababu hawajapata pesa. Kwa hiyo, naomba ufanyike utaratibu wa kuweza kuwalipa ili waweze kurejesha madeni yao benki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho, *SACCOs* na *SACAs*, tumekuwa tukiwahamasisha wananchi kuanzisha *SACCOs*

na SACAs lakini upo upungufu mkubwa wa watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Wafanyakazi hao wa ushirika hawatoshi na vile vikundi vilivyoanzishwa vijijini kwa maana ya SACCOs na SACAs wanahitaji elimu, hawajui jinsi ya kukopa, hawajui jinsi ya kurejesha na hawajui ili wakopesheke ni lazima wakaguliwe na vyombo vinavyofanya kazi ya ukaguzi wa pesa ili kubaini kama hawa watu tukiwapa pesa wataweza kuirejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ilianganalie eneo hili, watumishi wa ushirika hawapo kule vijijini na hata hao wachache waliopo hawana vitendea kazi. Kwa hiyo, tunaomba hawa watumishi wa ushirika, kwanza waajiriwe ili wawe wengi, lakini wapewe vitendea kazi ili waweze kwenda vijijini kuzifundisha SACCOs na SACAs zetu ziweze kuelewa vizuri, hatimaye tutakapopata pesa hata hizi asilimia 10 kwa maana ya wanawake na vijana zinapopelekwa kwenye vikundi wajue ni jinsi gani watatumia kwa sababu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Genzabuke, malizia.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Genzabuke. Nilishamtaja Mheshimiwa Zaynabu Vulu atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Saada Mkuya ajiandae.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe miongoni mwa wale wanaochangia hotuba hii ya bajeti ya awamu ya pili katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli, bajeti ambayo imeonesha dira na msisimko wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi anazozifanya kwa Watanzania kwa maendeleo ambayo anayaona yakiweza kufanikiwa basi Watanzania watakuwa wamegomboka na wamepiga hatua kuondokana na umaskini. Mheshimiwa Rais amelenga kuhakikisha pale palipokuwa na mianya ya mchwa anatia dawa wale mchwa wote waweze kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi sote ni mashahidi na sio tu humu ndani tu tunaompongeza Mheshimiwa Rais, Dokta John Pombe Magufuli hata Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi amesema hadharani kazi anayoifanya Rais Magufuli ni kazi ambayo imefanywa na wao kwa miaka 30 iliyopita. Kwa hiyo, sisi sote tuna kila sababu ya kuunga mkono juhudi zake.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze na wewe, jana umetuwakilisha vizuri sana, sisi tuko na wewe bega kwa bega, mguu kwa mguu, mbele kwa mbele hadi tujue mwisho wa wale ambao wanataka kuharibu na kudhulumu uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake wametuletea bajeti. Bajeti hii sisi tunaifurahia, wengine wanafurahia ndani ya mioyo lakini usoni hawataki kusema ukweli na huo ni ugonjwa. Kama wamekasirika waweke magari yao pembeni, kama wamekasirika yale yote ambayo yamependekezwa wayakatae hadharani kwa vitendo sio kwa maneno ya siasa ya humu ndani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amesema yeye tumpe ushirikiano na tumwombe dua, sisi wengine tuko kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, dua zetu, sala zetu, ibada zetu tumemwongezea yeye na tunamuomba na tunawaomba Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye kulipia mafuta nyongeza ile ya Sh.40/=, wataalam wa masuala ya uendeshaji

wamesema hakuna hasara yoyote inayopatikana, ni faida tupu. Kwa hiyo, hii itasaidia pesa hizo zikipatikana si vibaya kama zitapelekwa zikatumike kwa wananchi kwa ajili ya maendeleo ya maji, umeme na mambo mengine. Pia hii imeondoa mzigo, si kwamba kutakuwa na nauli kubwa, mbona petroli inapopunguzwa wamesema hapa wanaofanya hizo biashara, hakuna hasara yoyote, tusitie maneno chumvi kabla mchuzi haujaiva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la utalii. Utalii ni sehemu ambayo ina nafasi kubwa sana. Kuna aina nyingi za utalii, niombe wanaohusika Kijiji cha Makumbusho kiboreshwe tuweze kupata pesa zaidi na tuangalie maeneo mengine ambayo yatatuletea tija kwa maana ya kuingiza pesa. Utalii toke Kaskazini uweze kwenda Kusini, uje Pwani, Mafia tuna utalii wa kutosha, Kisarawe tuna utalii wa kutosha kuna mapango wanakaa popo mule ndani kinyesi cha popo kikichukuliwa kinaweza kikatoa nishati ya aina fulani, niombe hilo nalo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye kitabu cha bajeti, nimefarijika sana na si mimi tu nina jirani yangu Mbunge mmoja yeye pale Dar es Salaam maeneo yake mengi wanakaa watu wanaofuga kuku, sasa akiwa analipinga hili nitamshangaa sana tena nitakwenda hata kuwaambia hao watu wa huko...

**MBUNGE FULANI:** Mtaje.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Sitaki kumtaja yeye mwenyewe ameshajjua. Ufugaji sasa hivi umepunguzwa tozo, kwenye mayai ya kutotolea vifaranga, kwenye vifaranga vyenyewe, kwenye bei ya vyakula, sasa unataka nini binadamu wewe zaidi ya hayo? Huoni kwamba hiyo ni tija kwa wapigakura wako? Jirani yangu, nikisema jirani yangu anajjua, hebu simama ulipongeze basi hata hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongeze lingine kwenye ushuru wa mazao, hili jambo limetusaidia sana hasa sisi ambao



maeneo makubwa sana ya majimbo yetu ni sehemu za wakulima. Mkulima mdogo ndiye aliyekuwa anaumia sana, anatozwa ushuru wa mazao lakini leo akipakia gari lake halizidi tani moja, hadaiwi senti tano. Hii inatoa unafuu wa maisha, inampa nafasi mkulima aweze kuuza alichonacho, apate pesa ajiongezee katika kujiendeleza yeye, watoto wake, familia yake hali kadhalika na kujijenga katika mazingira ya kuondokana na umaskini. Sasa leo basi hata hilo ndugu zangu mnalikataa, mbona inakuwa mushkeli kidogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sitaki kusema hawana jipya, wanayo mapya lakini wajipange, wazungumze yale ya uhalisia wa maisha. Hakuna eneo katika jimbo ambalo halina wajasiriamali, leo wajasiriamali watapewa vitambulisho, watatafutiwa maeneo ya kufanyia biashara zao na sisi ndiyo wasemaji wao, leo hii wewe hata hilo ukilipinga, wewe mtu wa aina gani? Kilimo ukikatae, ushuru wa mazao ukatae, *license* ukatae!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dokta Magufuli katuletea neema, anataka kumtua mzigo mwananchi wa kijijini. Hii Sh.40/= ikienda kijijini wanawake watapunguziwa mzigo wa kubeba maji kichwani, watapunguziwa muda wa kufanya kazi za kutafuta maji watarudi watafanya kazi zao za kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri na niombe Wabunge tusimame kwa pamoja tuhakikishe kwamba bajeti hii inapita, mambo mazuri yanayoletwa na Mheshimiwa Rais yetu yanatimizwa, asilimia inayotakiwa kwa kila eneo ipelekwe lakini maendeleo yabaki palepale kwamba Watanzania tupate faraja, tuondokane na ukubwa wa matatizo ya kujiendesha kimaisha.

Mheshimiwa Spika, sisi tutaungana na wewe kwa yale yote ambayo umeyaahidi jana mbele ya Rais, Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli kuhusu makinikia na mazagazaga mengine yote ambayo yamezungumzwa tutakuwa pamoja na wewe, tutashirikiana na wewe. Nina

uhakika kwenye suala la tozo ya maji, wewe na Wabunge wenzangu tutasimama pamoja kuhakikisha tunatua ndoo ya mwanamke kichwani, tunahakikisha kwamba mwanamke atakuwa na nafasi ya kutosha katika kufanya kazi zake badala ya kwenda kukaa saa sita, saba anasubiri maji ayafikishe nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zaynabu Vulu. Sasa naomba kumwita Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Nianze na ugatuzi mikoani, jinsi sasa hivi Serikali inavyo-*treat* masuala ya Serikali za Mitaa ni kama vile Serikali za Mitaa hazitakiwi. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri Serikali hii inachotaka kukifanya ni kile ambacho Mwalimu Nyerere aliwahi kukifanya, kikashindikana na akaanza tena ku-*empower Local Government*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa TAMISEMI wote hapa kila jambo likifanyika wanaelekeza kwamba kwenye *Local Government* nyie Wabunge ni Madiwani, mkakusanye hela, mhakikishe mambo yanafanyika lakini wakati huo huo mnanyang'anya vyanzo vyote vya mapato kwenye *Local Government*, kwa hiyo, mnasema jambo lingine na huku mnatenda jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ni kwamba bajeti ya Mheshimiwa Waziri muundo wa ukusanyaji kodi una-*cripple* utendaji wa *Local Government*. Mlitoa *Property Tax*, marejesho yanayorudi kwenye *Local Government* yamekuwa ni kidogo sana ukilinganisha na jinsi tulivyokuwa tunakusanya. Kwa mfano, Iringa Mjini tulikuwa tunakaribia kupata karibu shilingi bilioni moja sasa hivi mmetuletea kama shilingi milioni 200 na bado *main power* watu wa *TRA* wanahitaji kutoka huko kwenye *Local Government* kitu ambacho hakina sababu mngetuachia tukusanye wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine kubwa ambalo tunalijadili wote na ambalo nami nataka niliseme kuhusiana na suala ambalo kama Taifa tunataka tupasuke lakini wakati huo huo hatutaki kwenda kwenye kina kuhusiana na suala hili la madini. Hili suala la madini mimi bado narudia *approach*, hawa wawekezaji waliokuja hapa nchini *is unfair to call them* ni wezi, mimi sikubaliani kuwaita kuwa wao ni wezi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mwaka 1997 na 1998 kuna sheria zililetwa humu ndani Bungeni na zikapitishwa. Chama cha Mapinduzi mlikuwa na sera yenu na mkanadi kwenye Ilani, Rais anapochaguliwa nyuma anasukumwa na *policy* ya chama, mtuambie sasa hivi *policy* ya madini ya chama chenu ni ipi. *Policy* ya madini ya chama chenu mkaleta, zikapitishwa humu ndani na haya mambo yote ambayo hawa wawekezaji waliingia nchini yalipitishwa kwa mujibu wa utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge tusishabikie hivi vitu bila sababu kwa sababu mambo haya kabla mikataba hajafanyika, kuna timu za wataalam zinakaa, zinajadiliana baadaye Makatibu wa Wizara wanakaa, wanapitisha baadaye Mawaziri mnakaa ndipo Rais anasaini. Vinginevyo mtuambie hata Mheshimiwa Magufuli hizi nyumba za Serikali aliuzam peke myake na kama aliuzam peke myake mna yeye tumchunguze aliuzaje nyumba za Serikali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kwenye kampeni mlisema ilikuwa ni *collective responsibility*...

**SPIKA:** Kidogo tu Mchungaji ...

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

**SPIKA:** Siyo nia yangu kukukatiza na dakika zako nikuhakikishie kabisa tutakutunzia na kwa sababu wewe ni Mchungaji hata ukitaka nusu dakika ya ziada utapata.

Umezungumzia habari ya kutetea hawa watu kwamba siyo wezi, iko hivi, kama mtu mmekubaliana kwamba atatoa kontena la tani 20 lakini yeye anajaza mzigo tani 25, 27 na kadhalika. Unakamata kule bandarini mzigo wa aina hiyo, huyo mtu utamwita ni Mchungaji wa Kanisa, Shehe au mwizi?

**WABUNGE FULANI:** Mwizi.

**SPIKA:** Kama mtu anakwambia anachukua makinikia kwenda kuchenjua na sababu ya kuchukua makinikia haya ni kwa sababu hapa Tanzania hatuna mtambo huo wa kuweza kufanya kitu hicho na ndiyo sababu ya makubaliano. Kumbe keshayauza juu kwa juu hapo yalipo wala hakuna mtambo wowote anaopeleka kwenda kufanya hicho kitu, huyo mtu hajawa mwizi?

**WABUNGE FULANI:** Mwizi.

**SPIKA:** Sasa nimetoa mifano miwili, mitatu lakini mifano iko mingi ya kwamba hata kama mkataba ni mbovu lakini bado ndani ya mkataba huo mbovu ule ukiukwaji ni mwingi wa kuonesha kwamba kuna wizi na dalili za wizi na dhamira ya wizi. Kwa hiyo, ushauri wangu tu kwa Mchungaji, najua hujasikiliza vizuri hizi hotuba, hujakuwepo, kukuambia tu kwamba hawa wezi wetu hawa, kwa kweli kwa tabia na mwenendo huu ni wezi tu, endelea kuchangia. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nimekusikia, naomba ninukuu kidogo, nikumbushe zile sheria ambazo Bunge hili lilizipitisha na *policy* ya Chama cha Mapinduzi ilisimamia sheria hizi. Sheria ambazo zilitungwa na Bunge hili, namba moja, Sheria ya mwaka 1997 iliwapa wawekezaji wa kigeni ulinzi mkubwa wa manufaa mengi kama vile kuondosha nje fedha na faida yote wanayoipata kwa uwekezaji wao nchini na mikataba ilikuwa siri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili, Serikali hii hii ilikuwa inaongoza, Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 1997 iliwapa wawekezaji wa kigeni ulinzi mkubwa na manufaa

mengi kama vile kuondosha fedha nje na faida yote wanayoipata kwa uwekezaji wao nchini, wanaondosha vyote sheria inasema hivyo, sasa tunawaitaje wezi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine, mwaka 1997 Bunge lilipitisha Sheria ya Madini ambayo ilitamka kwamba mwenye miliki ya madini na fedha yote itokanayo na mauzo ya madini ni mwenye leseni ya kuchimba madini hayo...

## T A A R I F A

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Endelea Msigwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji pokea taarifa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa rafiki yangu Peter Msigwa, makosa yamefanyika, sheria mbaya zilikuwepo, kwa sheria hizo tumeibiwa. Mheshimiwa Rais amekuja, kwa uzalendo wake kwa sababu aliapa kuilinda nchi hii, amegundua tunaibiwa, anasema sasa Spika nenda Bungeni ukabadilishe sheria hizo ili tukomeshe haya, tunaachaje kumpongeza? Naomba sana Waheshimiwa Wabunge huu siyo wakati wa kutafuta nani ametufikisha hapa, ni wakati wa kusahihisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mwenzangu, naombeni tuache kupiga kelele, hapa kinachosemwa kama mnasema semeni tuwajue basi kwamba yanayofanyika ni sawa, sisi tunataka tuyasahihishe, tunataka mwizi wetu atulipe pesa zetu, nyie mnakataaje?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Lazima mtuambie jamani. Hii ni vita, nilifurahi sana Mheshimiwa Hasunga asubuhi

alisema lazima Bunge hili tutoe *statement* ya kumpongeza Rais kwa kazi kubwa aliyofanya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla Mchungaji hujapokea taarifa hiyo na mimi niongezee tu kidogo, yaani mambo haya yanataka utulivu kuyaelewa kwa uhakika na ukweli wake, kila jambo huwa lina historia yake. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tufuatilie zile taarifa mbili tuzisome sisi wenyewe tuzielewe. Kwa mfano, Mchungaji anasema *rightly* kwamba zilipitishwa nafuu za uwekezaji zilizoruhusu wawekezaji hawa wakombe faida yote wapeleke kwao. Nataka kumwambia taarifa ile inasema, wala hiyo hela haijawahi kuwepo hapa yaani hata haya makontena washalipana huko kwa huko, ziko kwenye mabengi ya huko, kwa hiyo hapa wanakomba nini? Kwa hiyo, unaweza ukawa na taarifa wala haziko sahihi pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninachotaka kusema ni vizuri tufuatilie ili tunapokwenda na haya mambo tuelewe vizuri, tunaposema hawa watu wako hivi maana yake wakishauziana wanauziana huko huko, hela benki wanaweka huko huko. Inafanya hata *exchange rate* zetu hapa nyumbani tunakuwa kama siyo nchi ambayo tunamiliki madini yenye thamani kubwa. Hata *Tanzania Shilling* yetu ingekuwa na thamani, hizo hela zingekuwepo halafu zikakombwa angalau zingekuwa na *impact* fulani.

Mchunganji tuko pamoja katika hili siyo kwamba tunakulaumu, hapana. Tuko pamoja katika ugonjwa huu, tunaugua pamoja, tunataka sasa namna ya kutoka pamoja, Mchungaji endelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, mjadala ungekuwa mzuri kama tungepeana uhuru wa kuzungumza kwa sababu wenzetu wanazungumza mpaka wanaongezewa na dakika, *you got to see our views, smooth water never develop a skillful sailor. You guys you are looking for smooth water*, ukitaka upate baharia mzuri akumbane

na maji magumu, hebu mpate maji magumu ili muonekane umahiri wenu basi, mbona mnaogopa tukisema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokisema, hizo sheria zilikuja kwa Hati ya dharura hapa, tunachogaombana hapa, Serikali inafanya kazi kwa kuwajibika wote, lakini Mheshimiwa Rais mnalosema tumshangilie na tumuunge mkono, hakuna mtu anayekataa kuzuia wizi unaoonekana lakini Mheshimiwa Rais alikuwa miongoni mwa Baraza la Mawaziri. Wakati Zitto anazungumza na Karamagi hapa alikuwa ni miongoni mwa waliosema Zitto asulubiwe wakamtoa Zitto nje kuzungumza hii mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo haya masuala ya madini...

## T A A R I F A

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa siyo nia yetu kukukata sana lakini ndiyo yale niliyosea mwanzo, tukikuambia utoe ushahidi kwamba Mheshimiwa Rais yeye kama Mbunge wa Chato wakati ule alikuwa ni mmoja wa waliosema haya kweli utatoa ushahidi huo kweli?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Huoni kwamba hujilindi kwenye kuzungumza?

**MBUNGE FULANI:** Alikuwa Waziri.

**SPIKA:** Yaani mimi nia yangu uchangie tu vizuri maana sisi ni viongozi tunapotosha wananchi. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya taarifa sijui hata iko wapi hiyo taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ni huku.

**SPIKA:** Ni huku eeh.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Kwa Bwege.

**SPIKA:** Taarifa kwa nani?

**WABUNGE FULANI:** Bwege.

**SPIKA:** Unampa taarifa nani Mheshimiwa?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Nampa taarifa Mheshimiwa Msigwa.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa Kusini.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa Mheshimiwa Msigwa, tatizo lililokuwepo Serikali iliyofanya makosa ni Serikali ya CCM, hii si ni Serikali ya Magufuli hii? Sasa msichanganye mambo, Serikali iliyofanya makosa ni ya CCM, hii ni Serikali ya Magufuli, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji taarifa hiyo imefutwa, kwa hiyo, huna haja ya kujibu, endelea. *(Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, lakini nimeipokea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alichokuwa anasema wajina wangu Peter Serukamba nakubaliana kabisa, lakini mimi siyo mtu ambaye napenda ku-*embrace mediocrity*. Kwa nini nasema hivyo? *Let us be honesty*, hakuna mtu anayekataa tusiibiwe lakini kama Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Spika unasema kwamba siwezi kutoa ushahidi, Chama cha Mapinduzi ndiyo mmekuwa *majority* humu ndani, kwa hiyo, sheria yoyote hapa ndani haiwezi kupita bila ninyi kuipitisha. Kwa hiyo, sheria zote ziwe nzuri, ziwe mbovu zilipitishwa na Chama cha Mapinduzi.



Mheshimiwa Spika, sasa tunachotaka kukisema kama Rais ni muungwana, anajua hawa hawa akina Tundu Lissu ambao leo mnawatukana walipambana na haya mambo toka zamani, asimame kwenye *television* aseme kwamba mimi nimegundua wezi hawana Chama, wanaweza kuwa CCM wanaweza kuwa CHADEMA na mimi nimegundua ndani ya Chama cha Mapinduzi kuna majizi. Kwa sababu ndani ya Chama cha Mapinduzi kuna majizi naomba tushikane wote mikonong'oe wezi CHADEMA na tung'oe wezi CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashangaa sana wenzangu wa Chama cha Mapinduzi, kimsingi Rais anachokifanya Sera ya Chama cha Mapinduzi ameweka pembeni anaongoza kama vile ni Mgombea Binafsi. Hiyo mimi namuunga mkono kwa sababu sera yenu kuhusu madini ni hiki kilichofanyika, sasa leo mnageukaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasisitiza kama kweli Mheshimiwa Magufuli ana dhamira ya kweli ya kuleta mabadiliko katika nchi hii hapa, alete mabadiliko kwenye Katiba ili Marais waweze kuhojiwa. Hiyo ndiyo dawa pekee kwa sababu vinginevyo hata yeye ameua nyumba za Serikali kitu ambacho siyo kweli asingeuza bila Mkapa kusaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshangilia Muhongo kuondoka wakati sheria hizi mbovu maskini hata Muhongo hakuwepo wala hii sera hakuwepo, leo tunashangilia Muhongo kaondoka hakuwepo, *he was not here*.

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa unatukandamiza wote unamtoa Muhongo sijui kuna mkataba gani hapo? (Kicheko)

Mheshimiwa *Chief Whip* tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, nataka kuomba suala la utaratibu. Suala langu la utaratibu nalotaka kuomba linakwenda moja kwa moja kwenye Kanuni ya 64 na ina vipengele vingi ambavyo sasa Mheshimiwa Msigwa kadri anavyoendelea kuchangia anataka kwenda nje ya utaratibu wa kikanuni. Kwa sababu mjadala uliopo hapa mbele yetu unahusu bajeti lakini tunapoendelea kuchangia bajeti ni kweli kabisa tunachangia pia suala zima la maliasili zilizoko katika nchi yetu ya Tanzania kwa maana ya kuzilinda kama vile jambo ambalo limetokea katika nchi yetu ya Tanzania likiongozwa na Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli kwa nia njema ya kulinda maslahi ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu wangu, sioni kama ni busara katika jambo kubwa na lililofanywa kwa uzalendo mkubwa na Mheshimiwa Rais kama hili alilolifanya jana, Mchungaji Msigwa aamue sasa kuigeuza hoja hii na kutumia mifano ambayo inakwenda kuvunja Kanuni ya 64(b) kutaka sasa kumtumia Rais kwa vielelezo ambavyo vinapoteza dhana nzima ya mjadala wetu lakini na jambo jema ambalo amelifanya Mheshimiwa Rais wetu la kuhakikisha kwamba mali na rasilimali za nchi yetu ya Tanzania zinaendelea kulindwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mchungaji Msigwa aendelee kuchangia hoja iliyoko mbele yetu lakini kutaka kutumia jina la Rais kulithibitishia Bunge hili kwamba Rais ndiyo amefanya makosa hayo yote wakati siyo kweli...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Na wote tunaona baada ya Mheshimiwa Rais kuingia yeye sasa ndiyo amesimama imara kusaidia, kuimarisha na kuweka sawa mambo yote yanayoendelea katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala hili la kiutaratibu lifuatwe vinginevyo kwa kweli tunaenda kinyume na utaratibu wa Kanuni zetu za Bunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa nadhani ushauri uliotolewa ni ushauri mzuri tu, hauna sababu ya kuwa na ugomvi. Tunapogombana au tunapotofautiana ni mahali padogo tu kwamba lengo letu ni kusonga mbele, mwenzetu unajaribu zaidi kuangalia nyuma, sasa inakuwa ni gari ambalo haliendi kwa sababu kuna wanaotaka liende mbele, wanaweka *gear* ya kwenda mbele, kuna wanaotaka lirudi nyuma wanaweka *gear* ya kurudi nyuma, sasa tutabaki tumesimama, hatuendi mbele wala haturudi nyuma.

Kwa hiyo, ni ushauri tu wa kijumla, mambo haya yanahitaji kama tungekuwa kwenye semina hivi ili kila kipengele mnachonyanyuka nacho kipate majibu muafaka sasa hapa siyo uwanja wake mzuri sana kwa sababu hata hayo mambo ya kuuza nyumba kwa mfano, hizi zilikuwa Sera za *World Bank*, nchi nyingi tu ziliingia katika jambo hilo wakati ule ule.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Ndiyo, Malawi waliuza nyumba za Serikali ambao hamtembei ...

**MBUNGE FULANI:** Sumaye.

**SPIKA:** Zambia ninyi mnaotoka karibu na mpaka nyumba za Serikali ziliuzwa, ambao mpo Kagera kule Uganda nyumba za Serikali ziliuzwa na mahali kwingi ilikuwa hivyo. Huu ni upepo, ni msukumo maalum ndiyo maana tunasema Wabunge msome tuelewane.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Lakini mwisho wako watu unawataja kwa kuwasifia na kadhalika, mimi sitaki kuwataja lakini kila wakati nakuambieni mambo ya kuwatajataja watu kwa majina na kuwasifia kwamba wao ni *special*, mnawa-*expose* sana. Wewe unaweza ukamsifia sana mwenzako kumbe humjui yule mwenzako lakini kuna wanaomjua vizuri zaidi. Kwa hiyo, ni bora tu ukachangia hoja kuliko kum-*expose* mtu kama huyu fulani ni msafi sana, yeye alisema hivi, tunacheka lakini mtasababisha huko mbele, unaweza kukuta umemwekea moto mguuni sasa watu wakafungua huyo unayesema msafi na nyie watu wa dini mnajua mmefunga wasafi wachache, kama wangekuwa wengi msingekuwa mnafunga. Mheshimiwa Mchungaji malizia dakika zako bwana. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika wetu, ningepomba uwe Hakimu, tuache tu tucheze na hawa watu, ni wepesi sana hawa kucheza nao, usiwashikilie mkono, unanishika mno mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, rasilimali za nchi hii hatutaki ziibiwe...

**MBUNGE FULANI:** Ni zetu sote.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Vilevile tunatakiwa tuwe *skillful* tunapo-*deal* na hawa tunaowaita wezi. *These are not intruders, we invited them in this country.* Sasa kwa sababu tuliwa-*invite* siyo kwa sababu tu tuko vitani hatuendi *blindly* lazima tuwe *skillful*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunachokizungumza hapa hata haya mambo unayosema yalikuwa ya *World Bank* hata madini ni *World Bank* hivyo hivyo, tuko-*pushed* hivyo hivyo lakini sisi hatukulazimishwa kula, hawatukushikia, tulisaini hapa wengine wakaenda usiku, mkapiga mayowe hapa, mkaunga mkono. Bunge lililopita kwa Mheshimiwa Spika Makinda nakumbuka mara ya mwisho hapa zililetwa sheria tatu za dharura, Mnyika alikuwa anaomba...

**MBUNGE FULANI:** Kwa siku moja.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kwa siku moja, tukalazimika tukatoka nje, tukazomewa, tukafukuzwa humu ndani sasa leo mnasema twende mbele tu, tulitoka humu ndani wote, mnasema twende mbele tu tusikumbuke nyuma, *why?* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hii tunayosema kama mpo *sincere* mnataka tupigane hii vita kwa sababu kwanza hii vita mlikuwa hamuitaki, sasa kwa sababu Mheshimiwa Rais, yeye ameamua kutofuata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msigwa muda wako umeisha.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Aaaaah.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saada Mkuya atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kupata nafasi hii kuchangia bajeti yetu ya Serikali mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwanza nami nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha. Naamini kufikia hapa kwa uzoefu haikuwa kazi rahisi, tumefanya kazi kubwa na tumeleta bajeti ambayo inatafsiri dhana nzima ya Tanzania ya Viwanda. Mengi sana yamo na yanatafsiri hilo, kwa hivyo, ni lazima tukupongezeni kwa kazi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda niende katika maeneo *specific*, kwanza kuhusiana na ongezeko la Sh.40/= katika mafuta kwa ajili ya ku-*compensate* ile *Road License fee*

ambayo imefutwa iliyokuwa ikilipwa kila mwaka. Kiutawala nadhani hili limekaa vizuri zaidi na naamini kwamba Serikali itapata fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kutekeleza bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, binafsi naomba badala ya kuwa Sh.40/= tungeongeza Sh.10/= ziwe Sh.50/= kwa sababu tutapata ongezeko la Sh.6,950,000,000/=, hizi Sh.10/= *specific* zikaingie katika Mfuko wa Maji kama vile ambavyo tulikuwa tumeshauri kabla. Kwa sababu hizi Sh.40/= zinakwenda kutekeleza bajeti kwa ujumla wake, naomba tuongeze Sh.10/= tu ili ziwe Sh.50/= ziende zikaingie katika Mfuko wa Maji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji hususan katika maeneo ya vijijini ambapo ndipo kuna shida kubwa sana ya maji ukilinganisha na mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pengine wenzangu wanaweza wakauliza sasa tunaenda kuwapa shida sana wananchi ambapo hawatunii magari, lakini maendeleo ya nchi hayahitaji mtu yupo wapi, maendeleo ya nchi hii yanamhitaji mtu aliyeko kijijini na yule ambaye yuko mjini. Huko vijijini ambapo tunasema hawa watu tumewabebesha mzigo kutokana na kuongeza Sh.40/= ya mafuta ya taa lakini wao wana shida kubwa ya maji, wanahitaji sana barabara na umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hili ongezeko ambalo nashauri Mheshimiwa Waziri lifikirie liende *specific* kwa ajili ya kuondosha shida ya maji katika maeneo hasa ya vijijini. Nadhani siku ya bajeti ya maji karibu asilimia 60 ya Wabunge wote walisimama na wakapata nafasi ya kuongea kwa sababu ya dhiki ya maji ambayo ipo katika maeneo yao. Kwa hiyo, naomba hili tulifikirie ili twende tukatekeleze bajeti kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile na mimi nisiwe mkosefu wa fadhila sana, niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua za kiutendaji anazozichukua kuona kwamba *resources* za nchi zinafaidisha wananchi wenyewe. Ni kweli fedha nyingi zimepotea lakini *it is high time now* kuweza kusimamia zaidi hizi sekta za

kiuchumi. Inawezekana sana kama tungekuwa tumesimamia vizuri basi tusingekuwa hapa tunadonoa Sh.10/=, Sh.20/= kwenda kupeleka katika Mifuko ya Maji.

Mheshimiwa Spika, naamini kama tungekuwa tunasimamia vizuri, kwa utajiri ambao Tanzania upo tungeweza kutekeleza bajeti yetu kwa kutegemea kiasi kidogo sana cha misaada ama mikopo ya kibishara kutoka nje. Basi ndiyo hivyo imetokea, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amejitoa kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili bajeti iwe bajeti ambayo inaleta ufanisi, ni lazima bajeti hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iweze vilevile kuona ina-*support* vipi bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwenye hili Mheshimiwa Waziri nina mambo mengi kidogo. Kwanza ni *general budget support* (misaada ya kibajeti). Nimeona katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwamba misaada ya kibajeti tunaotea kupata *around* bilioni 311. Vilevile kuna maoteo ambayo tunatarajia katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesomwa jana ambayo inaelekeza mwelekeo wa kimaendeleo katika mwaka 2017/2018 lakini bajeti hii ambayo inakamilika ina kasoro ya fedha za *general budget support* ambazo zimeandikwa kwamba tutazipata. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hizi fedha kwanza angalau tujue ni kiasi gani mpaka sasa hivi zimepatikana ili kuona kiasi gani kinakwenda Zanzibar kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitakuwa busara sana kama bajeti yetu kwa upande wa Jamhuri ya Muungano inatekelezeka lakini kuna upungufu mkubwa katika kutekeleza bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunaomba tujue ni kiasi gani zimepatikana na hicho kilichopatikana ifanyike haraka, kipelekwe Zanzibar kiweze kutekeleza miradi ya maendeleo. Hii vilevile ni pamoja na hizo fedha za mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, mwaka jana tulibadilisha Sheria yetu ya VAT, kuna bidhaa ambazo zilikuwa zimezalishwa hapa na zimekwenda kutumika Zanzibar. Kuna fedha za *refunds* zinakaribia shilingi bilioni 21, bado hazijapelekwa Zanzibar na hili ni tatizo kubwa sana. *Refunds* za VAT pamoja *Excise Duty* zinachelewa kupelekwa Zanzibar, sasa kule tunachelewesha kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri pamoja na usimamizi mzuri wa kibajeti tunaomba asimamie fedha za VAT na *Excise Duty* ambazo ni *refund* zipelekwe Zanzibar kwa wakati ili tuweze kutekeleza bajeti vilevile kwa upande ule ambao ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka kuchukua fursa hii kupongeza Shirika letu la Bima la Taifa, kwa mara ya kwanza limetoa gawio kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania shilingi bilioni 1.7. Ni kwa mara ya kwanza limetengeneza faida na limetoa gawio. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri katika eneo hili vilevile tulishauri kwamba taasisi za Serikali pamoja na vyombo vyake viwe vinaweka bima kupitia Shirika letu, hii itaongeza faida katika *operation* za Shirika letu la Taifa na kwa maana hiyo sasa hilo gawio litazidi zaidi. Kwa hiyo, tunaomba hilo lizingatiwe taasisi zetu za Serikali ziwe zinaweka Bima kupitia Shirika letu la Taifa ili tuweze kupata fedha zaidi kutekeleza bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili katika hilo hilo kuna ombi la kuanzisha Bima hii ya Kiislamu *(Takaful)* limekaa kwa Mheshimiwa Waziri muda mrefu sana bila ya kupatiwa majibu. Hizi ni *products* ambazo zinaendana na wakati tu. Kama tumeruhusu Benki zi- *operate* kwa *principle* za Kiislamu, kwa nini tunazuia bima zisi-*operate* katika *principle* za Kiislamu? Hili linawezekana lakini limekaa sana muda mrefu kwake bila kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa litekelezwe ili tuone kwamba wale ambao wana imani za Kiislamu na wao



wanapata *products* ambazo zinaendana na imani zao. Ni biashara na ni *products* ambazo zinakuwa kutokana na mahitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusiana na Benki yetu ya *FBME*, Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri kwamba hii benki sasa hivi imeshanyang'anywa leseni hai- *operate* tena. Kuna mambo ya kadha wa kadha yametokea lakini wananchi wameweka fedha zao *FBME* na katika matoleo ya mwanzo tumeambiwa kwamba hii benki itafanyiwa *auditing two weeks* za mwanzo na baadaye wananchi wataambiwa benki gani watakwenda kuchukua fedha zao. Hivi tunavyokwenda nadhani tunaingia mwezi wa pili, hakuna taarifa yoyote kuhusiana na fedha au zile amana za wananchi ambazo wanataka wao wenyewe kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wetu wa Zanzibar Tawi la *FBME* linafanya vizuri zaidi kuliko matawi mingine ya *FBME* Tanzania. Wananchi wengi wa Zanzibar wameweka fedha zao kwa ajili ya kwenda kutekeleza Ibada ya Hijja baada ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kama leo hatujui wapi fedha zetu tutazipata mnakwaza watu ambao wanataka kwenda kutekeleza hiyo ibada.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tufanyiwe utaratibu kujua kwamba fedha hizi zinapatikana wapi, wananchi waende kuchukua fedha zao ili waweze kufanya pamoja na mambo mengine utekelezaji wa ibada hii muhimu ya Kiislamu baada ya kumaliza Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Namuamini sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, najua hili utalisimamia.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nipate majibu...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kupata majibu ya masuala hayo niliyozungumzia. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Saada Mkuya, siku nyingine ukipata nafasi ya kuchangia utuelimishe kidogo kuhusu Bima ya Kiislamu ni kitu gani siyo wengi tunafahamu. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na wenzangu kuchangia mapendekezo ya bajeti ya 2017/2018 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mpango. Kwanza kabisa nimpongeze sana kaka kwa umahiri mkubwa na utulivu aliotumia siku ya kuwasilisha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyotangulia kusema Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Shabiby kwamba wengi walikuwa wanasema hasikii, hachukui mapendekezo, amechukua mapendekezo na ametuleta taarifa ya mapendekezo ya bajeti yenye tija, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais, nami niseme jamani, niliwahi kusema siku za nyuma, suala la madini linatuhusu watu wote lakini siku Wizara ya Madini inawasilisha hapa chini ya Waziri wa Viwanda na Biashara, aliyesoma taarifa ya Kambi ya Upinzani mdogo wangu Mnyika, alionesha kabisa kwamba Rais ameanza kutatua tatizo dogo badala ya kutatua tatizo kubwa la mikataba.

Mheshimiwa Spika, nami nikasema, anawezaje kuanza na hilo bila kuchunguza na kuona hivi kweli nikivamia mikataba hawa watu ni kweli wanaiba madini? Akaunda Tume ya kwanza, ikatupa taarifa. Tume ya pili, imetupa taarifa na wote tumesikia tangu 1998 mpaka 2017 tumepoteza shilingi trilioni 108. Ukienda kwenye bajeti yetu ya mwaka huu tunayotarajia ianze tarehe Mosi Julai, ni mara tatu ya bajeti tunayokwenda kuipitisha ya trilioni 31.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa, ninachokiona mimi kisiasa kwa sababu wenzetu walikuwa hawaoneshi kuunga mkono kazi anayofanya Rais ya kupambana na wizi wa

rasilimali kwenye madini yanayotoroshwa, sasa wanatafuta *kick* kwa wananchi. Mimi niseme, wananchi ni waelewa, jana kwenye vyombo vya habari nilivyokuwa nasikia wapo wanachama wengi tu wa Vyama vya Upinzani wameamua kuachiaachia nyadhifa mbalimbali ili waweze sasa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme hivi ndugu zagu, haya mambo mazuri ambayo Mheshimiwa Rais anayafanya, hata kama msipotaka kuyaunga mkono, hata kama mtayapekuapekua mnavyotaka kupekua ninyi ili wananchi waone kwamba ninyi ndiyo bora na Rais wa Chama cha Mapinduzi siyo bora, nasema hamuwezi kupata tija katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie dhamira njema ya bajeti hii kwenye suala la viwanda. Tunafahamu kabisa kwamba Kigoma tuna kiwanda kimoja tu cha *Uvinza Salt Mine*. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kuna tatizo la wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi siku za nyuma, tangu 1994 wakaachishwa bila kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni la muda mrefu lakini lilifanyiwa kazi na Serikali na ikataka kujiridhisha ni kweli wafanyakazi wale wana haki za kulipwa? Suala hili likapelekwa mpaka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye naye akalifanyia kazi, akalipekua kisheria akaona kwamba wafanyakazi hawa wana haki kabisa za kisheria kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, suala hili lipo mezani Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango, lina muda mrefu, lipo kwenye meza ya Katibu Mkuu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mpango, alifanyie kazi ili wafanyakazi hawa walipwe. Wapo ambao wameshatangulia mbele ya haki, familia zao zipo, wajane na watoto wapo, watapokea ile haki ambayo wazazi wao walikuwa wapokee.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hilo hilo la viwanda niseme pia tunapotaka tuwe na Serikali ya Viwanda na Nchi ya Viwanda, tusingalie tu baadhi ya Ukanda ndiyo uwe na viwanda na Ukanda mwingine tusiwe na viwanda. Kwa hiyo, ninachoomba, tunatambua kabisa Kibondo pale tuna miwa mingi sana, tunaweza tukaanzisha Kiwanda cha Sukari. Uvinza tunaweza tukaanzisha Kiwanda cha kutengeneza Mafuta ya Mawese na mafuta ya mawese yanalika sana ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, ukienda Marekani kwenye *super market* zile unakuta *palm oil* ziko pale na ni *very expensive*, lakini sasa Serikali kama Serikali bado haijaweka jitihada za makusudi kuongeza tija kuanzisha viwanda katika Mkoa wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la ujenzi wa reli ya kati na ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge*. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa hatua hii ya ujenzi huu lakini niombe, naona kila mkizungumza ujenzi wa reli mnazungumzia itatoka Tabora itaenda Mwanza. Sasa sisi Kigoma kama alivyosema Kaka yangu Mheshimiwa Nsanzugwako tunapakana na Zambia, *DRC* – Kongo na Burundi na mizigo mingi sana inatoka huko. Ukienda *railway* kwenye *department* ya *transportation* ukiwauliza watakwambia mabehewa mengi yanayokodishwa yanapeleka mizigo Kongo na Burundi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tuombe, katika ujenzi wa reli ya kati, mtakapokuwa mmepata mkandarasi wa kuanzia Tabora kwenda Mwanza basi tupate mkandarasi mwingine wa kuanzia Tabora kwenda Kigoma. Tunafahamu kwamba sisi wananchi wa Kigoma huu ndiyo usafiri ambao tunauamini zaidi kuliko usafiri mwingine. Kwa hiyo, tunaomba mtufikirie katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, reli inayojengwa kwa kiwango cha *standard gauge* inapita kwenye Jimbo langu la Uvinza. Niombe, tusiwe na mambo ya kushtukizana, pale ambapo mmeshapanga kabisa

ifanyike *feasibility study* ya kujua reli hiyo itapita kwenye maeneo gani basi mtuambie mapema ili wananchi nao wawe na utayari wa kuipokea hii reli inayojengwa kwa kiwango cha *standard gauge*.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala wetu, majina yote mliyoniletea ninayo na wote ambao mpo kwenye orodha mtapata nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Tukirudi ule muda wetu wa kawaida tutaanza na wachangiaji wa upande wa *CUF* halafu tutaendelea na wengine wote kwenye orodha kama ilivyo kawaida.

### TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe taarifa ya Spika kuhusu maamuzi ya Kamati ya Uongozi. Leo asubuhi mtakumbuka katika Kikao chetu cha Arobaini na Sita cha Bunge, Mheshimiwa Japhet Hasunga, aliomba mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kutoa hoja ya kuwa na Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais kutokana na juhudi zake za kizalendo na hatua alizochukua za kuunda Kamati mbili za kuchunguza masuala yanayohusiana na mchanga wa madini (makinikia) unaosafirishwa nje ya nchi.

Baada ya mwongozo huo kuombwa, nililazimika na niliawatangazieni kuitisha Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kunishauri juu ya jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwataarifu kuwa Kamati ya Uongozi katika kikao hicho kilichofanyika leo tarehe 13 Juni, 2017 hapa nyuma kwenye *Lounge* ya Spika, kimeazimia kwa pamoja kwamba ni busara kwa Bunge kutoa Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa juhudi zake hizo za kizalendo na kuchukua hatua ya kuendelea kulinda rasilimali zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Azimio hilo linaandaliwa na litawasilishwa hapa Bungeni na kushughulikiwa kwa mujibu wa kanuni zetu na taratibu tulizonazo hapa Bungeni. Nami kwa nafasi yangu kama Spika sasa naagiza kwamba Azimio hilo liletwe kesho hapa Bungeni bila kuchelewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, niseme neno moja, wapo wenzetu ambao Bunge hili liliwachukuliwa hatua za kinidhamu mbalimbali, baadhi yao wamekuwa wakijaribu kufanya malumbano na Bunge na baadhi ya kauli zao zimekuwa ni kauli ambazo si njema au si nzuri kihivyo.

Napenda kuendelea kuwashauri kwamba tumewavumilia kwa mengi, lakini kama bado huko waliko wanafikiri wanaweza kuendelea na tabia hizo huko waliko, wajue kabisa bado tunaweza tukawaita na bado tunaweza tukawajadili kwenye Bunge hili na bado wakapata adhabu kubwa zaidi kuliko hii ambayo wamepata. *(Makofi)*

Kama mtu anataka kwenda Mahakamani, anataka kwenda wapi, hivi ukitaka kwenda Mahakamani unawaalika watu mkutano wa hadhara? Jamani njooni kijiji chote mimi nataka kwenda Mahakamani, si unaenda tu. Kwa hiyo, niwape tu onyo la jumla, kama viongozi ni vizuri huzuliwi kuongea lakini ongea vitu ambavyo unataka kuongea lakini ukitaka kupambana na watu wengine nao watataka kupambana na wewe, kwa hiyo utapima.

Baada ya maneno hayo, naomba wale ambao ni marafiki, ndugu na jamaa basi mjitahidi. Nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea, kama nilivyoahidi tutaanza na upande wa *CUF* kama wapo, Mheshimiwa Mtolea Abdallah Ally halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono mawazo mazuri ya Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni kwa namna ambavyo wameichambua kwa kina bajeti hii lakini kwa kutoa mawazo mbadala ili Serikali waweze kuyachukua na kuiboresha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa naamini siyo jambo geni kwa Serikali kuchukua mawazo ya Upinzani na kuyafanyia kazi kwa sababu hata Mheshimiwa Rais ameanza kuonesha njia kwa kuyachukua yale mawazo mazuri ambayo upande wa Upinzani tukiyatoa na kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze sana viongozi wetu wa Kambi kwa pamoja Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali kwa namna ambavyo wanatu-*groom* vizuri ili tuendeleo kutoa michango hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami pia ni miongoni mwa wanaoshangazwa na bajeti hii. Kama ambavyo mnasema bajeti ya kihistoria maana yake imeduwaza wengi na mimi pia ni miongoni mwa watu ambao tumeduwazwa na bajeti hii hasa kwa kutotarajia kuona kwamba bajeti ingeongezeka kufikia shilingi trilioni 31.7 wakati ya ile shilingi trilioni 29 tulishindwa kufikia. Naona ni kama vile mgonjwa ambaye ameshindwa kunywa uji sasa tunampatia pande la mhogo. Kwa mtazamo huo unaona kabisa tunatengeneza bajeti ambayo hatuwezi kwenda kuitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilifikiri baada ya kuona kwamba bajeti ya 2016/2017 tumeshindwa kuitekeleza hata kwa asilimia 40, Serikali ingerudi nyuma na kujiuliza wapi ilikosea. Kwa sababu unapokuwa na bajeti ambayo unashindwa

kuifikia maana yake ama mli-*overestimate* kwamba makadirio mliyoyafanya yalikuwa makubwa kuliko uwezo halisia. Kwa hiyo, nilitegemea leo bajeti yetu ishuke kwenye shilingi trilioni 29 iende kwenye uhalisia badala ya kuipandisha kuipeleka kwenye shilingi trilioni 31.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu moja ya vitu ambavyo vimechangia bajeti yetu 2016/2017 ku-*fail* ni mazingira mabovu tuliyonayo sasa kati yetu na wahisani wetu. Mazingira hayo bado hayajaondoka, mazingira yetu hayawavutii wahisani kuendelea kutupatia zile fedha ambazo walikuwa wakiahidi. Kwa hiyo, maana yake hata kwenye bajeti hii tunayoendelea nayo na yenyewe itapata changamoto zilezile ambazo bajeti ya 2016/2017 ilizipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wahisani hawaridhiki na uchaguzi wa Zanzibar ulivyoendesha. Tuliyasema haya wakati tunachangia bajeti ya 2016/2017, kwamba haya mazingira yaangaliwe. Tumekuwa tukijinasibu kwamba sisi ni kisiwa cha amani, kisiwa cha utulivu lakini kiukweli mazingira ya siasa za Zanzibar hayaoneshi kama kweli sisi ni watulivu na tuna amani kiasi hicho. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha inatengeneza mazingira mazuri ili yale makandokando yaliyozunguka yaweze kuondoka na wahisani hawa waendeleo kutuamini na kutuletea misaada yao kama ambavyo ilikuwa hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili mambo mengine haya ya kuiminywa demokrasia. Bado demokrasia katika Awamu hii ya Tano imeendelea kuminywa hapa nchi, tunazuiwa kufanya mikutano ya kisiasa. Kwa mfano, mikutano ya kisiasa ipo kwa mujibu wa sheria. Sheria iliyoanzisha Mfumo wa Vyama Vingi inavitaka vyama kuendeleza mitandao yao huko nje. Leo mnaambiwa kwamba msifanye mkutano ya kisiasa kwamba kila mtu afanye mkutano kwenye eneo lake aliloshinda.

Mheshimiwa Spika, tuna vyama vilivyosajiliwa zaidi ya 22 si kila chama kimeshinda uchaguzi, kuna vyama havina



hata mjumbe wa Serikali ya Mtaa, huyu akafanyie wapi siasa yake? Kwa nini huyu abanwe kufanya siasa? Kwa nini tutenge kwamba watu walioshinda tu ndiyo wafanye siasa wengine wakafanyie wapi? Ni lazima na wao wafanye siasa ili uchaguzi ujao waweze kushinda wapate wawakilishi kwenye nafasi hizo. Sasa tunapowanyima nafasi watu hawa tunaiminya demokrasia kwa upana wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi wasiwasi uko wapi, kama sisi Wapinzani tunasema uongo tufanye kwamba CUF tumefanya mkutano pale Mwembe Yanga Temeke tukasema kwamba maisha ni magumu kwa Watanzania, si kesho CCM na wenyewe wafanye mkutano Jangwani waseme maisha ni mazuri. Kwa sababu hii siasa tunayoifanya ni vita ya maneno tu, hasira zinatokea wapi? Mwenzi akisema hivi na wewe sema lile unaloliona la ukweli, halafu wananchi watakwenda kutupima 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niishawishi Serikali na naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri amepata Uwaziri kama mtaalam na siyo kama mwanasiasa japokuwa ameanza kuonesha *interest* za kuitaka Jimbo la Buhigwe, nikutakie kila la kheri, lakini kwenye haya mambo ambayo ni ya kisiasa lakini yanaharibu uchumi aiambie ukweli Serikali kwamba tubadilisha mazingira haya wahisani hawa waendeleo kutusaidia, lakini akiyakalia kimya mwisho wa siku mzigo unakuja kubebeshwa wewe. Watu wanaamini Mheshimiwa Waziri ni mtaalam mzuri sana, amefanya kazi ya kuishauri Serikali ya Awamu ya Nne na ilifanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali iweke mazingira sawa ili wahisani waendeleo kutoa zile *pledges* zao kama walivyokuwa wanafanya kwenye awamu zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ahadi za Mheshimiwa Rais, naamini kabisa Serikali hii inafanya kazi za kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ameahidi kwenye kampeni zake kutoa milioni 50 kwenye kila mtaa.

Tunakwenda kwenye bajeti ya mwaka wa pili huu hiyo milioni 50 haonekani, huku ni kumgombanisha Mheshimiwa Rais na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wana wasiwasi wa utekelezaji wa hiyo ahadi wangechagua hata *pilot regions* au *districts* kwamba hizi wilaya mbili au tatu tupeleke hizo milioni 50, tuzisimamie tuone utekelezaji wake utakuwaje. Hata Watanzania wangeona ile nia ya kweli ya kutekeleza ahadi hiyo, lakini wamekaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia aliahidi kutoa *laptop* kwa Walimu wote leo tunakwenda kwenye bajeti ya mwaka wa pili huu, tumepitisha hapa Wizara ya Elimu, Wizara ya TAMISEMI hakuna hata moja imetenga fedha kwa ajili ya hizo *laptops* za Walimu na hii ni bajeti kuu pia hili halizungumziwi. Kwa nini tunamgombanisha Mheshimiwa Rais na wananchi wake? Naitaka Serikali imsaidie Mheshimiwa Rais kutekeleza ahadi zake ili aendelee kunukia na kupendeza mbele ya macho ya watu aliowaahidi na walimpa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka kuchangia hapa ni namna ambavyo Serikali inazidi kupoka madaraka kutoka kwenye Serikali za Mitaa. Mwaka jana wametuchukulia *Property Tax* kibaya zaidi siyo kuzichukua hizo *Property Tax* lakini hazikukusanywa. Mpaka tarehe 31 Machi, Serikali ilikusanya asilimia 20 tu katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hata hao watumishi wenyewe wa kwenda kukusanya *TRA* hawana kwa maana hawajajipanga, wanaazima humo humo kwenye Halmashauri ndiyo wapate watu wa kwenda kuwakusanyia. Kama walikuwa hawajajipanga kwa nini wanalichukua jukumu hili, kwa nini wasiendelee kutuachia sisi tukakusanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hapa badala ya kujikita kwanza wajipange vizuri kwenye kukusanya *Property Tax*

wameongeza na mabango pia maana yake wanakwenda kuziua Halmashauri zetu kwa kutunyang'anya vyanzo vya mapato.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa mwongeeji kuhusiana na lile jambo alilosema kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi *Laptop...*

**MBUNGE FULANI:** Kenya.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ilikuwa ni uzushi wakati wa kampeni na Chama Makao Makuu kilitoa taarifa kwamba hakukuwepo na jambo la aina hiyo kwenye Ilani wala kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**SPIKA:** Alikuwa anaweka sawa tu kwamba siasa za uzushi isiwe sehemu ya siasa zenu Waheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii adhimu ili nami nitoe mchango wangu. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais jinsi anavyokwenda, nasema mwenye macho haambiwi tazama, tunasonga mbele. Pili naipongeza Wizara ya Fedha kwa hotuba yake ya Bajeti Kuu ni bajeti nzuri ya kiwango. Nichangie kidogo tu kwa maana ya kufanya marekebicho madogo, lakini bajeti ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza bado Tanzania tunahitaji maji na hasa vijijini. Maeneo makubwa na mengi suala la maji ni shida kubwa. Niungane na ushauri wa Kamati ya Bajeti, moja ya vipengele ambavyo walikuwa wameshauri ni kwamba ile Sh.40/= tuongezee Sh.10/= ifike Sh.50/= ikaungane na ile tuipeleke kule kwenye Mfuko wa Maji. Tafadhali sana naomba ifanyike hivyo, vinginevyo hali ya maji bado ni tatizo kubwa sana hata katika uwekezaji huu bado itakuwa ni shida na hasa kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili lake la maji hilo hilo naomba sana Wizara inayohusika na maji igawe rasilimali maji kwa usawa. Kuna maeneo hasa ya vijijini asilimia zile, nimejaribu kuangalia bajeti ya maji ukurasa wa saba walipozungumzia kwamba asilimia 72.58 vijijini wanapata huduma ya maji ndani ya mita 400, inawezekana ni sawa, lakini baadhi ya maeneo, baadhi ya vijiji si sawa, Jimbo ninalotoka mimi la Manyoni Mashariki ni asilimia 18 tu, ndiyo wanaopata huduma ya maji vijijini. Ndio maana nimesema tugawe hizi rasilimali maji.

Mheshimiwa Spika, hii fedha iende sawa kama kuna maeneo yako chini, tuwanyanyue na wenyewe, wale ambao wamefikiwa hiyo asilimia 72 basi sawa, lakini hawa ambao wako chini, wanyanyueni na wenyewe twende kwa pamoja, nataka nilisitize hilo kwa sababu Manyoni kule hali ni mbaya na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili bado nalalamika kwamba miji na vijiji naomba tuvipange kwa maana ya kupanga na kupima, bado hali ni mbaya,

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kupanga miji na vijiji kwanza ukusanyaji wa mapato unakuwa rahisi sana, tunaimba *property tax*, tunaimba *land rent*, haitakuwa na ubishi inapokuwa tumepanga miji yetu, lakini pia huduma zingine zote. Unapokuwa umepanga mji wako au vijiji vyako huduma zote zinakwenda vizuri na ndio ustaarabu wa kibinadamu hatuwezi kukaa kama nyanya tumerundikana hivi, haiwezekani tupange miji yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi mimi nasema imeelemewa isaidiwe. Kusaidiwa kwake, tuwape Halmashauri nguvu za kupima vijiji na miji na unapowapa Halmashauri kazi hii maana yake ni kwamba uwawezeshe ile *retention* ya fedha, makusanyo ya kodi za viwanja zile ile asilimia 30 bado naihitaji ibaki kwenye Halmashauri tuwasaidie Wizara ya Ardhi kupima, wenyewe hawataweza. Kwa mfano, mwaka jana wamefanya kazi kwa asilimia 30 tu ile fedha imetoka asilimia 30 tu. Hawawezi kupanga na kupima miji wao wenyewe, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, wamepeleka wataalam kule kuna *Valuer* kule kuna *Surveyor* kule, kuna Maafisa Mipango Miji kule Halmashauri, sasa kwa nini tusiwaachie hii asilimia 30 wapime huko wawasaidie. Wao wabaki tu ku-*control*? Kwa nini wang'ang'anie kukumbatia hii kazi na hawawezi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Fedha, ufafanuzi kwenye ukurasa 48 viwango vya kodi za majengo. Hapo kuna utata kidogo. Mimi ni mtaalam, unaposema *flat rate* kwa maeneo ambayo hayajafanyiwa *valuation*, sawa sikatai *flat rate* lakini *flat rate* ifanane fanane basi. Unaposema Sh.10,000/= kwa majengo ambayo yako chini, hujaweka pia *categories* ni ya aina gani, kuna watu wamejenga (*massions*) majumba makubwa lakini yapo chini, ukiangalia jumba kubwa zuri, hamjatenganisha ni biashara au ni ya makazi hii Sh.10,000/=, utakuta kuna *gest houses* sio za ghorofa lakini ni kubwa zina vyumba karibu 20 – 30 na wenyewe walipe hiyo *property tax* 10,000? Naomba waifafanue vizuri watumie wataalam wapo, tupo wataalam.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, niongezee kwenye hiyo *property tax*. *Property tax* pia ninavyojua mtalaam inalipwa mijini sheria ile ipo, waitazame ile sheria. Sheria hii tunaita *Local Authority (Rating) Act, 1983* inasema ni mijini. Sasa mnaposema *property tax* iende mpaka vijijini sijaelewa na imetoa *category* ya nyumba sio ya tembe iwe nyumba ambayo angalau ya bati kwa mijini, sasa sijaelewa kama *property tax* tunaenda kuwatoza mpaka vijijini kule kwenye vijumba vya Wagogo vile vya tembe, sijafahamu.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi na watumie wataalam zaidi pia, kwenye *flat rate* hiyo lakini na kwenye *category* ya majengo. Hata ghorofa nayo ina *category* zake, unakuta ghorofa ina vyumba vingi sana, kuna *flat* za kuishi kuna maghorofa ya biashara sasa ghorofa ipi ambayo itaingia kwenye *flat rate* kwamba ilipe 50,000; tutapoteza mapato mengi hapa lakini pia tutawaonea watu wengi hapa, naomba waifafanue sana watumie wataalam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja na naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, asimame na msimamo ule ule, nchi hii sasa twende mbele.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtuka. Mheshimiwa Mbaraka Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza. Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mbunge wa Mafia.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili nami nichangie hotuba hii muhimu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mwaka jana wakati nachangia hotuba hii ya bajeti nilisema hawa Madaktari wawili wa Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu, kama tutawapa *support* watatufikisha mbali

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

sana, wengi hawakunielewa, lakini kutokana na uwasilishaji huu wa hii bajeti ambayo wengi wanaita bajeti ya karne nadhani yale niliyoyasema mwaka jana yamethibitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana wakati Mtemi Chenge anaahirisha Bunge, alitoa maangalizo mazuri sana, kwamba jamani hii bajeti haya ni mapendekezo, sisi tunatakiwa tutie nyama, tutoe maoni yetu. Sasa mimi nina machache ya kujazia kwenye bajeti hii nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato, mimi natokea Mafia, kule Mafia tunavyo vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa mapato ambao kwa mitazamo yetu tuliopo Mafia kule tunaona kwamba Serikali inapoteza mapato mengi sana. Tuna taasisi kule, inaitwa Taasisi ya Hifadhi ya Bahari hawa kazi yao kubwa ni uhifadhi wa bahari, lakini wamejiingiza katika masuala ya ukusanyaji wa tozo.

Mheshimiwa Spika, tungeomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango na kupitia Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) wakichukue hiki chanzo, wawaagize *TRA* Mafia waanze kukusanya ile *entry fees* ya watalii wanaoingia katika maeneo ya hifadhi, tunawabebesha mzigo watu wa hifadhi ya bahari ambao si wao, kwa sababu wao wanatakiwa washughulike na hifadhi. Haya mambo ya kukusanya mapato yana wataalam na wataalam wa *TRA* wapo pale, Ofisi ya *TRA* ipo pale Mafia.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri achukue haya maoni na amwagize Kamishina wa *TRA* amwaagize Meneja wa *TRA* pale Mafia, waanze kukusanya mapato yale kutokana na watalii. Hawa watu yale mapato wanashindwa hawana *capacity*, hawana uzoefu, hawana wataalam, matokeo yake pale tunakadiria kupata karibuni bilioni mbili kwa mwaka lakini wao wanakuja kutuambia kwamba tumepata milioni 700 milioni 600.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza sana wanayatumia vibaya, wanarundika mle gharama za

uendeshaji nyingi sana, likizo yao yamo humo, safari zao zimo humo, makongamano yamo humo na mambo chungu nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi haya mapato mwisho wa siku Halmashauri ya Mafia inatakiwa ipate asilimia 10. Sasa wenzetu wanavyorundika haya matumizi wanasema kwamba asilimia 10 hiyo baada ya kutoa gharama zote. Sasa gharama wanarundika mambo chungu mzima. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie aagize Mamlaka ya Mapato waanze kufanya kazi hiyo ya kukusanya mapato katika *entry fees* ya watalii kule Mafia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linaweza likatusaidia sana kwa mapato limesemwa hapa asubuhi na Mheshimiwa Zaynab Vulu umefika wakati sasa tufungue hii *Southern Circuit* ya utalii kwani kuna fursa kubwa sana za utalii. Kama nilivyotangulia kusema mimi natokea Mafia, Mafia kuna fursa kubwa sana za kiutalii ikiwemo yule samaki anayeitwa potwe ambaye ni samaki maarufu sana duniani na anapatikana Mafia na Australia tu, lakini kwa bahati mbaya sana hatujaanza kumtangaza vizuri na watalii wengi wanakuja pale. Naomba sana Serikali ituangalie, tutangaze vivutio hivi, lakini sio tu kutangaza vilevile kuna tatizo la *accessibility* ya kuingia Mafia. Hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, usafiri wa kuingia Mafia ni mgumu, sasa hawa watalii watapita wapi, hatuwezi kila mtalii apande ndege afike Mafia, lazima wapite njia ya bahari, lakini njia ya bahari kwa bahati mbaya sana kuna matatizo, hakuna boti za kisasa, kuna magogo yale. Kwa hiyo tungeomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Ujenzi watusaidie sana pale Mafia kutupatia boti ya kisasa ambayo watalii wanaweza kuja, bahati nzuri Naibu Waziri wa Ujenzi Mzee Ngonyani nimemwona hapa, watupatie boti ya kisasa ili tuweze kufungua ile fursa ili watalii waje kwa wingi na wasafiri vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika hilo kwa kuwa Mheshimiwa



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Ngonyani nime mwona suala la Gati la Nyamisati, Gati ya Nyamisati mwaka jana zilitengwa pesa hapa na nilitoa angalizo jamani hizi pesa ziende zikafanye hiyo kazi, tumebakiwa na wiki hazizidi mbili mwaka wa fedha unakwisha pesa zilitengwa, gati halijaanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana ndugu zetu wa Wizara ya Ujenzi...

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mafia nasikia kuna taarifa fulani. Ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hao *whale-sharks* hawapatikani tu Mafia na Australia bali wanapatikana nchi zote ambazo ni za tropikia au yale maji ambayo yana umoto moto kidogo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dau nataka kukwambia tu huyo ni Dkt. Semesi na mama yake ndiye alikuwa bingwa wa masuala ya elimu ya bahari pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Endelea Mheshimiwa Dau kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, kuna tofauti kati ya Potwe *whale-sharks* na *dolphins*, kama yeye anazungumzia *dolphins* wanapatikana maeneo hayo aliyoyasema. Mimi namzungumzia *whale-shark* - potwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa watufungulie njia ya usafiri kwa upande wa Mafia, gati lile pesa zilitengwa, lakini mwaka unakwisha ujenzi haujaanza, tunaingia mwaka mwingine. Naomba sana Mheshimiwa

Waziri zile pesa zisiwe kama tena zimepotea, tutakapoingia mwaka mwingine wa fedha ule mchakato wa kujenga lile Gati la Nyamisati na kufungua fursa za utalii pale, ziweze kufikiriwa.

Mheshimiwa Spika, lingine suala la utalii kwa upande wa Mafia tulikuwa na Hoteli pale na ndugu yangu Mheshimiwa Maghembe anaifahamu. Hoteli ile ya Chole Mjini, ilifungwa kutokana na matatizo ya uendeshaji wa yule mmiliki pale. Kwa kiasi kikubwa sana yale matatizo yameshakwisha, pale ni chanzo kikubwa sana cha mapato. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI wakishirikiana kwa pamoja watufanyie utaratibu hoteli ile ifunguliwe ili Serikali isiendelee kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji watalii na utalii wa Mafia zaidi ni wa *scuba diving, sport fishing* na vitu kama hivyo. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho hapa, aligusie hilo na kwa kushirikiana na Wizara hizi nilizotitaja ili tuweze kufungua fursa za utalii pale Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii pia unakwenda sambamba na miundombinu iliyo bora, barabara ya kutoka Kilindoni kwenda Rasi Mkumbi kilometa 55 na Mheshimiwa Waziri alizungumza kwa uchungu sana tunakwenda kubana matumizi, bajeti hii ni ya kubana matumizi. Nilizungumza wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mbarawa kwamba kule Mafia kuna tatizo, kile ni kisiwa kuna udongo ambao unakwisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbaraka Dau, muda wako.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge wa Mafia. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Calist Komu.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Serikali. Kama walivyosema wenzangu bajeti ya mwaka huu kwa kweli ni bajeti ya kimapinduzi, (*transformation*) imeelekeza nguvu zote kuwasaidia wanyonge wakiwemo wakulima ambao ni wengi katika Tanzania yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii kodi za mitaji zimesamehewa (*Capital goods budget*), kodi imeondolewa ya kuondoa kodi ya thamani ya usafirishaji (*ancillary transport services*), kodi ya maeneo ya ufugaji nayo imeondolewa na kuwapa unafuu sana wakulima wetu huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, vilevile kufutwa kwa *road licence* kwa kweli hii kodi ilikuwa ni kero, ilikuwa haitusaidii kabisa. Nina imani kuwa hii kodi mapato yake ukilinganisha na gharama zilizokuwa zinatumika zilikuwa haziendani sawa sawa. Nashukuru baada ya kuisoma vizuri bajeti hii kuwa ongezeko la Sh.40/= linaongezwa kwenye pato, hii sio mbadala wa *road license*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeilewa vizuri sana kwa sababu hata ile *notion* ya kwamba hii inakwenda kuwaumiza wakulima kwa sababu wanalipia *road license*. *Road license* imefutwa kama inasomeka vizuri kwenye bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa reli kwa *standard gauge*, hayo ni mapinduzi makubwa sana ya kiuchumi. Vilevile mpango wa kujenga reli kutoka Tanga mpaka Musoma, hayo ni mapinduzi makubwa sana katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bomba la mafuta toka Uganda kwenda Tanga kwa kweli hayo ni mapinduzi makubwa sana. Pamoja na hayo tusisahau vilevile kwamba hizi *investments*

tulizokuwa nazo kama TAZARA, bomba la mafuta kwenda Zambia nazo ziboreshwe kuhakikisha zinafufuliwa na zinafanya kazi inavyotakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa makusudi kwa sababu punguzo la mbolea litawapa nafuu sana wakulima, lakini tusipoboresha usafirishaji hilo punguzo wakulima hawataliona, kwa sababu kodi nyingi zimeondolewa katika mbolea. Hata hivyo, ukiangalia *value chain* ya mbolea kutoka huko tunakoagiza nje asilimia 53 ni CIF ambayo ni gharama ya kununua mpaka bandarini lakini asilimia 47 ni ya kumplekekea mkulima, bila kuipunguza hiyo kwa kweli wakulima wetu hawataona huo unafuu. Kwa hiyo naiomba sana Serikali ijaribu kuelekeza ni namna gani tuondoe urasimu pale bandarini, ni namna gani tuboresha TAZARA, reli ya kati ili mbolea zote zisafirishwe kwa reli na hiyo italeta ushindani mzuri kwa mazao yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya kilimo kwa asilimia kubwa sana, Mbeya tunalima pareto. Pareto ni zao ambalo linatumika kutengeneza sumu, madawa kwa ajili ya kuulia wadudu, inatokana na maua, halihitaji mbolea. Hili zao kwa sasa hivi lina soko kubwa mno, tunazalisha tani 2000 lakini mahitaji sasa hivi ni karibu tani 10,000. Kwa kuangalia hili zao linaweza kutuletea *foreign exchange* kama tutapeleka nguvu huko, nguvu tunayoihitaji ni kidogo hatuhitaji kuongeza bajeti, tunachotakiwa kuongeza hapo ni usimamizi wa kumsaidia mkulima kwenye masuala ya masoko.

Mheshimiwa Spika, leo hii wakulima wanalima pareto lakini soko limekuwa *dominated* na mtu mmoja, wengine wanapokuja wananyimwa nafasi ya kwenda kununua. Mwaka huu Bodi ya Pareto hata ule mkutano wa wadau wameahirisha, hatujui mkutano utakuwa lini kwa sababu ule ndio tulikuwa tunaangalia changamoto nyingi za hili zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, zao letu lingine la kahawa halifanyi vizuri ukilinganisha bei za Tanzania na bei za majirani zetu Kenya. Wote tunalima kahawa aina ya Arabica, Kenya

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

inalimwa huku kwa wenzetu Kilimanjaro na Mbeya lakini kwa Nairobi *coffee exchange* bei ya sasa hivi ni dola 300 kwa kilo 50, kwa sisi ni chini ya dola 150. Sasa hii yote hii inatokana na nini, kwa nini kahawa ile ile na wanunuzi ni wale wale, kahawa ya kwetu Tanzania bei iwe chini? Inanikumbusha kwamba matatizo tuliyonayo kwenye madini ni yale yale matatizo waliyonayo wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie ni namna gani tutawasaidia wakulima ili tuwe na masoko ya uhakika ya kipindi chote ikiwemo masoko ya kahawa, pareto, viazi, ndizi, ndizi zetu kule Mbeya zinabebwa na magari kupelekwa nchi jirani *for export* na hata siku moja hutaona kwenye kumbukumbu zetu kuwa tuna *export* ndizi. Sasa yote haya tukiboresha masoko yetu nafikiri nchi yetu itapata *forex* nyingi kutokana na kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa tozo za mazao ya kilimo. Nashukuru sana kwa kweli kuna unafuu wa wakulima lakini je, hili punguzo la tozo tutazisaidia vipi Halmashauri kwa vile zilikuwa zimejumuishwa kwenye bajeti za Halmashauri. Kwa Halmashauri ya Mbeya mapato tunategemea zaidi kwenye kilimo na tunapata karibu nusu bilioni na hii nusu bilioni yote kama nilivyokuwa naiangalia leo kwenye bajeti ni kwamba hiyo imeenda na hiyo ni karibu asilimia 50 ya bajeti ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tusipoyakusanya hayo mapato Halmashauri itawajibika na kuadhibiwa. Sasa labda ningepomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha hayo mapato ambayo yameondolewa kwenye Halmashauri yatafidiwa vipi ili Halmashauri zetu ziendelee kufanya kazi kama kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilimo bila miundombinu mizuri kwa kweli hatuwezi kufanikiwa, naomba sana kuboresha miundombinu vijijini ikiwemo umaliziaji wa ujenzi wa kiwanja cha Songwe, ambacho mpaka leo hakina taa za kuongozea ndege na hakuna wigo kwa usalama wa uwanja...

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana.

Kabla ya Mheshimiwa Komu kupata nafasi niwatangazieni tu Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, baada ya saa 12 tutakakapoahirisha hapa, ndugu zetu wa Tanzania *Media Foundation* wameandaa futari kwenye eneo letu la kawaida nyuma ya jengo la Utawala pale, ambayo mnaalikwa Wabunge wote kuweza kufika pale na kushirikiana na wenzetu katika futari hiyo. Nitawakumbusha tena mwishoni lakini niwahi wahi ili wanaotaka kuwahi futari huko wajue ipo, imeandaliwa na ni ya nguvu kweli kweli.

Pia niwaombe Wajumbe wa Kamati ya Uongozi itakapofika saa 11 kamili basi mkutane tena kwenye chumba chenu kile kile ili muweze kumaliza mazungumzo yenu ambayo mlikuwa mmekubaliana kwamba mtakutana tena saa 11 kamili.

Tunaendelea na Mheshimiwa Anthony Calist Komu, Mbunge wa Moshi vijijini.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika mjadala huu ambao ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono maoni yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani na niombe sana Serikali kwamba mara nyingi ukitaka kwenda vizuri ni vizuri ukajiangalia kwenye kioo. Sasa haya maoni yaliyotolewa hapa kama Serikali ikiamua kujiangalia kwamba upande wa pili wanaonaje, inaweza

ikasaidia sana na ikawa na mchango mkubwa na tukakwepa kwepa haya mambo ambayo jinsi tunavyokwenda mbele tunaendelea kuumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli napata shida sana Wabunge wenzangu ambao wanawakilisha Watanzania ambao tunajua hali zao wanavyosema kwamba hii bajeti ni bajeti ya aina yake, ni bajeti nzuri. Kwa sababu nikianza kwenye kuangalia vipaumbele, nashangaa kabisa kwamba tunavyoweka ndege katika nchi hii kama kipaumbele sijui tunatumia vigezo gani, kwa sababu ukienda kwenye huu Mpango wa Maendeleo wa Taifa ukurasa wa Nane kuna uchambuzi umefanyika pale unaoonesha *key sector* katika pato la Taifa, hakuna ndege na katika michango yote hakuna ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mpango anafahamu kwamba unapotaka kuwekeza kwenye kitu chochote ni lazima uende kwenye kuangalia ni wapi utapata matokeo makubwa *(comparative advantage)*. Sasa inavyoamuliwa kwamba tukawekeze ndege wakati huu shilingi karibu trilioni moja, kwa sababu tumeshanunua ndege mbili, tumetenga billioni 500, tunachukua madeni yote ya ATCL na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye hili jedwali ambalo nimelirejea, mchango wa kilimo ni asilimia 29 kwenye pato la Taifa. Hata hivyo, ukienda kuangalia leo kwenye bajeti ya kilimo cha umwagiliaji tumetenga billioni 24, tena hizo billioni 24 bilioni 15 zinatoka nje, za kwetu tulizotenga ni bilioni tano. Leo hii tunanunua chakula kutoka nje ya nchi, ukienda kuangalia *imports* za nchi hii asilimia tisa ni chakula, tunawezaje kupiga hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa kama tunakwenda kuweka pesa nyingi namna hiyo na tunasema na tunakaa hapa kweli tunajivuna kwa sababu najaribu ku-*recall* Mzee wangu rafiki yangu sana Mheshimiwa Keissy siku moja hapa Mheshimiwa Heche alisema anataka kiwanja Tarime, Keissy

akasimama akasema kule kwao wanataka barabara tena za changarawe, leo hii tunakuja hapa tunapiga makofi kwamba eti ndege ni kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kuangalia *competency* yetu kwa maana ya soko la ndani sioni, ukienda kuangalia *competency* yetu Kimataifa kwa maana ya kushindana na kupata faida, sioni, hatuna *economies of scale*, hatuna ukubwa wa kuweza kushindana na ikawa ni faida. Kwa hiyo, suala la biashara ya ndege *is a high risk business*, ndio maana watu wanakwendaga kukopa sio kulipa *cash*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri kwamba huu ni mkenge ambao tumeamua kuuvaa na nafikiri kama tunawakilisha kweli Watanzania ambao siamini kama wanafika hata 10,000 ambao wanaweza wakawa na manufaa na hiyo ndege. Nafikiri tungesimama kama Bunge tukasema kwa kweli huu uwekezaji wa aina hii tumepotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye hoja yangu ya pili, nikienda kwenye hoja yangu ya pili...

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Komu kuna Taarifa naomba uipokee, Mheshimiwa Magolyo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba katika *record* za Serikali hivi sasa, Sekta ya Utalii inaongoza kwa kuingiza fedha za kigeni. Kwa *record* za mwaka jana tulingiza zaidi dola za Kimarekani billioni mbili na katika fedha hizi zaidi ya asilimia 60 zinatumiwa katika eneo la usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ili Watanzania waweze kunufaika na sekta hii vizuri Serikali na ilishauriwa na nadhani ni jambo la muhimu kulitazama kwamba ni namna gani inaji-*position* ili iweze kuchukua *this big chunk* inayochukuliwa na makampuni ya nje ya usafirishaji wa abiria



ambao ni Watalii. Nataka tu kumkumbusha hilo kwamba Sekta ya Utalii ni muhimu na inahitaji sana usafiri wa anga (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Komu unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu haina ukweli wowote kutokana na rejea mbalimbali ambazo ziko mbele yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili ni kwamba, bajeti hii ukiangalia kwa makini ina asilimia kubwa sana ya kubahatisha, asilimia kubwa sana ya kupiga kamari. Kwa sababu tuna pesa ambazo tumesema trilionini 7.7 tunakwenda kukopa tena ndani kwa kiasi kikubwa, tuna trilionini 3.9 ambazo tunatarajia tupate kutoka nje ya nchi kwa maana ya misaada kwa maana ya mikopo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukweli na uhakika wa kupata fedha hizi ni mdogo sana, bado tuna tatizo la Zanzibar ambalo linatuletea matatizo. Kwa hiyo, nafikiri tukitaka kuwa *realistic* bado tuna kazi kubwa ya kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga. Ukiangalia kwa kauli ya Waziri mwenyewe anasema huu ndio msingi mkuu wa kuchochea mageuzi ya viwanda katika nchi hii lakini ukienda kuangalia wanasema kila kitu kimekamili, ukienda kujaribu kusoma katika Wizara zote unaona kwamba tatizo lililopo sasa hivi ni Serikali yenyewe haijatoa *GN, are we serious?*

Mheshimiwa Spika, kweli tuko *serious* kwamba tunataka kwenda kwenye mageuzi ya viwanda katika *speed* ya namna hiyo, wanasema mwekezaji amekwisha patikana na ameshatenga pesa, lakini Baraza la Mawaziri lilikaa mwaka jana likaamua kwamba wakaipitie upya na kuona vivutio vile vilivyopo vina maslahi gani kwa Taifa. Ni jambo zuri lakini huoni kwamba hiyo ni ndoto katika hali ambayo

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

unasema unaye mbia lakini hujampa *package* ya *incentives*, maana yake utakapokuja kutoa hizo *incentives* anaweza aka-*withdraw*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni hili linaloendelea la mchanga, naomba niungane na wote wanaosema kama Rais yuko *serious* na kwa kweli vita hii haikuanza leo, mnakumbuka kulikuwepo na Kamati ya Dkt. Chipokola ya mwaka 2004 na ukienda kuisoma haina tofauti na mambo ya Osoro ya jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na Kamati ya Lawrence Masha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa nataarifiwa hapa kwamba muda wako umekwisha...(*Kicheko*)

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja na naomba ile kinga ya Marais waliotangulia iondolewe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Kapufi!

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote nami naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kufuatilia vipaumbele vilivyotolewa na Mheshimiwa Waziri, kwa maana ya utekelezaji wa vipaumbele eneo la ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi upande wa barabara, reli, usafiri wa anga, majini na umeme. Ukweli ni kwamba eneo hilo barabara, reli, usafiri wa anga, usafiri wa majini na umeme vikifanyiwa kazi tutafika sehemu, kama hiyo haitoshi eneo lile la pili naambiwa

kwamba kipaumbele kingine ilikuwa ni kuhakikisha madini na maliasili zetu zinatumika kwa manufaa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mimi nina maslahi katika eneo la uchimbaji wa madini. Naomba nijikite kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa 32, inaelezea kutoza kodi ya zuio ya asilimia tano ya bei ya kuuzia kwa wachimbaji wadogo ni hatua inayoongeza mapato stahiki ya Serikali...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapufi, kwa kuwa umetutaarifu kuwa una maslahi kwenye eneo hili, unasema ni maslahi ya aina gani halafu unaendelea kuchangia.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa ule kwa maana ya Taarifa ya Kamati inasema hivi: *“Kutoza kodi ya zuio ya asilimia tano ya bei ya kuuzia kwa wachimbaji wadogo ni hatua inayoongeza mapato stahiki ya Serikali, lakini inatafsiriwa kuwa wachimbaji wadogo watalipa mrabaha kwa asilimia tisa na inaweza kusababisha wachimbaji wadogo kufanya biashara haramu.”*

Mheshimiwa Spika, lengo langu ni nini? Ikiwa tumekusudia kuwasaidia wachimbaji wadogo na ambacho nakiona sasa hivi, mkakati mkubwa wa Serikali kutoa ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo, lakini kwa kupitia vyombo vyake kama GST kufanya utafiti ili wachimbaji hawa waende kuchimba katika maeneo yenye tija. Sasa hayo yote ambayo ni nia njema ya Serikali kuyafanya, inapokuja suala la mrabaha kuwa kubwa kwa kiasi hicho, mimi napata tabu.

Mheshimiwa Spika, mchimbaji huyu mdogo na naomba Bunge lako lifahamu ningependa Waziri angeenda hata kwenye tafsiri, tunapozungumzia mchimbaji mdogo ni yupi? Maana mchimbaji mdogo ninayemfahamu mimi hana tofauti na Mmachinga mwingine wa kawaida. Mchimbaji mdogo ambaye anaweza akaenda porini ndani ya miezi mitatu hajapata hata *gram* moja ya dhahabu, huyo ndiye

mchimbaji mdogo ninayemfahamu. Mchimbaji mdogo anayetumia sururu na nyundo, labda kama tunamzungumzia mnunujaji wa madini, lakini kwa maana ya mchimbaji mdogo na Serikali hii imelenga kumsaidia mchimbaji huyo mdogo.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia habari ya mrabaha kwenda karibu asilimia tisa napata shida na ukizingatia leseni ya hekta moja ni 80,000, kama atakuwa na hekta kumi, maana yake ni laki nane ada ya leseni! Kwa hiyo eneo hilo naomba tuliangalie. Nalisema hilo kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa nafuatilia taarifa ya mtaalam mmoja, ameitaja Botswana na uchimbaji wa *diamonds* kwa maana ya almasi. Botswana sasa hivi pato la Botswana linatushinda Tanzania lakini wamejikita kwenye uchimbaji wa almasi tu. Nchi yangu nzuri Tanzania, mikakati mikubwa na katika hili nimshukuru Mheshimiwa Rais jitihada anazozifanya katika maeneo yote hayo yanayogusa machimbo, lakini niendeleo kusema; ili tukafanane na watu kama Botswana, jitihada hizi za makusudi ziendeleo kulenga maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Spika, tunapomzungumzia mchimbaji mdogo akiwezesha vizuri makandokando mengine yakakaa pembeni mimi ninachofahamu uwekezaji wake haufanyi nje ya nchi, ataufanya Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija kwangu Katavi, majengo mengi mazuri ni yale yaliyofanywa na wachimbaji wadogo. Biashara nyingi kubwa ni zile zinazofanywa na wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu tuendeleo kuliangalia eneo hilo kwa umakini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufungwa kwa biashara. Kutoka Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kuna biashara 7,277 zilifungwa. Nafarijika kwa maana ya taarifa ya Waziri imejikita kwenye kutafuta kujua na jitihada zifanyike ni kwa nini biashara hizo zilifungwa ingawa upande wa pili ametuambia kuna zaidi ya biashara 224,738 ambazo ni mpya. Kubwa ambalo

ningependa kuendelea kushauri, ndugu zetu wa *TRA* na wafanyabiashara tuendeleo kutengeneza mahusiano sio uadui. Katika hili, Mheshimiwa Waziri nashukuru pale aliposema wenzetu wa *TRA* waendeleo kufanya mahusiano shirikishi na wenzetu wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la usambazaji maji vijijini na mijini. Naona Mheshimiwa Waziri ametenga bilioni 188.4. Katika eneo hili niendeleo kusema, pamoja na jitihada za Serikali kule kwangu kwa maana ya suala la maji na kila mtu hapa ameongelea suala la maji. Naomba Mheshimiwa Waziri, ufumbuzi wa muda mrefu, tuwekeze fedha kwenye kuyatoa maji ziwa Tanganyika, hiki ni chanzo cha uhakika, watu watapata maji ya kutosha na kelele hizi zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu dawa na vifaa tiba ambapo niliona pale inazungumziwa habari ya bilioni 156.1. Tuseme yote tutakayoweza kusema na nishukuru pamoja na kwamba tunakwenda kusaidia hospitali kwa maana ya Jakaya Kikwete na maeneo mengine hayo, lakini tusipowekeza kwenye hospitali zetu za mkoa kwa maana ya vifaa tiba na madawa kasi ya watu kutoka huku mikoani kwenda kuvamia huko kwenye hospitali hizo nyingine itakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, naliona hilo kwa sababu gani? Kwa mfano, kule kwangu Katavi japo hospitali ile ya mkoa haijajengwa, utengaji wa fedha wa bilioni moja kwa kila mwaka kama lengo kweli tunataka tuhakikishe eneo hili la tiba watu wetu wanapata huko huko, maana yake hospitali ya mkoa ikiimarishwa, ikiwa na vifaa vyote, umerahisisha kazi, watu hawatakuja katika hizo hospitali nyingine kama Muhimbili na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nami niungane mkono na wale wote kuhusu kusamehe kodi eneo la ufugaji pamoja na vyakula vya mifugo. Tutaiona tija katika eneo hilo, eneo la mifugo na kwa kweli tunasema ili mambo mengine yote yakae vizuri, tukiweza kukusanya mapato ya

kutosha, maeneo mengine yote hayo yatakaa vizuri. Kwa hiyo, hapa tuliposamehe kodi katika eneo hilo la ufugaji pamoja na vyakula vya mifugo, naliona hilo limekaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ujenzi wa reli ya kati kwa maana ya kiwango cha *standard gauge*...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kama nilivyosema mwanzo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi, mchimbaji mdogo. Mheshimiwa Moshi Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein wa *CUF*.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii. Awali ya yote niipongeze Serikali kwa kazi nzuri sana ya kuleta bajeti hii ili iweze kuwa ya mfano na kusaidia wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa sababu imekuja na mpango mzuri. Niwapongeze Kamati ya Bajeti kwa kuja na mapendekezo mazuri ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo nataka kuzungumzia ni suala zima la Serikali kuja na mpango wa kujenga au kuanza uchimbaji makaa ya mawe na chuma Mkoani Njombe. Eneo hili litakuza uchumi mkubwa sana kwa Serikali ya nchi yetu na itafanya maeneo haya ya ukanda wa kusini na Serikali kwa ujumla kuwa na kipato kizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunaishauri Serikali iwekeze kwa nguvu zote ni ujenzi wa reli ya kati. Ujenzi wa reli ya kati ni suluhisho kwa wananchi wa maeneo karibu yote ya nchi hii. Asilimia kubwa wananchi wa kada ya chini

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wanatumia sana usafiri wa reli. Kwenye maendeleo, tukiboresha eneo la ujenzi wa reli ya kati tutakuwa tumesaidia sana wananchi wa maeneo ya nchi hii. Siyo tu kwa maeneo ya Dar es Salaam, lakini tutakuwa tumetengeneza uchumi wa Mikoa mingi kuanzia Dar es Salaam mpaka Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, sambamba na tawi la reli la kutoka Tabora kwenda Mwanza, naamini uchumi kwenye maeneo hayo na maisha bora kwa kila Mtanzania yanaweza kupatikana kwa kiwango kikubwa sana. Niiombe sasa Serikali kwenye bajeti hii iwekeze nguvu kubwa sana kwa ajili ya kuimarisha ujenzi wa reli ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna maboresho ambayo yamefanyika, maboresho ya Shirika la Ndege, ujenzi wa mitambo ya gesi, ni maendeleo ambayo yanategemewa sasa kwa Serikali yanaweza yakatoa suluhisho kubwa na kupata mapato makubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo ningependa kushauri Serikali ni kuachana na uwakala wa kukusanya kodi ya nchi ya Congo. Eneo hili tunapoteza mapato makubwa sana. Ni vema Serikali ikaangalia ule mkataba ambao tumewekeana na Congo, hauna manufaa kwetu sisi. Karibu wafanyabiashara wengi wa nchi ya *DRC* wamehama kutumia Bandari ya Dar es Salaam, kwa hiyo ni vizuri kwenye maeneo haya wakatazama upya ili kuweza kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nina ushauri kwa Serikali. Ni vizuri sasa Serikali ikaangalia upya, nchi ya Zambia ni miongoni mwa nchi inayotegemea sana Bandari ya Dar es Salaam lakini bahati mbaya Zambia wanalipa ada tofauti na nchi zingine. Ni Vizuri Waziri wa Fedha akakaa na wenzetu wa Zambia wakaangalia zile tofauti ambazo zipo wakazitoa ili wenzetu waweze kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo

ningependa kuzungumzia sana ni kwenye sekta ya kilimo, kwenye sekta ya kilimo, ni eneo pekee ambalo tukiwaboresha wakulima wa nchi hii watakuwa na nafasi ya kutoa mchango mkubwa sana wa pato la Taifa. Tunaomba sana Serikali iangalie kuweka mazingira mazuri yatakayowasaidia wananchi kupata pembejeo zenye bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapowawezesha wakulima, tumewawezesha wananchi karibu wote wa nchi yetu. Ni vema sasa Serikali ikaja na mkakati wa kusaidia hawa wakulima wadogo, wavuvi na wafugaji ili iweze kuwawekea mazingira ambayo yatakuwa rafiki kwenye uzalishaji kwa gharama nafuu na kuwawekea miundombinu ambayo itawasaidia sana katika kuboresha shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ili nchi iweze kwenda vizuri Serikali sasa iangalie uwezekano wa kuweza kusaidia wakulima wakubwa. Ni vema tukaangalia hata Taasisi za Serikali tulizonazo, tukawekeza kwenye Jeshi la Magezea, Jeshi la JKT, tukawawezesha waweze kuzalisha kilimo kikubwa, wakalima mashamba makubwa ambayo kimsingi kwanza yatatatua tatizo la njaa, lakini bado watakuwa na ziada ya kuweza kuzalisha hata kuuza nchi za nje na kuleta pato la Taifa. Kwenye eneo hili tukifanya vizuri tutakuwa tumewasaidia sana Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine naishauri Serikali, dhamira ya Serikali ni kupeleka umeme vijijini. Naomba Serikali sasa ipeleke umeme vijijini na iangalie maeneo yote ya nchi. Tusije tukawa na maeneo ambayo mengine yananufaika na sehemu nyingine hakuna. Ni vizuri umeme vijijini ukapelekwa kwenye maeneo yote hasa kwenye mikoa ile ambayo iko pembezoni. Nafurahi Mheshimiwa Waziri wa Fedha na yeye ametoka kwenye maeneo ya pembezoni, anajua mazingira jinsi yalivyo. Naomba sana Serikali iweze kuangalia maeneo hayo ili iweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara. Nchi yetu



ilikuwa na dhamira ya dhati kuhakikisha Mikoa yote inaunganishwa. Namwomba sana Waziri wa Fedha aangalie sasa uwezekano wa kuunganisha mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami. Mkoa wa Rukwa uunganishwe na Katavi, Mkoa wa Katavi na Kigoma, Mkoa wa Tabora na Kigoma, Mkoa wa Katavi na Tabora. Tunahitaji maeneo yote hayo yaweze kuunganishwa ili yaweze kutoa mchango mzuri kwa pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya maeneo yalisahaulika. Kwenye bajeti hii tunaomba sasa dhamira ile ya Serikali iweze kuonekana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anajua mazingira yalivyo na anakotoka. Tayari Mkoa wa Kigoma hauna mawasiliano na Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kigoma hauna barabara za lami na Mkoa wa Katavi; Mkoa wa Kigoma bado hauna mawasiliano na Mkoa wa Tabora sambamba na Katavi na Tabora. Tunaomba ile miradi iliyopangwa iweze kusimamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nisisitize zaidi huduma ya maji vijijini. Tunaomba sana, fedha ambazo zinapatikana kwa michango ambayo tutaichangia hasa ile Sh.40/=, tuiielekeze iende kutatua tatizo la maji. Katika maeneo haya tutakuwa tumewasaidia sana wananchi hasa akinamama walio wengi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba na kuishauri Serikali iangalie mazingira haya kuyaboresha na tupeleke hii miradi iweze kwenda kuwasaidia wananchi kwenye maeneo hayo ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji kwani bila kuwa na maji uwezekano wa kupata nafuu ya kuzalisha ni mdogo sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Immaculate Semesi Sware.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** *Bismillah Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kabla sijaanza nina maombi, naomba uniongezee dakika kumi ili nitoe somo leo humu Bungeni. Pili, nakusudia kusema ukweli ili tuondoke hapa tulipo twende mbele na ukweli unauma kwa hiyo nakuomba univumilie na Wabunge wa pande zote wanivumilie. Kama umeniruhusu uniambie ili nijue najipanga vipi katika hoja zangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Wabunge kwanza tuache ushabiki wa kufuata ngoma. Naomba mnisikilize vizuri nitakayoyasema. Kama nchi yetu inapita katika kipindi kigumu au ilishawahi kupita, nchi yetu sasa hivi inapita katika kipindi kigumu sana. Vita hii ambayo Rais John Pombe Magufuli anaendelea nayo ni vita moja ngumu sana na yeye peke yake kama yeye hawezi kufaulu katika vita hii ni lazima Watanzania tushirikiane tukiwa kama Watanzania na siyo CCM, Wapinzani au nani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vita hii ni kubwa kwa sababu ni vita ambayo imekamatana na kitu ambacho ni fitna, kitu ambacho ni mali/fedha. Kwa hiyo hii ni vita moja kubwa sana ambayo ni lazima kama Watanzania tukae pamoja, Waheshimiwa ni lazima tuondoe tofauti zetu. Suala la wana CCM kutuona sisi Wapinzani kama maadui au wakoloni tunaotoka nchi nyingine tunataka kuitawala Tanzania halitatufikisha. Suala la sisi Wapinzani kuwaona CCM ni maadui, ni wezi, ni nani, ni nani halitatufikisha lazima tukawe kitu kimoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpasuko uliopo ndani ya nchi yetu hivi sasa kama hatujatumia busara, hekima na akili zetu, *wallah wabillahi wataalah* na hii Ramadhan, Tanzania ndiyo imefika mwisho wake hapa. Nayasema haya leo, wenye kuweka kumbukumbu waweke. Tulipo ni pabaya sana kuliko

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kipindi chochote kile ambacho nchi yetu imepitia. Vita hii ni ngumu na vita hii inahitaji umoja wa kweli kweli. Tufanye nini ili tutoke katika mkwamo huu tuliokwama? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima turejeshe umoja wa Kitaifa. Hatuwezi kuondokana na matatizo haya kwenye nchi hii lazima tukae pamoja kama Taifa, tuache kubaguana kwamba huyu Mpinzani, huyu Chama Tawala ana nguvu au ana hiki! Tukae pamoja tuweze kuweka mfumo mmoja wa Kitaifa, tuwe na *National vision*, tunataka nini kama Taifa ili Rais Magufuli leo vita hii anayoyoiendeleza najjuliza baada ya miaka kumi akiondoka anayekuja ataiendeleza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hakuendeleza anayekuja tutakuwa tumefanya nini? Leo anakamatwa Chenge, anakamatwa Ngeleja, anakamatwa mwingine tunawatoa kafara. Mheshimiwa yaliyotokea ni mfumo na lazima Chama cha Mapinduzi kikubali kubeba lawama hii, tufike mahali tusameheane, tufike mahali tukae pamoja, ndiyo kwa sababu Chama cha Mapinduzi ndio kinachoongoza dola. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima wakubali kubeba msalaba huu kwamba jamani tumekosea na tulipofika sasa tukae pamoja kama Taifa tuzungumze tuwe na mfumo mmoja wa Kitaifa ambao utatuondoa hapa tulipo kutupeleka mbele. Malumbano haya tunayoendelea nayo hatutafika hata siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpasuko huu, hawa wanaotajwa tajwa ni wanadamu, wanadamu, wana nyongo, wana fikra na wana watu nyuma yao, wanaumia, wanavumilia lakini ipo siku watasema, mwisho wa siku Taifa hili tutakuwa tunalipasua sisi wenyewe. Ni wakati sasa tukae pamoja kama Taifa, tuangalie tunataka nini katika kila sekta tuwe na *vision* tunataka nini.

Mheshimiwa Spika, leo akiwa Mheshimiwa Magufuli ndio Rais aende hapo atupeleke katika *vision* hiyo, kesho akija

Mlinga ndiyo Rais wa Tanzania atupeleke hapo, sitaki ushabiki nimesema Waheshimiwa, sio kwamba Mlinga amekuja anasema yeye kwa sababu ni mpenzi wa mpunga tunaondoka katika hapa leo tulime mpunga ili tusafirishe nje ya nchi, hapana! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tusiwe hivyo tuwe na *National Vision* ambayo kila Kiongozi anayekuja awe wa Chama Tawala, awe wa Upinzani anatupeleka hapo, tutakuwa tumeondokana na hili, vinginevyo narudia tena *Wallah wabillah watallah* vita hii hatutashinda na tutagawanyika na kama Taifa hili litatawanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa kuna fitna na mali ni fitna na hili Mwenyezi Mungu amesema hii ni fitna na tusipokuwa makini Taifa hapa ndio linafikia mwisho wake.

Mheshimiwa Spika, niseme hivi, namuunga mkono Mheshimiwa Rais Magufuli, katika vita hii na namuunga mkono kwa sababu ameamua kujitoa muhanga, nilikuwa nafikiri Rais Magufuli yupo katika zile sifa za unafiki lakini hayumo na ndio maana nikasema ni mfumo. Alipotoka kwa sababu kipindi kilichopita alikuwemo katika Baraza la Mawaziri, alikuwemo ndani ya Serikali na haya yote yanayotendeka leo yeye alikuwemo alisema? Alitakiwa aondoe kwa mkono wake wakati ule hathubutu, alitakiwa aseme hathubutu, lakini alichukia, leo amefika mahali anaweza kuondoa kwa mkono wake anaondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliopo hawa Mawaziri hawa tusidanganyane hakuna mmoja anayeweza kumwambia Rais hili usifanye, hakuna!

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Umeanza sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Victor Mwambalaswa nimekuona.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumpa taarifa msemaji anayeongea sasa hivi, kwamba kwa hoja nzito ambazo anazozijenga nitamletea debe la asali toka Chunya kesho. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa zawadi wakati wa mwezi wa Ramadhan inaruhusiwa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Eeh naam. Napokea sadaka hiyo kwa mikono miwili. Mwenyezi Mungu akujaze kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo ambao ulijengeka haumwezeshi Waziri yeyote aliyepita au Mwanasheria Mkuu au yoyote kuweza kumwambia Rais usifanye hili hayo ni makosa yametendeka na mwanadamu yeyote lazima afanye makosa ndio akawa binadamu, ambaye hafanyi makosa ni Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo niwaombe, niwaombe ndugu zangu wa CCM mbadilike, mkubali kwamba Taifa hili ni letu sote tukae pamoja tuseme nini *vision* ya Taifa katika kila idara, katika kila sekta ili tujenge nchi yetu kwa pamoja. Malumbano hayatatusaidia, nguvu zenu za dola hazitasaidia na hapa Taifa litagawanyika na tutagawana mbao kuanzia hapa.

Mheshimiwa nije hoja ya pili, Rais ana nia safi katika hili na kwamba...

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Nataka nimpongeze, nimpe taarifa tena awaambie pale wanaposema siyo, waseme siyo, kila kitu kinakuwa ndiyo, taarifa hiyo lazima uipokee. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa kwa sababu tatizo lililopo inapoletwa sheria hapa Bungeni, unapoletwa Muswada wowote hapa unakuja

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na maagizo, inatakiwa Wabunge waachwe huru, wawe huru kujadili, wawe huru kuishauri Serikali, yasiletwe maagizo kwamba *Caucus* ya CCM ikutane twendeni hivi, *Caucus* ya UKAWA ikutane twendeni hivi, tuwe huru kujadili mawazo, kujadili masuala ya Taifa letu, mhimili huu usiingiliwe, Rais abaki na Muhimili wake, atuache Wabunge tuweze kusaidia Taifa hili. Tukienda na tabia hii tutalimaliza Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, naenda kwa Mheshimiwa Waziri, nimwombe Mheshimiwa Rais *a-pause* kidogo huko kwenye madini, kwa sababu huu uchafu na uozo huu upo nchi nzima, katika Wizara zote na Idara yote na Taasisi zote. Baada ya pato ambalo litapatikana huko kwenye madini na sehemu nyingine, upotevu na wizi wa namna hiyo hizo fedha zikipatikana zinaenda wapi? Zitakwenda Hazina, Wizara ya Fedha huko ndio kumeoza ndio kwenye wizi ndio kwenye ubadhirifu mbaya kupita wote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri waanze hapa, nataka tuiangalie Benki Kuu kuna matatizo, sitaki kuingia kwenye mambo ya watu sana hapo. Ninachotaka kusema tu, tuiangalie ndoa ya Benki Kuu na *Bureau de Changes* kuna nini hapa? Pia tuangalie ndoa ya *TRA* na hawa watu wa *clearing and forwarding*, kuna upotevu mkubwa wa fedha katika eneo hilo, Mheshimiwa Waziri aangalie tusafishe hapo ili fedha yetu itakapotoka hapo sasa kwenye madini, kwenye uvuvi, kwenye maliasili, kwenye kilimo ikienda pale Hazina tuwe na uhakika fedha yetu ni salama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba univumilie nitapiga nikilegeza kidogo mshipa si msumari, lakini tunahitaji kuwa katika umoja huo ili tuondokane na hili tulilionalo. Naiomba Serikali kwa heshima zote, kwa heshima zote tuachane na kubaguana, tuachane na Rais leo kutuona sisi Wapinzani kama maadui, tukae pamoja tuweke mustakabali wa Taifa letu ili tuondoke hapa tulipo twende mbele.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye kuchangia na

kuelekeza Wizara katika mapato, suala la kukuza kilimo, ufugaji na uvuvi. Mheshimiwa Waziri amezungumza tu lakini hakueleza na ndio pale niliposema tunahitaji *vision*, je tunataka kukuza kilimo, lakini ni kilimo gani? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa nilitamani nikuongezee muda lakini siku nyingine nitakumbuka. Nilikutaja Mheshimiwa Dkt. Immaculate Semesi Sware, utafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika bajeti hii na nitajikita kwenye masuala makuu mawili ambayo ni kilimo na mambo ya mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimeamua kugusia kilimo kwa sababu nchi yetu bado ipo kwenye *category* ya kimaskini na karibu asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo na katika hao asilimia 70, asilimia 80 ni wanawake. Sasa kwa nini nimeamua kuchagua kilimo kwa sababu naona kwenye kitabu cha mpango cha Mheshimiwa Waziri 2016/2017 malengo hayakugusa kilimo wala hayakugusa mazingira. Katika kilimo aligusia tu shamba la miwa na kiwanda cha sukari ambacho kitaanzishwa huko Mkulazi, kitabu hicho hicho baadaye 2017/2018 hajagusia tena kilimo, lakini amegusia tena shamba hili hili la Mkulazi, mazingira pia haipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inashangaza kwamba hatuwezi kutoka kwenye huu umaskini katika nchi yetu, wenzetu mfano nchi ya Mexico ilikuwa maskini tena hata kuliko sisi nafikiri. Hata hivyo, mwaka 1940 waliamua kujikita kwenye kilimo na walichagua zao moja tu la ngano, sasa hivi Mexico ni nchi ya 13 duniani kwa utajiri na ni nchi ya 11 duniani yenye uwezo ya kununua bidhaa. Sasa sisi tunaimba tu tunagusa mambo mengi, mipango mingi ambayo haina *focus na focus* yenyewe ambayo tunayo tumesema sisi kilimo ndio uti wa mgongo lakini hatukipi *priority*.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini Mheshimiwa Waziri ataamua sasa tutoke hapa tulipo akaacha *legacy* katika nchi hii kwa kipindi hiki alichonacho, akajikita katika kilimo kukitengeneza kilimo? Kilimo sio tu kimekuwa hakitukomboi Watanzania, bali pia kimekuwa kikishuka. Kilimo kimeshuka kutoka asilimia 2.3 mwaka 2015 mpaka asilimia 0.3...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti ili tuweze kumsikia mwenzetu anavyochangia, punguzeni sauti ziwe chini kidogo.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kilimo kimeshuka kutoka asilimia 2.3 mwaka 2015 mpaka asilimia 0.3 mwaka 2016. Sekta ya Kilimo ambayo tegemeo kwetu na ambayo inaweza kututoa kwenye hali tuliyonayo, sekta ya kilimo ilitengewa bilioni 101 hadi sasa zilipelekwa bilioni 3.3 tu sawasawa na asilimia 3.31.

Mheshimiwa Spika, mifugo na Uvuvi vilitengewa bilioni 15.8 hadi sasa zilitolewa bilioni 1.2 tu sawa na asilimia nane, sasa tunavukaje hapa? Fedha za maendeleo katika sekta hii ya kilimo ambayo ni kilimo, mifugo na uvuvi na shughuli zote zinazohusiana na uvunaji na kilimo, zilitolewa chini ya asilimia 97 katika Wizara hii. Sasa tutaongea sana, tutapanga sana lakini hatuwezi kutoka hapa tulipo kwa kutokuwekea kilimo kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 nchi yetu ilianzisha Benki ya Kilimo ambayo ilitarajiwa kupewa trilioni moja, lakini Benki hii mpaka sasa imepewa bilioni 60 tu. Benki hii ili-*target* kuwapa mikopo wakulima 200,000 kila mwaka, lakini mpaka sasa ni wakulima 3,700 tu wameweza kupata mkopo. Kwa hali hii hatuwezi kuvuka hapa tulipo, umaskini bado utaendelea kuwa pamoja nasi. (*Makofi*)



NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa nane wa kitabu cha Mpango kimesema kwamba baadhi ya shughuli za kiuchumi zilishindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji ikiwemo sekta ya kilimo ambayo ni dhahiri sasa tunajua kwa sababu gani ambayo iliweza kukua kwa asilimia 2.1 tu. Shirika la Chakula Duniani (FAO) 2014 ilisitiza tena kwa nchi maskini za Afrika tujikite katika kilimo, kilimo ndio kinachoweza kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jopo hili la wataalam limesema kwamba tuendeleo kushikilia Maputo *Declaration* ambayo tuli-*commit* Watanzania kutenga *ten percent* ya bajeti yetu kwenye shughuli za kilimo na kuhakikisha pia kwamba kilimo hiki angalau kinakuwa kwa *six percent* kwa mwaka, sisi tupo chini ya hapo, tunaongelea *two point, one point*, hatuwezi kuvuka. Naomba bajeti iangaliwe upya iweze kujikita katika hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mifano iko mingi ya nchi ambazo ziliweza kuendelea, hata Wakoloni wetu Waingereza miaka ya 1800 walikuwa na *agricultural revolution* ndio wakafika hapo sasa hivi, sasa kwa nini sisi hatuamki wakati tuna mifano na tukijua kwamba *population* yetu asilimia kubwa ni hawa wakulima? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia katika ukurasa wa saba wa kitabu cha Mpango namba 12 imekiri kuwa mfumko wa bei ulikuwa pia umechangiwa na ukame au kuchelewa kwa msimu wa mvua. Wabunge wengi ni Wabunge wa maeneo ya vijijini ambao wanashughulika na kilimo na Wabunge wengi tumeona njaa mwaka huu na bado wananchi wetu wanalia kwa njaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasisitiza kwamba Serikali sasa inabidi iwekeze pia kwenye sekta ya maji, kwenye *irrigation* hatuwezi kuvuka kwenye kilimo cha sasa hivi cha kutumia jembe na kutegemea mvua tukasema kwamba tutaweza kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilipatwa na kigugumizi,

nimepatwa na bumbuwazi kuona kwamba *issue* ya *road license* malipo yake yamepelekwa kwenye lita ya mafuta. Wiki kadhaa zilizopita humu Wabunge karibu asilimia kubwa waliosimama kwenye sekta ya maji, walikuwa wanapendekeza Sh.50/= kwenye kila lita ya mafuta kwa ajili ya Mfuko wa Maji, sasa *road license* mnajaribu kumbeba nani katika hili, inamsaidia nani? Ile tozo ya shilingi 40 kwa kila lita inakwenda kujenga barabara, barabara inamsaidiaje Mtanzania ambaye anakufa na njaa?

Mheshimiwa Spika, kwa nini hiyo hela wasitafute *means* nyingine za kuwasaidia hao wenye kudaiwa hiyo *road license* au malimbikizo yao, badala ya kuwapongeza kwa kuweka kwenye lita ya mafuta. Mheshimiwa Shabiby yeye anakuja na *concept* yake kwamba inakuwa ina unafuu lakini haina unafuu, inakwenda kuwakandamiza wakulima, inaenda kutukandamizi sisi, maji ni uhai tutaendeleaje hivi?

Mheshimiwa Spika, hii naomba iangaliwe upya iwe *reviewed* ile Sh.50/= ambayo ilikuwa inakwenda kwenye Mfuko wa Maji iendelee kuwepo kwenye Mfuko wa Maji kwa sababu hii ndiyo itakayotukomboza sisi, bila maji maendeleo yanapatikana wapi? Bila maji kilimo hakipo, hatuwezi kuwa tunategemea kilimo cha mvua wakati kuna mabadiliko ya nchi ambayo hata sisi tumeshindwa ku-*accommodate*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, dhima ya bajeti ya mwaka wa 2017/2018 imejikita katika kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii. Naomba tu niwaachie hili swali, kiviipi? Hapo tu, naomba mkajitafakari kwa hapo, najua mna timu yenu ya wataalam, Mawaziri najua mpo vizuri, naomba mtujibu, kiviipi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 19 na 20 wa kitabu cha Mpango kimegusia suala *very briefly* mabadiliko ya maisha ya watu. Hotuba ilipogusia hili naona ilijzungusha bila kutuambia haijajielekeza umaskini utashuka au utashushwa kwa kiwango gani? katika nchi yetu na nafikiri walishindwa kujieleza utashuka kwa kiasi gani kwa sababu

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wameshindwa kushika zile sehemu muhimu ambazo zitatutoa wananchi kuondoa umaskini; kilimo na maji, elimu na vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopita ilitekelezwa kwa chini ya asilimia 30 na miradi ya maendeleo haijawahi kuzidi asilimia 40. Nafikiri hapo ndio maana Mheshimiwa Waziri alipata kigugumizi cha kuweza kutueleza kwa umakini, umaskini unaweza ukaondoshwaje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:**Ahsante.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Immaculate Semesi Sware. Mheshimiwa Aisharose Matembe hayupo, nafasi yake nampa Mheshimiwa David Mathayo David na atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu lissu, Mheshimiwa Subira Mgalu ajiandae.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Fedha amesoma bajeti vizuri sana na nilikuwa namwangalia kwa makini hata maji alikuwa haombi na sauti yake imekwenda vizuri bila kupungua mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza, kwanza bajeti hii ni ya kihistoria, mimi nimekaa hapa miaka12 lakini ndio mara kwanza kusikia bajeti inayoeleweka kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa hiyo ni bajeti ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, hii ni mara ya kwanza sera za

viwanda, uanzishaji wa viwanda na *ku-favour* viwanda imejikita moja kwa moja kwenye bajeti ya Serikali. Bajeti hii imetoa majibu ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, bajeti hii vilevile inaonesha ni jinsi gani *National Development Plan* ilivyokuwa *incorporated* kwenye bajeti hii ya mwaka huu pamoja na dira ya Taifa ya mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii pia imepunguzia wakulima na wafugaji ambao tunasema kwamba ni walala hoi wamepunguziwa kodi mbalimbali, hususani kwenye kilimo kwenye chakula kwenye madawa kwenye pembejeo mbalimbali, kwa hiyo ni bajeti ambayo inastahili kuungwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaeleze tu Waheshimiwa Wabunge ambao ni wanya kwa maana ya kwamba wameingia wale asilimia 70 kwamba wasishangae sana kupata kusikia Wapinzani wanaendelea kupinga bajeti hii. Hata siku moja Wapinzani hawajawahi kuunga mkono isipokuwa na kumbuka Mzee John Momose Cheyo na Mzee Augustino Lyatonga Mrema ndio walikuwa Wapinzani wa kweli na ndio waliokuwa wanasema ukweli, kama Mheshimiwa wa Chama cha *CUF* ambaye ndio amemaliza sasa hivi muda mchache uliopita kuongea. Ameongea vizuri kiungwana, lakini wenzetu pale hawakumpigia hata makofi kwa sababu alikuwa anaongea vitu vya ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba Wapinzani kazi yao ni kupinga na sisi kazi yetu ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano kwa sababu sisi ndio tulioshinda uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wapinzani hawa kwa wale wasiowajua ni watu ambao wanabadilikabadilika, wamekuwa ni kinyonga. Kwa mfano, mwaka 2015 wakati Mheshimiwa Lowassa yuko Chama cha Mapinduzi walikuwa wanasema ni fisadi, alivyohamia kwao wakampa kugombea Urais, sasa si wanabadilikabadilika hao. Sasa hivi tunazungumzia mikataba mbalimbali lakini wasisahau kwamba Mheshimiwa Sumaye ambaye alikuwa Waziri Mkuu

kipindi hicho ndio alikuwa msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni alikuwa hapa wakati mikataba hiyo inaingiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii presha ambayo...

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, hii presha ambayo Wapinzani wanaiona ni kwa sababu wanajua kwamba 2020 tunapita bila kupingwa na viti vyao vitapungua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mathayo naona kuna Mheshimiwa amesimama. Tafadhali nakupa nafasi

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, naomba ulinde muda wangu.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nataka tu kumpa mchangiaji taarifa kwamba Sumaye ndiye alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza kuunda Tume ya Madini ya Jonas mwaka 2004, ambayo Serikali mpaka sasa haikutekeleza maelekezo ya Tume hiyo. Kwa hiyo, hii Tume siyo ya kwanza ilishaundwa na Waziri Mkuu Sumaye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mathayo David unapokea hiyo taarifa?

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa hiyo kwa sababu akiwa kama Waziri Mkuu alitakiwa ahakikishe kwamba inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajenda ya Wapinzani kwa sasa walikuwa wanasema; maana sasa hivi wanasema kwamba bajeti hii ya Serikali haitekelezeki, lakini ajenda yao ya hapo nyuma, miezi miwili iliyopita walikuwa wanasema demokrasia imebanwa. Sasa hivi wamebadilika wanasema bajeti haitekelezeki, wakitoka hapo wataanza kusema tena demokrasia imebanwa, lakini embu waulize, sisi tangu

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mwaka 2000 mpaka leo tumebadilisha Wenyeviti wa Chama cha Mapinduzi watatu, Mheshimiwa Mkapa, Mheshimiwa Kikwete na Mheshimiwa Magufuli, wao bado wako na Mbowe sijui mpaka miaka mingapi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimwona Tundu Lissu yeye ndio Mwenyekiti wa CHADEMA nitasema kweli mna demokrasia, lakini kama CHADEMA bado iko Moshi bado. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu ndio mwongaji unayefuata naomba uvumilie tu utatumia dakika zako, maana yake wewe ndiye unayefuata.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ni taarifa wala sio kitu kingine.

**SPIKA:** Baada tu ya hapo unafuata wewe.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ni taarifa nataka kutoa taarifa.

**SPIKA:** Haya taarifa fupi.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, naomba ulinde muda wangu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, atakulindia muda wako.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu kule Pwani kule ukisikia yeleeeee! ujue dawa imeshaingia. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lissu kwa kifupi.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, taarifa fupi.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, Wapinzani wanasema kwamba Serikali itapata wapi trilioni 31.7 someni bajeti muone vyanzo vya mapato, kwa nini hamsomi? Kama...

## TAARIFA

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu kumpa taarifa fupi msemaji kuhusu hili ambalo amelisema la Wenyeviti wa Vyama vya Upinzani kukaa muda mrefu. Taarifa yenyewe iko hivi, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Rais wa TANU kuanzia mwaka 1954 mpaka 1977 na akawa Mwenyekiti wa CCM kuanzia mwaka 1977 mpaka 1992. Kwa hiyo nani ambaye...

**MBUNGE FULANI:** Yaani unataka kumfananisha Nyerere na Mbowe!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nani ambaye amekaa madarakani muda mrefu kati ya huyu aliyekuwa madarakani miaka 40. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mathayo endelea kuchangia nakulinda.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Tundu Lissu akumbuke kwamba tulikuwa chama kimoja cha Chama cha Mapinduzi peke yake. Pili, kujikosoa siyo udhaifu bali ni dalili ya kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shazia huwa inashona gunia, lakini shazia ili ishone gunia inatungwa uzi huku nyuma, sasa wasubiri 2020 tunawatunga uzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha ajabu sana kuona kwamba Mheshimiwa Rais wetu, kwanza amefanya makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nitayarudia tu halafu mtaona hamna hata mmoja atakayepiga makofi kule. Kwanza,

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ameondoa watumishi hewa zaidi ya 19,700. Pili, ameondoa watumishi wasio na vyeti 9,900; wanafunzi hewa walioondolewa kwenye Bodi ya Mikopo 3000; kugharamia elimu ya msingi hapo nyuma haikuwepo hii, elimu ya msingi sasa hivi inagharamiwa bila malipo, ukusanyaji wa kodi uliongezeka kuanzia bilioni 800 mpaka bilioni 1200 na zote hizo zinakwenda kwenye shughuli ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia ameweza kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma, maamuzi haya yalifanyika mwaka 1973 lakini yamefanyika leo miezi 18 tayari Mheshimiwa Magufuli ameweza hiyo kazi. Ujenzi wa reli ya *standard gauge* haijawahi kutokea kwa muda mfupi namna hii. Kununua ndege mbili na zingine zinakuja na akina Mbowe ndio wanazipanda zinakuja, ni makubwa aliyofanya Mheshimiwa Jemedari wetu Dokta John Pombe Magufuli, kwa nini hampigi makofi? Hizi ndege mtapanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeshinda kwa kukubaliana na Uganda kujenga bomba refu kutoka Hoima mpaka Tanga, Wakenya nao walitaka lakini walishindwa kwa sababu tuko vizuri. Vilevile meli mbili zimenunuliwa kule Nyasa na wanazitumia wananchi na tumefanikiwa kuzuia makinikia kwenda nje na tumeshajua hela tuliyokuwa tunaibiwa. Mambo yote haya aliyoyafanya Mheshimiwa Rais anastahili hongera, anastahili kuombewa na viongozi, anastahili kuombewa na Wakristo na Waislamu ili aweze kuwa na afya na maisha marefu ili aendelee kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika...

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, naomba muda wangu ulindwe.

**SPIKA:** Naomba mngevumilia tu kidogo, nina wachangiaji watatu wa mwisho ambao ningependa nao wapate nafasi pia.



**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, taarifa fupi tu.

**SPIKA:** Naomba tuvumilie amalizie muda wake naomba sana. Mheshimiwa malizia, bado dakika moja tu amalize.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba ulinde muda wangu hiyo dakika moja nitasema hivi. Tulivyotoza kodi asilimia sifuri ya kusafirisha mizigo nje ya nchi ....

**MBUNGE FULANI:** Wewe si ulikuwa Waziri?

**SPIKA:** Waheshimiwa sasa hiyo ni fujo, naomba sana wanaoongea wapewe nafasi.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, tunaomba kudhibiti kuwe na *tracking system* inayodhibiti magari yanayosafirisha mizigo, lakini kwenye ada ya *registration* kwa mara ya kwanza tunaomba angalau iongezeke laki moja kwa kila *capacityya engine* kwa sababu hela iliyowekwa ya ongezeko la 50,000 ni hela ndogo sana, kwa sababu wana-*register* mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, hii ada ya magari iliyofutwa tunaomba ziongezeke Sh.50/= kwa kila lita ili tuweze kupeleka maji vijijini jamani, ndio maamuzi haya yatatusaidia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mathayo David, sasa ni Mheshimiwa Tundu Lissu na atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kusema kwamba, mimi sio mtaalam wa maandiko matakatifu lakini kuna

mahali katika Biblia kunasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa, na nchi yetu inaangamia kwa sababu ya kukosa maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, asubuhi umesema kwamba haya masuala ya madini yanahitaji semina. Hilo ni jambo muhimu sana, kwa sababu hoja hii inahitaji maarifa sana haiwezi ikajadiliwa sawasawa kwa hizi dakika tano au kumi.

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite katika masuala ya madini kwa sababu ambazo ziko wazi kabisa. Kamati ya Rais ya Profesa Osoro ya jana na Kamati ya Profesa Mruma ya mwezi uliopita, siyo ripoti za kwanza kuzungumzia, kuchunguza matatizo ya kwenye sekta ya madini katika nchi hii, siyo za kwanza na Rais Magufuli siyo wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, Rais Mkapa aliunda Kamati iliyoongozwa na Jenerali Mboma inaitwa Kamati ya Mboma kuchunguza matatizo ya sekta ya madini, hasa madini ya vito vya thamani 2002. Mwaka 2004 Waziri Mkuu Fredrick Sumaye, Serikali ya Mkapa iliunda Kamati ya Dkt. Jonas Kipokola, kuchunguza matatizo ya sekta ya madini, taarifa yake ni ya Agosti, 2004.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliofuata 2005 Rais Mkapa na Serikali yake waliunda Kamati ya Bukuku alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kuchunguza matatizo ya sekta ya madini. Mwaka 2006 miezi michache baada ya Rais Kikwete kutawazwa kuwa Rais akaunda Kamati ya Lawrence Masha bahati nzuri nimekuja na taarifa yake hii hapa. Kamati ya Lawrence Masha kuchunguza Sheria za Madini, Sheria za Kodi, Sheria za Fedha, mikataba ya madini, kila kitu cha madini, taarifa hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 baada ya mgogoro wa Buzwagi hapa Bungeni, Rais Kikwete aliunda Kamati ya Jaji Mark Bomani hii hapa, Kamati ya Jaji Mark Bomani taarifa yake ni ya Aprili, 2008. Kamati ya Osoro na Kamati ya Profesa Mruma ni Kamati ya sita kuundwa kushughulikia masuala ya madini. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nimekuja na muhtasari wa Kamati ya Profesa Osoro ya jana hii hapa na kwa sababu nafahamu taarifa zote hizi za Kamati zingine, naweza nikawaambia Waheshimiwa Wabunge, hadidu za rejea za Kamati ya Mruma na Osoro ni zilezile zilizokuwa hadidu za rejea za Kipokola, za Bukuku, za Lawrance Masha na za Kamati ya Bomani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo yake, *findings* na *recommendations* ziko hapa kwa kiasi kikubwa ni *findings* na *recommendations* zilezile zilizokuwa kwa Bukuku, zilizokuwa kwa Kipokola, zilizokuwa kwa Masha, zilizokuwa kwa Bomani, hazijawahi kutekelezwa kwa sababu mnayoifahamu.

Mheshimiwa Spika, watu ambao wameuza madini ya nchi hii walipitisha sheria kwenye Bunge hili na ndio maana inashindikana na hii ya Dkt. Magufuli, nazungumza Mungu anasikia na watu wasikie, mtaniambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii ya jana, wamependekeza watu fulani fulani washughulikiwe, Mawaziri, Makamishna, Mwanasheria Mkuu Bwana Chenge, akina Ngeleja, akina nani, naombeni niwaambieni kitu Waheshimiwa Wabunge ili muwe na maarifa. Mtu wa kwanza kusaini mikataba ya madini na leseni za madini tarehe 5 Agosti, 1994, Meja Jakaya Mrisho Kikwete, leseni ya Bulyanhulu hii inayopigiwa kelele leo, Leseni ya Bulyanghulu ya tarehe 5 Agosti, 1994 ilisainiwa na Jakaya Kikwete akiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini, hakuwa na kinga ya Urais wakati ule, hana kinga ya Urais leo kuhusiana na masuala aliyoyafanya wakati hajawa Rais. Hana! Alisaini leseni siyo ya Bulyanhulu peke yake, pia ya Nzega na ya Geita. *Golden Pride* - Nzega na *Geita Gold Mine* zina sahihi ya Kikwete, anaponaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mapendekezo haya anaponaje? Kama mnataka kweli kushughulikia watu walioshiriki mambo haya, mbona mnachagua chagua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi leseni na hizi sheria tatizo kubwa tangu mwaka 1999 wenye kujua tumesema, tatizo kubwa ni sheria za Tanzania. Sisi ni wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa kulinda uwekezaji (*The MIGA Convention*). Tumesaini mikataba na nchi moja moja zenye wawekezaji Tanzania, nchi 26, mikataba ya kulinda Wawekezaji hawa. Tumetunga Sheria ya Madini yenyewe, Sheria za Kodi za mwaka 1997, Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997. Hizi za 1997 zilipitishwa siku moja tarehe 26 Machi, *under Certificate of Urgency*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kuna mchango utakaoutoa kama Spika na utakumbukwa, upige marufuku hii habari ya *Certificate of Urgency* kwenye utungaji sheria, inatuletea mabomu. Sheria za Gesi Asilia na mafuta mlizotufukuza hapa mkazipitisha ni mabomu matupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesoma hizo takwimu mlizoambiwa na Profesa Mruma na Profesa Osoro za madini ambayo yameondoka. Mimi sitasema sana, nawaombeni kama mnaweza, mlinganishe takwimu za utajiri wa madini zinavyozungumzwa kwenye Kamati ya Bomani na mlinganishe na utajiri unaozungumzwa kwenye Kamati ya Profesa Osoro, halafu mniambie nani ni mwongo kati ya hizo mbili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu dakika zako zimeisha.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2017/2018.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa Tume mbalimbali zilizotajwa muda mfupi uliopita, lakini ripoti zao si Msahafu wala Biblia ambazo haziwezi kubadilishwa. Kwa ujasiri alioonesha kwa kipindi kifupi Mheshimiwa Rais, kwanza cha angalau kutekeleza maamuzi ya kuhamia Dodoma, tangu mwaka 1973, lakini uamuzi wa kuanza ujenzi wa reli ya kisasa, uamuzi wa kuwaondoa watumishi wenye vyeti feki, uamuzi wa kuondoa watumishi hewa, uamuzi wa kuondoa wanafunzi hewa, naamini ripoti ya Profesa Osoro na Profesa Mruma zitafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti hiyo tumefuatilia wengi, kwa kuwa Mheshimiwa Spika, ulihudhuria na kwa kuwa Mheshimiwa Spika ulitoa kauli ya kulitaka Bunge lako kuwa tayari kupokea maelekezo na sheria mpya zitakazoletwa, nina imani mwaka huu mwarobaini wa ripoti mbalimbali umepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile ripoti ya jana ya Profesa Osoro na ripoti ya Profesa Mruma zilikuwa na mambo mengi. Ukiacha mambo ya kisera, ukiacha mambo ya kisheria lakini yapo mambo ya kiutendaji yaliyosababisha hasara kubwa lazima yashughulikiwe. Kwa mfano, katika ripoti ilisema kiwango cha mrahaba kilichooneshwa kwenye hesabu za makampuni ya Bulyankulu na Pangea zilioneshwa dola za kimarekani milioni 111, wakati zilizopelekwa Serikalini kama mrahaba kati ya mwaka 1998 mpaka 2017 ni dola za kimarekani milioni 42, tofauti ya bilioni 68. Hili la kiutendaji lazima lishughulikiwe, siyo la kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ripoti imeonesha namna ambavyo wasafirishaji kupitia Wakala wa Meli walivyofanya utapeli wa kutisha, takwimu zinatofautiana baina ya hati za kusafirisha meli na hati za Wakala wa Meli, hili ni jambo la kuachwa? Haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naunga mkono bajeti hii na naunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais. Naunga mkono bajeti hii kwa sababu, kwanza bajeti ina nia ya kumwondoa Mtanzania kwenda kwenye kipato

cha kati. Pili, bajeti imewagusa Wanawake ninaowawakilisha kitendo cha kufuta VAT kwenye chakula cha mifugo inatosha kabisa mimi kuunga bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha bajeti hii kuondoa VAT kwenye vipuli vya viwanda ambako Mkoa wangu unaongoza kwa viwanda kwa sasa nina kila sababu ya kuunga bajeti hii. Pia kitendo cha bajeti hii kutoa *motor vehicle licence* ya mwaka mzima na kupendekeza tozo ya Sh.40/= nikiwaona wanawake wengi wananunua maji kwa elfu moja, kwa elfu mbili, kwa elfu tano dumu, naamini wana uwezo wa kuhimili tozo hii ya Sh.40/= endapo sehemu ya tozo hii itahamishwa kwenye Mfuko wa Maji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napongeza namna gani Mheshimiwa Rais wetu anavyosimamia uboreshaji wa mapato. Amesimamia maboresho ya mtambo wa *TTMS* wa kurekodi dakika zote za simu, tunaona mapato ya simu yameongezeka. Amesimamia uanzishaji wa mfumo wa kukusanya mapato kielektroniki, amesimamia hata kutembelea *data center* na ameelekeza makampuni yote ya simu yaende kujisajali Dar es Salaam *Stock Exchange*.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, naomba nipendekeze, Waswahili wanasema ukiumwa na nyoka, ukiona nyasi unastuka. Kwa kuwa, tumeona makampuni mengi ya nje hata taarifa zilizotolewa zinaonesha makampuni mengi ya nje yanatutapeli kupitia *transfer pricing*, nishauri kwenye soko la Dar es Salaam *Stock Exchange*, makampuni ya simu, Serikali ilete mapendekezo ya kutafsiri upya maana *listed shares* ili Serikali yetu ipate fursa ya kuangalia miamala ya makampuni haya hata ile ambayo *shares* zake nyingi zinatawaliwa na wageni.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Kampuni ikiwa *registered* Dar es Salaam *Stock Exchange* ikiuza *share* zake kwa asilimia 25 ili zile *share* zote Serikali iwe na nguvu lazima tubadilishe maana halisi ya *listed shares* ili iende kwenye zile *share* za makampuni. (Makofi)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhehimiwa Spika, sambamba na hilo, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa ujenzi wa *standard gauge* kama nilivyosema. Hata hivyo, nashauri suala zima la kufuta VAT kwenye vipuri liende sio tu kwa viwanda vilivyotajwa vya mafuta peke yake, lakini viguse viwanda vya usindikaji wa korosho, Mkoa wa Pwani tunalima korosho, viguse pia viwanda vya kuzalisha mafuta ghafi hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini nimalizie kama dakika zangu zipo kwenye suala zima la nia ya Serikali ya kufungua *Escrow Account* kwa ajili ya makampuni yanayotumia sukari ya viwanda. Niombe Serikali ilitazame upya suala hili, makampuni yale yenye viwanda vya kutengeneza vinywaji baridi kwa kweli wamezidiwa, pesa zao nyingi hazijarudishwa kiasi cha bilioni 20, imesababisha viwanda hivi kupunguza wafanyakazi, inasababisha viwanda hivi kupata tabu katika uendeshaji wa shughuli zao. Naomba Serikali itazame upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ione namna ambavyo itatusaidia wakazi wa Pwani viwanda hivi ambavyo vimeanzishwa vingi na namna ya kutusaidia jinsi ya kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu bajeti hii Mheshimiwa Waziri amesema Mama Lishe watatambuliwa sasa hivi, wauza mboga ndogondogo watatambuliwa. Imani yangu utambulisho huu utakwenda sambamba na huduma za kifedha, utakwenda sambamba na uwezeshaji na naamini kupitia Baraza la Uwezeshaji la Taifa, wanawake wengi watafikiwa, bodaboda wengi watafikiwa kwa kuwa watakuwa na utambulisho rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa spika, mwisho, ni kuhusu Serikali zetu za Mitaa. Niombe sana kwa Mheshimiwa Waziri, nia ni njema ya kufanya mapato yote yakusanywe na Serikali Kuu, lakini niombe urejeshwaji wa mapato hayo uende kwa wakati. Halmashauri zetu nyingi zitashindwa kujiendesha endapo makusanyo yatakayokusanywa kupitia *property tax*, kupitia

vyanzo vingine vya mabango ambavyo vimekwenda Serikali Kuu kwa nia njema ya kuongeza hayo mapato yatakuwa hayarejeshwi kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushukuru kwamba kwa upunguzaji wa *produce cess* kwa wakulima wetu, kwa kweli ni suala ambalo ni la msingi. Kila siku tulikuwa tunalisemea lakini namna ambavyo Serikali mmelishughulikia. Mheshimiwa Waziri nakupongeza, bajeti hii imesikiliza maoni ya Kamati, bajeti hii inamgusa mwananchi wa kawaida, bajeti hii imemgusa mkulima na bajeti hii imemgusa mwanamama wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru, karibu orodha nzima ya leo wamepata nafasi na kama kuna mmoja au wawili ambaye hakuwepo au jina lake halikupatikana, basi tutajitahidi kesho kwa sababu tunaendelea na mjadala huu.

Niwajulishe tu Waheshimiwa Wabunge mliopo na wale ambao wako nje ya Dodoma kwa sasa, ni vizuri tuanze kuambiana kwamba tarehe 20 Jumanne ijayo ndio itakuwa ile siku muhimu kabisa Kikatiba ambayo tutakuwa tunapitisha bajeti yetu kwa kupiga kura jina moja hadi lingine. Kwa hiyo, kwa hitaji hilo la Kikatiba nawaomba sana na tutaendelea kuwakumbusha kwamba tarehe 20 mwezi huu wa Sita Jumanne ijayo sote kabisa tuwepo hapa, hiyo Jumanne itakuwa ndio siku ambayo tutashughulikia suala zima la bajeti yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo kipekee nimtambue Hope mtoto wa Mheshimiwa Manyanya popote pale alipo. Nimeamua kumtambua kwa sababu huyu hapo anapunga mkono, binti yetu ni mlemavu wa miguu yote miwili lakini amejitahidi ameweza kumaliza *form six* majuzi hapa, hongera sana Hope. Pamoja na rafiki zako karibuni sana, huo ni mfano mzuri sana wa bidii, kujituma na kujitoa



lakini pia hongera mama kwa kutomchelewesha mtoto kumpeleka shule. Huyu ni mziwanda wa Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kuhusu ile futari mara tu baada ya hapa ambayo imeandaliwa Tanzania *Media Foundation* kama nilivyowaeleza na tunakaribishwa wote kabisa, hata wale Wasukuma wasiojua kukunja miguu kuna viti vimewekwa kule, kwa hiyo msiwe na wasiwasi kuna viti vimewekwa kwa ajili yenu. Akinamama mnaoona aibu kula mbele ya wanaume kuna sehemu ya akinamama na wale wenzangu mimi kuna sehemu yenu pia. Maandalizi yote ni mazuri sana na mara tukimaliza hapa nawatia moyo wote tukitoka hapa twende pale.

Waheshimiwa Wabunge, mambo haya ya kijamii yanatusaidia kuwa pamoja zaidi, hata hisia hizi za tofauti zinapungua na zinakwisha, tunajikuta sisi ni wamoja zaidi na ni Watanzania wote. (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho ambalo ningependa kusema, Mheshimiwa Tundu Lissu alishauri kwamba nijitahidi kama Spika nisipokee mambo ya sheria ambazo zinakuja chini ya hati ya dharura. Ushauri wake ni ushauri wa maana tu na kama mnavyojua hatufanyi shughuli yoyote hapa mpaka Kamati ya Uongozi imekaa na kupitisha huwa sio suala la Spika peke yake. Hata hivyo, ningependa kusema yafuatayo:-

Kwa wakati wowote ule katika hili jambo la Madini na kadhalika na gesi na mafuta, Serikali ikituletea mabadiliko ambayo tunatakiwa tuyafanyie kazi kwa haraka *under Certificate of Emergency* tutafanya hivyo. Kwa sababu moja tu, tunaibiwa sana, sasa kama kuna sheria inasababisha tunaibiwa kwa kweli ikiletwa hapa hiyo ni hapo hapo ili mrija huo tuukate kabisa. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hizi sheria zingine za kilimo cha karanga Kongwa hizo zitasubiri tu, tutawaambia akina Jenista hii haraka ya nini, lakini zikija hizi za kushughulika na

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

hili ninyi wenyewe mmesema sijui Tume ya nani, sijui Tume ya nani na hii nayo ishindwe, haiwezekani! Sisi kama Bunge ni sehemu ya historia hii, tuna- *role* yetu ya *ku-play*, tukisema tu Mheshimiwa Rais Magufuli peke yake ndiye afanye hiki na hiki, kuna mambo hawezi kufanya. Kuna mambo hawezi kufanya kama hayo ya kisheria, kama inabidi sisi tubadili sheria ili afanye, lazima na sisi tumwezeshe, au sio jamani? (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba sasa niwashukuru sana kwa michango yote ya leo, tunaendelea na kesho, tunaendelea vizuri na kwa kweli tuendeleo hivi hivi.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 14 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*